# Nipashe

Alhamisi Aprili 2, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580195

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




## Majaliwa asema atakayethibitika na corona kutangazwa bila kujali cheo


UKURASA 3





UKURASA 13

TISHIO LA CORONA

# Wagojwa wafikia 20




• **Tito** wa LHRC afichua hatari mahabusu, Mchungaji ataka adhabu kali wakaidi, mabweni kuweka washukiwa karantini... *Endelea Uk. 2, 4, 22, 23, 26*



**BAA LA CORONA**

**Maambukizo 783,360 ya virusi vya corona yamethibitishwa mpaka jana duniani, vifo vilivyotokea kwa ugonjwa huo ni 37,203 na nchi zilizoathirika ni 206. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO)**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## WB yatoa mkopo wa Dola mil. 500 kukuza elimu

UKURASA 3




Dereva wa bodaboda anayeegesha katika kijiwe cha Nyahanga, mjini Kahama, mkoani Shinyanga, akimnawisha mikono mteja wake, jana, kabla ya kumpeleka safari yake, kwa kutumia dumu la maji alilofunga nyuma ya pikipiki, kama tahadhari ya maambukizi ya virusi vya Corona. **PICHA: SHABAN NJIA**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Makonda aruhusu bodaboda, bajaji kuingia katikati ya jiji

UK. 2


MICHEZO YANGA YATUA AS VITA KWA KISINDA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Hotuba upinzani yagonga mwamba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limezuia kusomwa kwa maoni ya Kambi ya Upinzani katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa madai kuwa yamevunja kanuni za kudumu za bunge huku likisisitiza kuwa aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu hadai hata shilingi moja.

Aidha, limetoa ufafanuzi wa tuhuma za Kiongozi wa Upinzani bungeni, Freeman Mbowe, kunyanyaswa na kukosa huduma alizopaswa kupewa na Bunge ikiwamo nyumba ambayo aliikataa na kumpa Lissu.

Zuio hilo lilitolewa jana na Spika Job Ndugai baada ya maoni ya Kamati mbalimbali za kudumu za Bunge kuwasilisha taarifa zao. Maoni ya kambi hiyo yalitakiwa kusomwa na Mbunge wa Kawe (Chadema), Halima Mdee kwa niaba ya Mbowe.

Alisema madai yaliyotolewa ni uzushi na mengine yanavunja kanuni za Bunge.

"Tuhuma ambazo hazina sababu hatuzitaki. Mara oooh Tundu Lissu hajalipwa mishahara yake wala posho. Tundu Lissu hadai hata shilingi moja na hata mshahara mmoja, muulizeni aseme tena. "Kuna madai Kiongozi wa Upinzani ananyanyaswa, huduma hapati, gari lipo na hatujapata magari mapya tutayapata kupitia bajeti hii kwa ajili ya Bunge la 12, gari lilikuwapo na alikuwa analitumia yeye,"alisema.

Aidha, alisema suala hilo la gari ni kati yake na Katibu wa Bunge na si mambo ya kupeleka bungeni. "Nyumba hana, nyumba ipo ambayo inahudumiwa na bunge na ni ile aliyoikataa tangu mwanzo na badala ya yeye kukaa akampa Tundu Lissu. Ile nyumba aliyokuwa anakaa Lissu si nyumba ya mnadhimu wa kambi ya upinzani bali ni nyumba ya kiongozi wa upinzani kwa mujibu wa taratibu zetu.

"Lakini aliikataa akaenda kukaa 'site two' kwenye nyumba aliyoitaka yeye mwenyewe. Pamoja na hayo zile huduma ambazo alipaswa kupewa, zinatolewa huko anakoishi, ikiwamo mhudumu wa usafi na upishi, ulinzi, umeme na maji," alisema.



Mfanyakazi wa Idara ya Afya katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, akipulizia dawa ya kuzuia virusi vya corona katika magari ya abiria yanayofanya safari za maeneo ya ndani na nje ya Manispaa hiyo, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wagonjwa wa corona wafikia 20

**Na Mary Geofrey**

SIKU moja baada ya kuripotiwa kwa kifo cha mgonjwa aliyekuwa na maambukizi ya virusi vya corona (Covid-19) , idadi ya wagonjwa waliothibitishwa kuwa na maambukizi ya virusi hivyo imeongezeka na kufika 20.

Mgonjwa mmoja aliyekuwa katika kituo cha matibabu cha Temeke, jijini Dar es Salaam, amethibitika kupona maambukizi corona na ameruhusiwa kurudi nyumbani.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na kusema mgonjwa aliyegundulika kuwa na virusi hivyo ni raia wa Marekani.

Ummy alisema mgonjwa huyo mwanamke (42), alikuwa karibu na mtu aliyesafiri nje ya nchi na baadaye kuthibitika kuwa na maambukizi ya virusi hivyo aliporejea nchini.

"Wizara ya Afya inathibitisha kuwapo kwa kesi mpya ya maambukizi ya virusi vya corona nchini iliyopatikana jijini Dar es Salaam. Mgonjwa huyu ni raia wa Marekani," alisema Ummy. Alisisitiza jumla ya kesi za wagonjwa waliobainika nchini zimefika 20 na kati yao 17 wanaendelea na matibabu.

Alisema idadi ya wagonjwa waliokwisha kupona ugonjwa huo ni wawili baada ya mmoja kuruhusiwa juzi na wa kwanza kuwa na maambukizi hayo ambaye aliruhusiwa wiki iliyopita.

Juzi aliripotiwa mgonjwa mmoja wa corona, mwanaume (49) na kufariki dunia katika kituo cha matibabu ya wagonjwa wa corona kilichopo karibu na Hospitali ya Mloganzila, jijini Dar es Salaam, wakati akipatiwa matibabu.

Ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na homa ya mapafu, ulianza kubainika nchini Machi 17, mwaka huu, baada ya mgonjwa mmoja mkoani Arusha aliyetokea nje ya nchi.

Serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo, ikiwamo kuzifunga shule zote nchini kuanzia za msingi hadi kidato cha sita na vyuo vikuu na vya ufundi kwa siku 30 kuanzia Machi 17, mwaka huu.

# Makonda aruhusu bodaboda, bajaji kuingia katikati ya jiji

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameruhusu pikipiki za miguu mitatu maarufu kama bodaboda na bajaji kupeleka abiria katikati ya jiji mpaka hapo ugonjwa wa Corona utakapodhibitiwa nchini.

Pia amewaomba wenye nyumba na maeneo ya biashara kupunguza bei ya kodi kwa asilimia 50 kwa kipindi cha miezi mitatu, ili kuwawezesha wananchi kumudu gharama za maisha na kulipa.

Makonda alitoa kauli hiyo jana alipofanya ziara katika stendi ya daladala ya Makumbusho, Kinondoni jijini humo.

Alisema katika kipindi hiki ambacho nchi inachukua tahadhari ya kupambana na ugonjwa huo ni vyema bodaboda zikasaidia kubeba abiria kupeleka katikati ya jiji huku akiwasisitiza madereva kuzingatia sheria.

"Masharti yaliyopo ni ya siku zote kwamba bodaboda ni lazima mzingatie sheria, ikiwa ni pamoja na kuvaa helmeti na kutokuingia kwenye barabara ya Mwendokasi. Lakini zaidi ya yote mna ruhusa ya kuingia katikati ya jiji na kuwabeba abiria wenye uwezo wa kupanda usafiri wao binafsi na kuhakikisha wanawahi kazini," alisema Makonda.

**MWENDOKASI**

Kuhusu usafiri wa magari yaendayo kwa haraka, Makonda alisema usafiri huo hauko katika mamlaka yake, lakini ameandika barua kupeleka Ofisi ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ili iingilie kati na kuruhusu magari 200 ambayo hayafanyi kazi kutokana na mgogoro uliopo.

"Suala la mwendokasi haliko chini ya mamlaka yangu, iko Tamisemi, lakini hivi tunavyozungumza watu wangu wanamalizia kuandika barua, nimemuomba waziri aingilie kati, ninafahamu yako mabasi si chini ya 200 ya mwendokasi yamepaki Ubungo, Bandari kavu."

"Nafahamu yale magari kuna mgogoro, lakini kutokana na hali tuliyonayo sasa hivi, nimemwandikia barua ya kumuomba aone uwezekano wa kuyaruhusu yale magari yaingie kwenye laini ya mwendokasi kutoka Kimara ili wananchi wasirundikane na kubanana, waingie mjini na kuchapa kazi huku wakilinda afya zao."

**KODI WENYE NYUMBA**

Makonda alisema kutokana na kuyumba kwa biashara nyingi kwa sababu ya ugonjwa huo, ni vyema wamiliki wa nyumba za biashara na nyumba za kupangisha kwaajili ya makazi kodi ikapunguzwa kwa asilimia 50 kwa kipindi cha miezi mitatu. "Kutokana na changamoto ya ugonjwa huu wa corona, baadhi ya biashara haziendi vizuri, lakini wako watu ambao wamepanga, kuanzia wanaoishi kwenye chumba kimoja, vyumba viwili, wako waliopanga kwenye ofisi au apartment,"alisema Makonda na kuongeza:

"Nimeanza kuzungumza na wamiliki wa majengo baadhi yao wamekubali, naomba kutoa rai hii kwa wenye nyumba, wenye majengo, yawe ni ofisi, 'apartment' au majumba ya kawaida au ni vyumba vya vibanda. Naomba kwa kipindi hiki cha miezi mitatu, mpunguze kodi kwa asilimia 50, kuwawezesha wananchi wamudu hali ya kawaida."

"Wananchi hawa wana changamoto ya biashara zao, biashara ya nyumba ni matokeo ya biashara inayopatikana kutokana na mtu kufanya kazi yake. Kama anaenda na ana changamoto yake huko ofisini, biashara haina wateja, tena unakuja kumuua kwenye kodi yako kudai pale pale, ninawaombeni wenye nyumba na wenye majengo wote mkubali."

Makonda alisema tayari amezungumza na wenye majengo na nyumba 50 na wamekubali kushusha kodi kwa kutoza nusu ili kumsaidia mpangaji apate akiba ya kununua chakula cha kutunza ndani hususani katika kipindi hiki.

"Siyo kwamba natangaza bei mpya ya upangaji, isipokuwa nimeomba kama ombi kwa sababu jukumu langu pia ni kusemea mwananchi wa hali ya chini ambaye hana uwezo wa kujisemea," alisema Makonda.

**WATU WABAKI NYUMBANI**

Alisema katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa ni vyema wasio na shughuli za kufanya mjini wakabaki nyumbani badala ya kuzurura kwenda katikati ya mji bila shughuli yoyote ya maana.

"Kama huna ulazima wa kwenda baa, kama unapenda muziki, unapenda disko, unataka kucheza, fungua nyumbani kwako, weka muziki, cheza na mkeo. Ni bora ukawa na afya njema kuliko ukaugua ugonjwa wa corona."

**UPOKEAJI WAGENI UWANJA WA NDEGE**

Aliwaomba wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuacha kwenda kuwapokea wageni wao wanaoingia katika uwanja wa ndege kutoka nje ya nchi na kwamba serikali kupitia watu walioandaliwa ndio wanajukumu la kuwapokea na kuwahifadhi kwa siku 14 kama maelekezo yalivyotolewa.

Aliwataka wakazi wasio na ulazima wa kutoka au kuingia Dar es Salaam wabaki katika mikoa yao.

HELIKOPTA KUPULIZA DAWA

Makonda alisema anaendelea kuchukua jitihada za kila namna kuhakikisha anawalinda wananchi wa mkoa huo ikiwamo kupulizia dawa. "Mungu akipenda tunategemea kwamba kutakuwa na helikopta za kupulizia dawa katika Jiji la Dar es Salaam, kuhakikisha tunaua wadudu wote, tumeanza na mashine ya kupulizia, tunatumia gari zote za zimamoto na gari za polisi," alisema Makonda.

# WB yatoa mkopo Dola mil. 500 elimu

**Na Romana Mallya**

BENKI ya Dunia (WB), imeidhinisha mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 kwa Tanzania kwaajili ya kuboresha elimu ya sekondari Tanzania.

Mkopo huo unaotolewa kupitia Bodi ya Wakurugenzi Watendaji wa Chama cha Maendeleo ya kimataifa (IDA), umepewa jina la 'Mradi wa Uboreshaji wa Elimu kwa Shule za Sekondari (SEQUIP)', ambao utanufaisha wanafunzi milioni 6.5, kwa kuhakikisha wanasoma na kumaliza elimu yao katika mazingira bora.

Mkurugenzi Mkaazi wa Benki ya Dunia nchini Tanzania, Mara Warwick, alisema mkopo huo ni hatua muhimu ya kukabiliana na changamoto za kielimu wanazokumbana nazo watoto.

Kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa jana jijini Washington DC, Marekani, mkopo huo ni kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata elimu ya sekondari.

Pia ilisema kuwa fedha hizo ni kwaajili ya kuboresha mazingira ya elimu kwa wasichana na kuinua uboreshaji wa elimu kwa jinsia zote. Warwick alisema, "Kila mtoto Tanzania anastahili kupata elimu bora, lakini maelfu ya watoto wananyimwa fursa hiyo ya kubadilisha maisha kila mwaka.

"Mradi huu umetoa kipaumbele zaidi kwa watoto hawa kupata haki yao ya msingi ya elimu na kuweka mazingira mazuri kwa watoto wa kike." Warwick alisema ni hatua muhimu ya kukabiliana na changamoto ambazo watoto wa Tanzania wanakumbana nazo katika elimu."

Hata hivyo, alisema Benki ya Dunia itaendelea na mazungumzo na serikali kuhusu masuala mapana yanayohusu usawa kwa wanafunzi wote. "Mradi huu umetoa kipaumbele zaidi kwa watoto hawa katika kupata haki yao ya msingi ya elimu na kuweka mazingira mazuri kwa watoto wa kike," alisema Warwic.

Mkurugenzi wa Elimu wa WB, Jaime Saavedra, alisema "Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani, inakabiliwa na tatizo la kujifunza, kuna watoto ama hawapo shule au wapo shule lakini hawajifunzi. Kati ya watoto 100 wanaoanza shule Tanzania, zaidi ya nusu humaliza elimu ya msingi na ni watatu tu ambao humaliza elimu ya juu. Hili ni tatizo."

Alisema mradi huo utasaidia kupata elimu bora sekondari na kuzifanya shule kuwa sehemu salama za kuishi na wasichana bila kujali mazingira yaliyopo watapata njia kumaliza elimu zao. Taarifa hiyo ilieleza kuwa, zaidi ya miaka miwili iliyopita, karibu watoto 300,000, nusu yao ni wasichana, wameshindwa kuendelea na shule ya sekondari kwa sababu ya ufinyu wa nafasi katika shule za umma na inakadiriwa wasichana 5,500 ambao hupata ujawazito kuacha shule kila mwaka. Ilisema kuwa, SEQUIP imeundwa kuwezesha wasichana na wavulana wenye umri mdogo kumaliza elimu ya juu ya sekondari.



Wakuu wa mikoa (kutoka kushoto), Christopher Ole Sendeka (Njombe), Loata Sanare (Morogogo), Martine Shigela (Tanga) na Mrisho Gambo (Arusha), wakiweka shada la maua katika kaburi la Alazaro Sokoine ambaye ni mtoto mkubwa wa Waziri Mkuu wa zamani, Hayati Edward Moringe Sokoine, Monduli, mkoani Arusha juzi. **PICHA: OMR**

# Majaliwa asema atakayethibitika kuwa na corona lazima atangazwe

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI idadi ya walioambukizwa virusi vya corona nchini ikifikia 20 jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema yeyote anayebainika kuwa na virusi hivyo vinavyosababisha homa kali ya mapafu lazima atangazwe.

Vile vile, mtendaji mkuu huyo wa shughuli za serikali, amesema bila kujali cheo chake, yeyote anayethibitika kuwa na virusi hivyo atapelekwa mahali palipoandaliwa. Majaliwa alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini hapa alipowasilisha hotuba kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha.

"Mgonjwa akithibitika, kutangazwa ni lazima bila kujali cheo chake, awe waziri, katibu mkuu au mkurugenzi atalala palipoandaliwa," alisema na kuongeza:

"Watanzania wenzangu, tuendelee kupuuza taarifa za uzushi zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii. Niendelee kusisitiza kuwa sote tuzingatie maelekezo yaliyotolewa na serikali toka tulipoanza kampeni ya kupambana ugonjwa huu."

Hotuba ya kiongozi huyo safari hii imejikita katika kuzungumzia mafanikio ya serikali ya awamu ya tano katika kipindi cha miaka mitano, akibainisha kuwa yameonekana dhahiri kwenye kuimarisha miundombinu, kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi pamoja na kuhamasisha uwekezaji.

Alisema serikali imeanza utekelezaji wa miradi muhimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, ununuzi wa ndege kwa lengo la kufufua Shirika la Ndege Tanzania, kusambaza umeme vijiji, ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali, kuongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba na kutoa elimu bila malipo. Pia, alisema serikali imejidhatiti kuimarisha upatikanaji wa maji, huduma za kisheria na nidhamu serikalini imeongezeka kutokana na kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa watumishi wazembe, wadanganyifu na wasio waadilifu.


## TATHMINI YA AWALI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII

### TAARIFA KUHUSU MRADI TARAJIWA WA MCHANGA WENYE MADINI UNAOJULIKANA KAMA TAJIRI, ULIOPO WILAYA YA PANGANI, MKOA WA TANGA

Ili kutimiza matakwa ya sheria ya mazingira Sura ya 191 (Namba 20) ya 2004 pamoja na kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira za mwaka 2005 na mabadiliko yake ya mwaka 2018, taarifa hii inatolewa kuutaarifu umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited kwa kushirikiana na kampuni ya Environmental Resources Management (ERM), wamepewa kazi ya kufanya tathmini ya awali ya athari za kimazingira na kijamii kwa niaba ya kampuni ya Jacana Resources (Tanzania) Limited kwa ajili ya mradi wa mchanga wenye madini wa Tajiri.

Mradi huu tarajiwa upo wilaya ya Pangani mkoani Tanga takribani kilometa 40 kutoka jiji la Tanga. Eneo la mradi lipo ndani ya leseni mbili za utafiti (PL): PL 7321/2011 iliyopo wilaya ya Pangani. Leseni hii ya utafiti inamilikiwa na kampuni za Jacana Resources ambayo imesajiliwa Tanzania na ni kampuni tanzu ya kampuni ya Strandline Resources Limited, kampuni iliyosajiliwa katika soko la hisa la Australian (Australia Stock Exchange listed mining company (ASX: STA) ambayo imejikita katika utafiti na uendelezaji wa miradi ya madini Tanzania na Australia. Makadirio ya kiasi cha rasilimali za madini yaliyopo katika mradi wa Tajiri ni kiasi cha 239Mt kwa asilimia 3.3 ya jumla ya kiasi cha madini mazito (Total Heavy Minerals (THM) concentration).

Miradi ya uchimbaji wa madini ya aina hii huangukia katika kundi A la miradi kama ilivyoelezwa katika jedwali la kwanza la kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Taarifa hii imetolewa ili kutafuta maoni ya pande zote zinazohusika na zitakazoathirika na uwepo wa Mradi huu. Mtu yeyote mwenye nia, maoni ama dukuduku au ufahamu mahususi kuhusiana na athari za mazingira na kijamii zinazoweza kutokea kutokana na uwepo wa Mradi uliopendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anuani zifuatazo.

Jacana Resources (Tanzania) Limited
P.O Box 105009
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 222 600 430
Email: enquires@Strandline.com.au

The Director General, National Environmental Management Council (NEMC),
P.O. Box 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 22 2774889
Email: nemc@nemctz.org

MTL Consulting Company Limited
Masaki, Plot No. 689 Sandvick Street
P.O. Box 77894
Dar Es Salaam.
Tel: +255 22 2666879
Email: info@mtlconsulting-tz.com

115687502

# Magoti adai hofu mahabusi kusongamana

**Na Hellen Mwango**

HAKIMU Mkazi Mkuu, Janeth Mtega, amemtaka Ofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti na mwenzake wanaokabiliwa na tuhuma za Uhujumu Uchumi na wote walioko mahabusu kufuata mwongozo na kuchukua tahadhari ya kujikinga na virusi vya corona.

Mtega alitoa rai hiyo jana wakati akiahirisha kesi kwa njia ya mtandao kati ya ukumbi wa Mahakama ya Kisutu na Gereza la Segerea.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hata hivyo, Tito alinyoosha mkono na alipokubaliwa alidai kuwa zuio la msongamano ni mahakamani pekee, lakini watu wanapoishi gerezani halitumiki kwa sababu wanasongamana na wao wamesongamana.

Alidai kuwa jambo ambalo linawafanya wanaishi kwa hofu, watuhumiwa wanahisi wamesahaulika na kupuuzwa katika jitihada za kitaifa za kujikinga na ugonjwa wa corona.

"Siku 14 tangu kesi yetu iahirishwe hatujawasiliana na mawakili, familia, wazazi, watoto na wake zetu, tunajisikia kutengwa katika hatua hii muhimu, tunaiomba mahakama iangalie suala hili kisheria kuona uwezekano wa kutuondoa katika ya hofu na kusahaulika," alidai Tito mbele ya Hakimu Mtega.

Akijibu hoja za utetezi, Wankyo alidai mshtakiwa ametoa hoja, lakini kutokana na kujikinga na virusi vya corona serikali ilichukua hatua mbalimbali za tahadhari na Jamhuri inawatoa hofu kuwa washtakiwa wote hawajabaguliwa bali ni tahadhari ya kitaifa kudhibiti wageni kuingia gerezani.

Hakimu alisema upande wa Jamhuri uharakishe kukamilisha upelelezi, washtakiwa wote wafuate mwongozo wa serikali kuhusu kujikinga na virusi hivyo.

Alisema washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu na kesi hiyo itatajwa Aprili 14, mwaka huu.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni, Mtaalamu wa Tehama, Theodory Gyan (36), wote kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kumiliki programu ya kompyuta iliyotengezwa mahususi kufanya kosa la uhalifu na kutakatisha Sh. milioni 17.3.

Upande wa Jamhuri ulio wasomea mashtaka washtakiwa uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Joseph Pande na Wankyo Simon.

Katika kesi ya msingi, Wankyo alidai washtakiwa wote katika tarehe tofauti kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya Jiji la Dar es Salaam na mahali tofauti nchini kwa pamoja na watu ambao hawapo mahakamani, kwa makusudi walishiriki kutenda makosa ya kiuhalifu ya kumiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa kufanya kosa la jinai na kuwawezesha kujipatia Sh. 17,354,535.

Nchimbi alidai katika tarehe tofauti kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya jiji na Mkoa wa Dar es Salaam kwa pamoja washtakiwa hao na wengine ambao hawapo mahakamani walimiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kutenda makosa.

Mkude alidai katika shtaka la tatu, Inadaiwa kuwa kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019, jijini Dar es Salaam washtakiwa hao kwa pamoja walitakatisha na kujipatia Sh. 17,353,535 wakati wakijua mapato hayo yametokana na zao la kosa la kushiriki genge la uhalifu.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi mpaka ipate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mshataka nchini (DPP) au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kulia), akiteta jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dk. Anold Kihaule, wakati wa mkutano na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, ambapo ameahidi kuwashughulikia watendaji wasiotoa huduma stahiki kwa wananchi wanaofika kuomba vitambulisho. **PICHA: WMNN**

## Shule kuhifadhi washukiwa corona

**Na Happy Severine,** BUSEGA

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, amesema Mkoa huo hautatumia hoteli kwa ajili ya kuhifadhi watu watakaohisiwa kuwa naa maambukizi ya virusi vya corona.

Mtaka amesema kwamba badala yake watatumia shule za sekondari za bweni.

Alisema wameamua kuchukua uamuzi huo ili kuwapunguzia gharama za kuishi katika hoteli siku zote ambazo watakuwa karantini.

Hata hivyo, Mtaka alisema kwamba utaratibu huo hautawafunga watu wenye uwezo ambao watapenda kwenda hotelini.

Mtaka alisema hayo jana alipokuwa akipokea msaada wa vifaa vya ujenzi wa Shule ya Sekondari Mtaka wilayani Busega kutoka kwa viongozi wa Umoja wa Makanisa 21 ya Kikristo Tanzania Kata ya Lamadi.

Alisema kila wilaya imetenga shule yenye vitanda vya kutosha na mazingira mazuri kwa ajili ya kuwahifadhi washukiwa hao, huku akiwataka wananchi wa Mkoa huo kuendelea kuchukua tahadhari.

"Tumeamua kuwa hatutatumia hoteli kuhifadhi mtu yeyote ambaye atabainika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona, tumeamua kutumia shule za sekondari za bweni ...labda mtu mwenyewe aamue kupelekwa katika hoteli zilizoainishwa," alisema Mtaka.

Katika hatua nyingine, aliwataka wazazi wa wanafunzi wa madarasa ya mitihani mkoani humo kuwafuatilia na kuwasimamia watoto wao kuhakikisha wanajisomea katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa kutokana na tishio la ugonjwa huo.

# Mtambo wa kisasa kumaliza tatizo la vitambulisho taifa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema imepatia ufumbuzi wa malalamiko ya wananchi juu ya kuchelewa kwa vitambulisho vya taifa kwa kununua mashine mpya za kisasa zenye uwezo wa kufyatua vitambulisho 9,000 kwa saa.

Wakati suala la vitambulisho likipatiwa ufumbuzi, serikali imesema inakusudia kufanya mabadiliko makubwa ndani ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) kutokana na utendaji usioridhisha. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema jana kuwa hatua hiyo imetokana na kubaini kuwa uchakavu wa mashine ndicho chanzo cha ucheleweshaji wa utoaji vitambulisho hivyo kwa wananchi.

Akizungunza na waandishi wa habari jijini hapa, Simbachawene alisema mashine hizo zilizonunuliwa kwa Sh. bilioni 8.5 zitakuwa mwarobaini kwa tatizo hilo ambalo limekuwa likilalamikiwa na wananchi kwa muda sasa.

Pamoja na changamoto hiyo, alisema mpaka sasa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), imeshatoa vitambulisho milioni sita na kutambua wananchi milioni 21. 8 kati ya watu 27. 7 waliotarajiwa kusajiliwa.

Alisema namba za kipekee za utambulisho ni milioni 17. 8 zilikiwa zimezalishwa na zinaweza kutumika katika utambuzi wa watu.

Kwa mujibu wa Waziri, mashine hizo mpya zitakamilika kufungwa mwezi huu na kuanza kufanya kazi na kwamba baada ya hapo hakutakuwa na tatizo la kucheleweshwa kwa vitambulisho vya taifa.

Alisema mitambo mipya kwa kushirikiana na ile ya zamani, anaamini itatoa vitambulisho vingi na kwamba wanatarajia kukamikisha utoaji wa zana hizo ndani ya miaka miwili.

"Safarii hii vitambulisho vitakuwa bora. Awali vilivyotolewa havikuwa na ubora kutokana na mashine kuwa chakavu, " alisema Simbachawene huku akibainisha kuwa mtambo wa awali ulikuwa ukizalisha vitambulisho 500 kwa siku lakini kwa sasa vitaboreshwa na kuzalishwa vingi kwa siku.

Simbachawene aliwaomba radhi wananchi kutokana na kupata shida katika kupata vitambulisho na kuahidi kuwa kuanzia sasa watavipata kwa haraka bila usumbufu. Katika hatua nyingine, Waziri Simbachawene alisema kutokana na utendaji usioridhisha, serikali inatarajia kufanya mabadiliko ndani ya Nida ili kuboresha.

Alisema pia watakuwa makini katika ugawaji wa vitambulisho kwa wageni wakaazi na wakimbizi.

HABARI KITAIFA

## Uamuzi kesi ya Mdee Aprili 28

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeshindwa kutoa uamuzi wa kama Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, ana kesi ya kujibu dhidi ya tuhuma za uchochezi au la baada ya mshtakiwa kushindwa kufika mahakamani kwa madai kuwa anasumbuliwa na maumivu ya mkono.

Mdee kupitia mdhamini wake, Farisi Upono, amewasilisha barua akieleza kwamba anasumbuliwa na maumivu ya mkono na kushindwa kufika kwenye kesi yake.

Madai hayo yalitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Awali Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto, alidai kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kusikiliza uamuzi wa mahakama kama mshtakiwa ana kesi ya kujibu au la.

Hata hivyo, Upono alidai kuwa mshtakiwa ameshindwa kufika mahakamani kwa sababu anasumbuliwa na maumivu ya mkono.

Hakimu Simba alisema mahakama yake itatoa uamuzi Aprili 28, mwaka huu, kama kigogo huyo wa kitaifa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mdee ana kesi ya kujibu au la.

Mapema mahakamani hapo, mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri walitoa ushahidi akiwamo Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Urafiki, Mrakibu wa Polisi (SP) Batseba Kasanga.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Julai 3, 2017 katika Makao Makuu ya Ofisi ya Chadema iliyopo Mtaa wa Ufipa, Wilaya ya Kinondoni, Mdee anadaiwa kutamka maneno dhidi ya Rais John Magufuli kuwa "anaongea ovyo ovyo , anatakiwa afungwe breki" kitendo ambacho kingeweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Mdee alifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza na kusomewa mashtaka yake Julai 10, 2017 na yupo nje kwa dhamana.



Baadhi ya wabeba mizigo katika soko la Mabibo maarufu kama Mahakama ya Ndizi, jijini Dar es Salaam, wakiwa wamejipumzisha huku soko hilo, likiwa limezingirwa na matope kutokana na mvua ndogo iliyonyesha jana na kusababisha usumbufu kwa wateja. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbaroni tuhuma kukutwa na vifaa tiba bila ya vibali

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kupatikana na dawa za binadamu na vifaa tiba bila kibali huku wakidaiwa kutoa huduma za kitabibu kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Wilbroad Mutafungwa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika maeneo tofauti ya mkoa wa Morogoro wakati wa doria za askari baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wasamaria wema. Tukio la kwanza, alisema lilitokea katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro ambako Barnabas Mayunga (32), mkazi wa Kihonda kwa Mkomola, Manispaa ya Morogoro alikamatwa na dawa mbalimbali za binadamu pamoja na vifaa tiba vingine vikiwa na nembo ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Alisema mtuhumiwa huyo alikutwa na vifaa hivyo vikiwa katika gari lake lenye namba za usajili T 394 DKP aina ya Toyota Harrier na vingine akiwa navyo nyumbani kwake bila kibali.

Mutafungwa alivitaja vifaa vilivyokamatwa kuwa ni 'cotton wool', fomu ya bima ya afya moja isiyojazwa, dripu sita za MSD, Ketavit 50, lignocain injection moja, sare moja ya rangi ya kijani, kitambulisho cha mpigakura, glovu mbili, folic Acid dozi moja, Chromit Catgut 15, Eocost Plastnne na Calvista mbili.

Vifaa vingine alivyokamatwa navyo ni vitabu vitano vya matibabu ya wagonjwa, fomu nne za matibabu, mkasi.

Vingine amevitaja kwa majina ya heine moja, Feiya moja, Kiboksi cha huduma ya kwanza, Gentremycine 10, Epirucks maboksi mawili, mpira mmoja wa kupitishia mkojo, Acne free mbili, Oracure moja, Irefone Gery 01, Amoxyline saba, Lamopazzle boksi moja, Nirixone Aoana Phamaecetical maboksi mtano, Pantacid moja, Lignocare moja pamoja na Ketajet.

Vingine, kwa mujibu wa Mutafungwa, ni mabomba 22 ya sindano, mashine ya kupima shinikizo la damu, nailoni moja ya 60 MG, Artesun moja, boksi moja la Panadol, Aroxicam moja, D-Artep moja, Safeteram moja na Haema cap moja.

Kamanda Mutafungwa akabainisha kuwa, Polisi wanaendelea kuchunguza kwa kina taaluma ya mtuhumiwa huyo kwa madai kuwa bado ameendelea kujitambulisha kama daktari katika maeneo mbalimbali.

"Awali alikuwa akifanya kazi hospitali ya mkoa na akaondolewa, kwa hiyo bado haieleweki aliingiaje hapo hospitalini na amesomea wapi taaluma hiyo ya udaktari. Kikikubwa zaidi ni kuwa na hivi vifaa tiba na dawa ambazo zingine zina nembo ya MSD bila kuwa na kibali," alisema. Mutafungwa alisema tukio lingine linamhusisha Daniel Nelson (28) mkazi wa Kitongoji cha Minjenja, Wilaya ya Gairo, aliyekamatwa akiwa na vifaa vya matibabu ya binadamu anavyomiliki nyumbani kwake bila kibali.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na Canula, MVA-Set and Tube, Stetoscope, mashine ya kupimia shinikizo la damu, koti la kitabibu, Metal Tray, Mayo scissor, speculam, penguinsucker, toothed, artery force na sponge holding force.

SACP Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa baada ya awali kukamatwa kwa tuhuma za kumtorosha binti kutoka kwenye himaya ya wazazi wake na alipokwenda kufanyiwa upekuzi nyumbani kwake, alikamatwa akiwa na vifaa hivyo.

Inadaiwa mtuhumiwa awali alikuwa akifanya kazi kwenye hospitali moja ya misheni katika idara ya maabara na baada ya kuacha kazi, ikadaiwa akawa anaendelea kutoa huduma za matibabu ya binadamu kienyeji na kwa uficho nyumbani kwake.

Kamanda huyo wa Polisi alisema watuhumiwa hao wote wawili bado tuhuma zao zinachunguzwa na baadaye watafikishwa mahakamani.

# DC aagiza kigogo wa ununuzi kusimamishwa, kuchunguzwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameagiza kusimamishwa kazi na kuchunguzwa kwa Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Sabiano Wambura.

Ofisa huyo anatuhumiwa kununua kwa bei ya ulanguzi matofali ya ujenzi wa zahanati ya kwa Tito. Zahanati hiyo iliyoanza kujengwa mwaka 2009 katika Kijiji cha Kwa Tito, Kata ya Weruweru, inatarajiwa kuhudumia zaidi ya kaya 250 na wananchi wa vijiji jirani zaidi ya 1,000.

Ole Sabaya jana alitoa amri ya kukamatwa na kushikiliwa kwa mkuu wa kitengo hicho na kisha polisi kumkabidhi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru). Aliagiza Takukuru kuanza kumhoji ofisa huyo kutokana na tuhuma za kuchelewesha ujenzi wa kituo hicho licha ya serikali kutoa Sh. milioni 30 za ujenzi Agosti, mwaka jana.

"Mkurugenzi Mtendaji (Elia Machange) tafuta watu na nataka majibu ndani ya siku 14 kazi imefikia wapi. Mna pesa kwenye akaunti zimeletwa tangu mwezi wa nane mwaka jana na wananchi wanateseka, wanatembea umbali mrefu, ninyi mnafanya nini?

"Mwezi wa nane mwaka jana mliletewa fedha za umma hamkutumia na leo ni mwezi wa nne mwaka 2020. Mheshimiwa Rais John Magufuli ameleta fedha hapa ziwasaidie watu wa kawaida hawa. Hamjali halafu ninyi mnaenda kutibiwa na familia zenu hospitali ya Wilaya au Moshi Mjini," alisema.

"DED (Mkurugenzi Mtendaji) nataka ndani ya siku 14 hili jengo liwe limekwisha, fanyeni namna mnavyoweza liishe. Tujitahidi watu waanze kutibiwa hapa tuache blaablaa niwe nawaambia jambo hilo hilo hakuna anayesikia," alisisitiza.

Akijitetea kuhusu kusuasua kwa ujenzi huo, Wambura alimweleza Ole Sabaya kuwa alichelewa kutangaza zabuni hiyo kwa sababu ilikuwa lazima mchakato wa utoaji wa fedha hizo upitie katika vikao vya Kamati ya Fedha ya Baraza la Madiwani wa Wilaya hiyo.

Akizungumzia mkwamo huo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kwa Tito, Olivia Mwasamba. alisema kusuasua kwa ujenzi wa zahanati hiyo, kumetokana na kitengo cha ununuzi kuchelewesha utoaji wa vifaa vya ujenzi yakiwamo matofali, saruji na mchanga.

Diwani wa Weruweru, ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Ujenzi ya Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, Swalehe Juma, aliunga mkono uamuzi uliochukuliwa na mkuu wa wilaya akieleza kuwa hata madiwani wameshalalamika na kushangaa fedha za serikali zipo kwa ajili ya ujenzi lakini vifaa hakuna.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tume isimamie ahadi ya uchaguzi huru, haki

**KAMATI** ya Uangalizi wa Chaguzi Tanzania (Temco), imeibua madai mbalimbali kuhusu kasoro zilizojiri wakati wa kuliboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura, ikielezea namna ambavyo watu wengi huenda wasipate nafasi ya kupiga kura kutokana na kuzuiliwa, kwa kutumia sababu ambazo pengine hazina mashiko.

Temco inataja moja ya yaliyobainika kuwa ni pamoja na hatua ya kushangaza ya kuwarudisha nyumbani waliovaa fulana yenye ukosi au kola ya duara. Tunajiuliza hii ni sababu ya mwananchi anayetafuta haki yake ya kuwa mpigakura kuikosa?

Si hivyo tu, yapo zaidi , kuna masuala mengine mengi kama kukosekana wawakilishi wa vyama katika mchakato wa kuwasajili wapigakura wapya. Kuharibika mashine za kusajili kwa teknoloji ya bayometria au mashine za BVR na ukosefu wa elimu ya wapiga kura. Tunapozichunguza kasoro hizi tunaona kama hazina mashiko kwa vile ni kama kuwakwamisha wapiga kura waliotakiwa kuhimizwa kujisajili badala ya kuwaridisha majumbani.

NI imani yetu pengine na ya Temco kuwa kuhakiki daftari hili kusingetegemewa kuwa na kasoro nyingi kama hizo kwani kuwapo na visingizio na vikwazo kunawafanya watu kutojitokeza na hivyo kuwa na idadi ndogo ya watu wanaofika kujihakiki ambao wangepiga kura Oktoba.

Tunaona kama kuwapo kwa kasoro kunaufanya utaratibu na mchakato huu kuwa jukumu lenye changamoto kidemokrasia au lawama badala ya tija licha ya gharama kubwa inayotumika ili kutekeleza azma hiyo na kufanikisha uchaguzi.

Kimsingi kuhakiki daftari kulitakiwa kuwe jambo linalowahamasisha wananchi wengi kujitokeza kujisajili hata wale ambao wanaona wanabanwa na kazi au wanaohisi wana majukumu makubwa kifamilia.

Lakini, iwapo watu watatimuliwa kisa mavazi , inashangaza ingefaa wapewe nguo stahiki ambazo walitakiwa kuzivaa ili kupigwa picha badala ya kufukuzwa, hivyo maofia wa tume inayosimamia uchaguzi ilifikiria nini kuhusu kuwafukuza waliokuwa na mavazi kama hayo?

Hali hiyo, inachangia kujenga mazingira ambayo husababisha visingizio na wengi kupuuza uhakiki na hivyo kuwa na idadi ya watu wachache wanaojitokeza kupiga kura.

Tunaona kuwa iwapo wengi watakosa haki yao ya kupiga kura inaweza kuonekana kuwa ni kasoro na kama inawezekana ni vyema ili kuondoa kosa hilo kwa zoezi kufanyika tena ili kuwapa nafasi wale ambao hawakushirikishwa kikamilifu .


Ikumbukwe kuwa wakati mwingine wananchi wanakuwa na mawazo kuwa mambo haya hufanywa kwa lengo au nia ya kufanikisha malengo fulani.

Wakati mwingine tunajiuliza kwanini kusiwekwe orodha ya mambo ya kufanya na ya kuacha wakati wa kuhakiki daftari hilo au hata kwenye kupiga kura kuliko kuwafukuza watu wanaojitokeza? Temco inazungumzia ushiriki wa vyama vya siasa kuwa ni wa muhimu kwa mafanikio na kuaminika kwa mchakato wowote wa uchaguzi. Tungependa kushauri kuwa uchaguzi ni mchakato unaohusisha wadau wengi kuanzia wapiga kura, wagombea, vyama vya siasa, waangalizi wa ndani na wa nje, hivyo ni muhimu kuzingatia demokrasia na ushirikishwaji ili kuondoa lawama na malalamiko miongoni mwa wadau hao.

Linazungumzwa pia suala la ucheleweshaji wa vifaa vya kuandikisha wapigakura Zanzibar na mikoa ya Njombe na Ruvuma, hali hii ilisababisha zoezi liahirishwe kwa siku kadhaa na sehemu nyingine kutofikiwa.

Yote haya yanaongeza hisia za kulalamika na kutoridhika , kama tulivyosema uchaguzi ni mchakato ni vyema wadau wote wakaridhika na kuwa na imani na mchakato unaofanyika ili kufanikisha azma ya kufikia demokrasia ambayo wengi wanaitamani na kushuhudia uchaguzi ukiwa wa haki na huru kama Rais John Magufuli alivyoahidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Unashiriki vipi kuikabili Corona?

Na Beatrice Moses

**KUENEA** virusi vinavyosababisha Corona, (COVID-19), kumetikisa dunia katika nyanja mbalimbali, ikiwamo, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk Tedros Ghebreyesus, alikaririwa hivi karibuni akizungumza mjini Geneva, Uswisi kuhusu dalili ya kuenea duniani kote kwa covid-19.

Dk Tedros alibainisha kuwa, hatua ya kutangaza kuwa virusi vya corona vimeenea duniani na tayari kuna vifo vya ugonjwa huo, unaoaminika ni hatari na unaua haraka.

Alisema WHO wamejiwekea utaratibu wa kutathmini mlipuko, kutokana na kuzuka kwa hofu kubwa ya kuenea kwa ugonjwa huu katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea.

Kwa mujibu wa Dk Tedros, ni mara ya kwanza kwa virusi hivi vya corona kusambaa dunia nzima akitamka: "Hili ni janga la kwanza la kusababishwa na virusi vya corona..."

WHO kupitia vyombo vya habari, imekuwa ikichukua hatua tangu ilipoarifiwa kuzuka ugonjwa huo, ikizitaka nchi kuchukua hatua za kudhibiti kuenea maadhi hayo.

Ni ugonjwa unaoathiri shughuli za kijamii na kubadilisha mfumo mzima wa maisha, ikiwamo kuzuia utamaduni wa kusalimiana kwa kupeana mikono.

Tayari nchi kadhaa ikiwamo Tanzania zimezuia shughuli za mikusanyiko, hivyo inalazimu shule na vyuo kufungwa kwa muda. Hatua zaidi hata vyombo vya usafiri havitakiwi kujaza abiria zaidi ya waliokaa.

Ni hatua ya kusababisha usumbufu mkubwa na gharama kwa wazazi, walezi na shule, pia ni wazi imesababisha usumbufu kwa baadhi ya wanafunzi na shule, hasa waliopo kwenye maandalizi ya Mtihani wa Taifa wa kidato cha Sita.

Taasisi za dini kwa nyakati tofauti, nazo zimelazimika kuchukua hatua ya kutoa tahadhari kwa waumini wake kupitia vyombo vya habari na zipo zilizotangaza kubadili utaratibu wa baadhi ya vitendo ambavyo vinafanywa katika ibada, kama ishara ya amani ya kupeana mikono.

Kisiasa, baadhi ya watu wamechukua suala hili kisiasa kujaribu kueneza uzushi kwa nia ya kujijenga ndani ya jamii wakikusudia kubomoa chama tawala.

WHO kwa kutambua umuhimu wa kupambana na hilo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu (IFRC), walitangaza mwongozo kusaidia kulinda watoto dhidi ya maambukizi ya virusi hivyo.

Katika mwongozo huo, inapendekezwa hatua za kuchukua kupunguza madhara kwa uwezo wa mtoto kujifunza na ustawi wake, kwa ujumla hasa wakati huu shule nyingi zimefungwa.

Hatua hiyo inatajwa kulenga kuweka mipango thabiti ya mtoto kuweza kuendelea kusoma hawapo nyumbani, kama vile elimu mtandao na elimu kupitia matangazo ya redio na wakati huohuo mtoto apate huduma muhimu.

Katika mwongozo huo, imebainishwa mipango hiyo ijumuishe hatua salama za kuhakikisha pindi shule zifunguliwapo, zinaendelea kuwa salama kwa mtoto.

Iwapo shule bado zimefungwa, mashirika hayo yanapendekeza ni lazima kuhakikisha watoto na familia zao wanaendelea kulindwa na kupata taarifa sahihi kuhusu ugonjwa huo.

Katika mwongozo huo, inabainishwa kuwa inapaswa watoto wapatiwe taarifa ya jinsi wanavyoweza kujilinda, ikiwa ni pamoja na kutambua umuhimu wa kuwa kwenye eneo lenye mfumo mzuri wa hewa.

Mapendekezo ni watoto wafundishwe namna ya kunawa mikono na vifaa vya kutumia wakati wa kujisafisha, kwenye eneo linalopitisha hewa na yanataka mtoto afuatiliwe, hata pindi anaugua abakie nyumbani, huku wakati wote wahamasishwe kuuliza maswali na kuelezea mambo yanayowatatiza.

Wametakiwa kuelekeza kuwa, kukohoa na kupiga chafya kufanyikie kwenye kitambaa au kwenye kona ya kiwiko, wakikwepa kugusa uso, macho, mdomo na pua.

Rais Dk. John Magufuli, alishaagiza wasafiri wote watakaoingia nchini, kutoka nchi zilizoathirika zaidi na ugonjwa huo, watalazimika kufikia sehemu zilizotengwa, na kukaa huko kwa siku 14 kwa gharama zao wenyewe.

Hizo ni baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika ngazi ya kimataifa, kitaifa na kijamii. Sasa ni wajibu kila mmoja wetu kujiuliza je, amechukua hatua gani katika kushiriki kuepusha kuenea kwa virusi vya ugonjwa huu tishio. Bottom of Form

# BARUA & MJADALA

## Tujipange kwa usafiri huu

**Mhariri,**

*SASA wakazi hasa wa mijini, tumepatikana kutokana na hatia nzito zinazoenadana na maradhi ya Corona. Magari yote sasa ni 'level seat' ikiwa lugha ya usafiri kwa maana ya hakuna abiria wa kusimama.*

*Kweli uamuzi huo ambao unahesbabu siku 'mbili tatu' umekuwa shubiri kwani kwetu wakazi wa mjini tunatawaliwa na mfumo wa maisha wa safari ya kwenda na kurudi, nyenzo kuu ya usafiri ni daladala.*

*Pia, kutokana na uhalisia uliopo kwamba idadi ya maambukizi hatuna jinsi, uhalisia wa mapambano ni lazima tuingie katika mfumo mpya wa maisha.*


*Mfano, huko nyuma tulizoea kuona linakuja daladala linatuzoa wote katika kurupushani kituoni tunawahi katika shughuli zetu. Hiyo sasa ni simulizi, tunaingia katika maisha mapya.*

*Nimesema hivyo baada ya kuona baadhi ya wenzetu wako katika mjadala wa vipi hilo na lile, ingawa majibu yake ni kutakiana mema kimaisha.*

*Kimsingi, najua imekuwa shida, wapo waliotembea umbali mrefu na wapo walionyanyasika kwa namna hii na ile, kuanzia mabasi hadi huduma za treni jijini.*

*Ushauri wangu wa mwisho, ni kwamba sote tunapaswa kujiunga na mabadiliko haya kuangalia tunasonga kwa namna gani sasa.*

**Hamudi Juma,**
**Kongowe, Dar es Salaam.**




## Madereva daladala zingatieni kinga corona, kuliko kipato

**Na Sabato Kasika**

MAKALI ya maagizo ya Mamlaka ya Udhibiti Usafi wa Ardhini (Latra) ya kuwataka wasafirishaji wote kuchukua tahadhari ya kuhakikisha hakuna abiria wanaosimama katika daladala, yameanza kuuma.

Hali hiyo imeanza kujitokeza jijini Dar es Salaam, pale daladala zinazokiuka maagizo kukamatwa na kushushwa abiria wanaokutwa wanasafiri wamesimama.

Kwa mujibu wa Latra, abiria wote wanatakiwa kuwa wamekaa katika viti, pia wananawa mikono kabla ya kupanda daladala. Utekeklezaji wa hayo bado ni kitendawili kwamba kuna abiria wengi hawatekelezewi na wasafirishaji wao.

Badala yake, wamebuni mbinu nyingine ya kujaza abiria kama kawaida, wakiamini kwamba hawawezi kukamatwa na vyombo vya dola, kumbe tayari mchezo huo umeshagundulika.

Kuna makondakta na madereva wa daladala wanaojaza abiria kama kawaida, lakini wanapofika maeneo ambayo wanajua kuna askari, wanawaambia abiria waliosimama wachuchumae kwenye korido za gari.

Wanafanya hivyo, ili daladala ionekane ina 'level seat' na wakishavuka eneo lenye askari, wanawaruhusu abiria kusimama tena na kila wanapohisi kuna askari mbele wanawaambia wachuchumae.

Mtindo huo umekuwa ikitumiwa pia na baadhi ya mabasi yanayokwenda mikoani, ambayo yalikuwa yanajaza abiria kupita kiasi na yanapofika maeneo yenye askari, abiria waliosimama huchuchumaa.

Baada ya kuvuka kikwazo hicho, husimama na kuendelea kujaza wengine kama kawaida, hata kwenye mzani, abiria wasio na viti huambiwa warudi nyuma ya gari na kuchuchumaa.

Lengo ni kukwepa kujulikana kama yamejaza abiria kupita kiasi, ili wasafirishaji wasitozwe faini, Niseme, sasa umefika wakati wa kuachana na tabia hiyo ya kutaka fedha hata kwenye mazingira ambayo ni hatarishi.

Baadhi ya madereva na makondakta wa daladala jijini Dar es Salaam, wanaiga mtindo huo bila ya kujali kwamba serikali imezuia, kutokana na tishio la virusi vya corona.

Kwa bahati nzuri wanaofanya mchezo huo, wameanza kugundulika na kunaswa, Askari nao wanajibu mapigo kwa kuzisimamisha daladala, wanaingia ndani kukagua ili kuhakikisha kama maagizo ya kiserikali yamezingatiwa.

Juzi waliingia katika daladala moja inayofanya ruti kati ya Mbezi Mwisho na Makumbusho na kushuhudia baadhi ya abiria wasio na viti, wakiwa wamechuchumaa kwenye korido ya gari.

Ni tukio lililotokea eneo la Kimara Mwisho, jijini Dar es Salaam, majira ya saa 11 alfajiri. Polisi waliamrisha abiria wote washuke ili kupanda daladala nyingine, huku dereva na kondakta wakishikiliwa kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Ingawa kilichofanywa na askari kilikuwa ni usumbufu kwa waliokuwa wamekaa kwenye viti, lakini inanifurahisha kuonyesha ni jinsi gani serikali imedhamiria kupambana na tishio la maambukizi ya virusi vya corona katika usafiri wa umma.

Ni hatua inayowakumbusha wasafirishaji na abiria kuzingatia maelekezo ya kutojazana katika daladala, bali watambue serikali imedhamiria kupambana na maambukizi ya virusi vya corona, ambavyo madhara yake ndani ya nchi yetu na nje ua mipaka, tunayasikia.

Kutojaza abiria katika gari kuna changamoto zake, ila jambo la msingi ni kutambua kwamba, serikali imeamua kuchukua hatua hizo kwa ajili ya usalama wa Watanzania wote.

Ni kweli kila mtu anataka kuwahi kwenye shughuli zake na wenye daladala wanataka kufanya biashara. Lakini, ni vyema kuangalia mazingira yenyewe ya biashara, kuliko kulazimisha kujaza abiria wakati hairuhusiwi.

Biashara ya usafirishaji inaweza kuwa mbaya kimapato, kutokana na kubeba abiria waliokaa kwenye viti tu. Lakini, ni muhimu kuzingatia afya kwanza, kuliko fedha zinazogombewa na baadhi ya makondakta na madereva hao.

Kubeba abiria waliokaa tu, kunasababisha wengi kubaki vituoni wakisubiri usafiri. Bado, ni bora ibaki hivyo, kuliko kujazana katika daladala moja na kujiweka katika hatari kubwa ya kuambukizana maradhi.

Ndugu kondakta anapoelekeza abiria wachuchumae pale daladala inapopita eneo ambalo kuna askari, ni mbinu za kutaka kujiongezea kipato cha nauli, lakini hatari yake ni kusambaza maambukizi ya virusi vya corona kwa kasi.

Hivyo, ni vyema tishio la virusi hivyo likawa fundisho kwa jamii kuzingatia afya kwanza, kuliko kulazimisha kusafiri katika mazingira yasiyo salama, katika jitihada za kutaka kuwahi sehemu ya kazi au nyumbani.

### WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

### KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Marin Hassan afariki dunia

**Na Maulid Mmbaga**

MTANGAZAJI nguli wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Marin Hassan Marin (48), amefariki dunia katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Dar es Salaam, alikopelekwa kwa ajili ya matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurungenzi Mkuu wa TBC, Ayub Rioba, mtangazaji huyo aliyekuwa ofisini hadi juzi usiku kwa ajili ya maandalizi ya kipindi cha Azidhio kilichoanza kurushwa hewani juzi, alifariki dunia jana asubuhi.

Kutokana na kifo hicho, Rais John Magufuli alituma salamu za pole huku akimwelezea Marin kama mwandishi mahiri aliyelitumikia taifa lake kupitia kazi ya utangazaji. Alisema alimfahamu Marin kama mtu aliyetoa mchango mkubwa katika ustawi wa uandishi wa habari Tanzania na kwa juhudi zake kubwa TBC ambako aliripoti habari kwa ubunifu wa hali ya juu.

"Marin ameondoka wakati ambao tunamhitaji zaidi. Ni shujaa wa habari Tanzania, aliipenda sana TBC na nchi yake kwa ujumla. Naungana na familia ya TBC na waandishi wote kumwombea apumzike mahali pema peponi," alisema Rais Magufuli.

Mmoja wa wafanyakazi wenzake, Elisha Elia, alisema Marine alikuwa mchapakazi na ni mtu mwenye shauku ya kuinua vipaji vya vijana hususani katika tasnia ya habari.

Alisema Marin alipata mafunzo yake ya utangazaji nchini Kenya na alitangaza katika kituo cha televisheni cha KTN nchini humo na baadae alihamia Zanzibar na kujiunga na Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC).

Baada ya kuachana na ZBC, alihamia TBC ambako alikuwa mmoja wa waasisi wa kipindi cha Jambo Tanzania na mshiriki wa Kapu la Wiki na kushiriki kutangaza vipindi vingine vingi ambavyo vinarushwa kupitia shirika hilo. Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Matukio wa TBC, Frank Bahati, alisema Marin alianza kujisikia vibaya majira ya saa 12 asubuhi na akapelekwa Lugalo na ilipofika saa 3 kasoro alifariki dunia.

"Hakuna asiyemfahamu Marin katika tasnia ya habari. Kwetu wana TBC ni pigo na taifa kwa ujumla ma taarifa hizi zimetushtua sote lakini tunamwomba Mwenyezi Mungu atupe subira," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi wa Televisheni, Martha Swai, alisema Marin alikuwa mwandishi mahiri na kwamba pengo lake ni kubwa katika tasnia.

Pia alimshukuru Rais magufuli kwa kutoa ndege binafsi ambayo ilibeba familia ya Marin kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam na baadaye kusafirisha mwili na familia kwenda Zanzibar kwa ajili ya mazishi.

Marin alizikwa visiwani humo jana. Mungu amlaze mahala pema peponi, Amen.



Wasamaria wema wakisaidia kuisukuma pikipiki ya matairi matatu, baada ya kushindwa kupanda mlima katika njia ya kuelekea Msewe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Takukuru yaanza kusaka bil. 4.5/- kwenye Saccos

**NaA Francis Godwin,** IRINGA

KIASI cha Sh. 683,408.00 walizokuwa wamekopeshana kiholela baadhi ya viongozi na wanachama wa vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa (SACCOS) katika wilaya tatu za Mkoa wa iringa, zimeokolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Wilaya hizo ni Kilolo , Mufindi na Iringa, kwa mujibu wa Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Iringa, Mweli Kilimali.

Alieleza kuwa taasisi hiyo imedhibiti kiasi hicho kutokana na uchunguzi wa ubadhirifu wa fedha baada ya kuzifanyia uchunguzi wa kina Saccos zilizopo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Iringa .

Alisema kwenye uchunguzi huo zaidi ya Sh. bilioni 4.5 zilizofanyiwa ubadhirifu na viongozi katika vyama 58 vilivyopo katika Wilaya za Mufindi , Kilolo na Iringa, fedha hizo ni madeni ya wanachama ambayo hayajareshwa kwa kipindi kirefu kwenye vyama hivyo. "Kutokana na na ukiukwaji wa urejeshaji wa madeni ambao ni kinyume cha sheria na taratibu za uendeshaji wa vyama hivyo, taasisi hiyo ilifanya uchunguzi kwa vyama hivyo na kuwabana wahusika, hivyo kufanikiwa kuokoa fedha hizo, " alisema. Kilimali alisema kutokana na wanachama na baadhi ya viongozi kushindwa kurejesha mikopo yao, Takukuru ilifanya uchunguzi wa kina katika vyama hivyo na kubaini ubadhirifu huo ulioshirikisha baadhi ya madalali waliopewa kazi ya kukusanya fedha hizo, madalali hao badala ya fedha hizo kuzifikisha kwenye vyama husika, waliishia kuzitafuna wenyewe.

"Takukuru Mkoa wa Iringa inawataka madalali wote waliotafuna fedha za vyama vya ushirika kurejesha fedha hizo na tutafanya msako mkali kuwanasa endapo watakaidi maelekezo haya," alisema na kuongeza: "Madalali hawa wamekuwa wakikusanya fedha za wadaiwa sugu na badala ya kufanya minada ya mali zao walizokamata fedha wanazopata wamekuwa wakizitafuna wao, tutawasaka wote na kuwachukulia hatua kali.".

## Auawa na simba akiwa na mumewe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA wa Kijiji cha Kimbemba, Kata ya Mangirikiti, Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Darie Chisangwe (58), amekufa kwa kushambuliwa na simba majira ya usiku akiwa na mumewe.

Chisangwe alikutwa na mauti alipotoka nje ya nyumba yake kwenda kujisaidia haja ndogo akiwa na mumewe.

Habari kutoka kijijini hapo na kuthibishwa na majirani na viongozi wa Serikali, zinaeleza kuwa Chisangwe alishambuliwa na simba huyo usiku wa Machi 30, mwaka huu.

Baadhi ya majirani waliojitambulisha kwa majina ya Kindamba Hemedi, Juma Yusufu na Vivian Joseph, walisema siku hiyo Chisangwe akiwa na mumewe (bila kumtaja jina), walitoka nje kwa lengo la kujisaidia.

Walisema wakati mume akiwa amesimama katika uwanja wa nyumba yao akimsubiria mkewe amalize haja zake, ghafla simba aliyekuwa katika mawindo yake alimvamia mwanamke huyo kichwani na kumjeruhi vibaya eneo la usoni.

Pia, walisema wakati mnyama huyo akijaribu kumvutia kichakani mwanamke huyo, mumewe ambaye alikuwa akiomba msaada wa majirani zake, alijitosa kumuokoa mkewe, alishajeruhiwa vibaya ikiwamo kutokwa damu nyingi.

Walisema majirani walipojitokeza kutoa msaada walikuta mume amefanikiwa kumuokoa kisha kumpeleka Hospitali ya Wilaya iliyoko Mjini Liwale kwa matibabu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Evarist Sanga, alithibitisha kupokelewa kwa majeruhi huyo na kueleza kuwa amefariki wakati akipatiwa matibabu.

"Ni kweli huyo majeruhi amefikishwa hapa, lakini wakati tunampatia huduma alikata roho," alisema Dk. Sanga na kuongeza kuwa kifo chake kilichangiwa na kutokwa na damu nyingi.

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Sarah Chiwamba, alithibitisha tukio hilo na kufafanua kuwa simba aliyesababisha kifo hicho aliuawa na askari wanyamapori.

# Bil. 3/- kutafiti mbegu michikichi

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni tatu kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Kihinga mkoani Kigoma kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za kisasa za michikichi ili zitolewe bure kwa wakulima.

Lengo la mkakati huo ni kusaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini.

Fedha hizo pia zitatumika kujenga miundombinu na maabara ya kisasa ya kituo hicho ili kiweze kutoa huduma kwa wakulima wa michikichiki nchini.

Akitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi hiyo, Dk. Yohana Budeba, aliyetembelea kituo hicho kwa jili ya kufuatilia utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema kiasi cha fedha hizo kimeanza kuzalisha mbegu bora za michikichi aina ya Tenela na kuzigawa bure kwa wakulima katika mkoa huo.

Dk. Mkamilo alisema Tari Kihinga imepewa jukumu la kuzalisha mbegu bora za kisasa aina ya tenela milioni tano kupanua kilimo hicho ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini, hatua ambayo itaipunguzia gharama serikali kutumia fedha nyingi kuagiza mafuta hayo kutoka nje.

Alisema Tari Kihinga kwa kipindi kifupi imefanikiwa kuzalisha mbegu za michikichi aina ya tenela milioni 1.7 na kuzigawa kwa wakulima waliopo katika wilaya zote za mkoa wa Kigoma na kiasi kilichobaki uzalishaji wake utakamilika Julai mwaka huu.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa kituo cha Tari Kihinga, Dk. Filson Kagimbo, alisema uzalishaji wa mbegu aina ya tenela inayotoa mafuta tani tano kwa hekta, unafanywa kwa kuunganisha mbegu ya zamani aina dula na pesifela, ambazo uzalishaji wake ulikuwa wastani wa tani moja kwa hekta.

Dk Kagimbo, ambaye ni mtafiti wa michikichi, alisema mbegu za tenela zinazozalishwa kwenye nyuzi joto 40 kwa kutumia gemineta na nyingine kutumia teknolojia ya mapipa, zimeonyesha endapo zitaendelea kuboreshwa zaidi zitaongeza uzalishaji wa mafuta, hivyo kusaidia kumaliza tatizo la upungufu wa mafuta nchini.



Mafundi wakipaua moja ya madarasa mapya ya Shule ya Msingi Murangi, Musoma Vijijini, mkoani Mara juzi. Shule hiyo, kwa sasa ina madarasa saba na yanahitajika mengine tisa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Operesheni kusaka wahalifu mpaka Tanzania na Msumbiji

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

JESHI la Polisi nchini kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vimeimarisha ulinzi katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji kwa lengo la kukabiliana na vitendo vya uhalifu, yakiwamo mauaji.

Matukio ya vurugu na mauaji yamekuwa yakitokea Msumbiji, hivyo kuhatarisha usalama wa Tanzania.

Hayo yalisemwa jana mkoani Mtwara na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi nchini, Liberatus Sabas, alipokuwa akikagua kikosi maalumu cha kupambana na uhalifu nchini kilichowasili mkoani Mtwara kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

Alisema kwa siku za hivi karibuni, kumekuwapo na matukio ya uhalifu yanayofanywa na baadhi ya watu, yakiwamo ya mauaji kwenye maeneo ya mpaka na ndani ya Tanzania, na kwamba na Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwakamata wahusika na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Alisema baadhi ya wahalifu wamekuwa wakikimbia nchini na kwenda Msumbiji kisha kuungana na wahalifu wa nchi hiyo na kufanya vitendo vya uhalifu kwenye maeneo mbalimbali katika nchi hizo mbili.

Alisema katika operesheni hiyo watahakikisha wanawasaka kwa nguvu zote wahalifu hao na kuwakamata kisha kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Alisema lengo ni kuona vitendo vya uhalifu havipati nafasi nchini na Watanzania wanaishi kwa amani.

Sabas alisema wahalifu hao wamekuwa wakivamia kambi za jeshi, vituo vya polisi, kuchoma moto na kuchukua silaha Msumbiji kisha kuzitumia katika vitendo vya uhalifu kwenye maeneo mbalimbali ya nchi hizo.

Alieleza kuwa pia wahalifu hao wameripotiwa kuvamia benki na kuporwa fedha Msumbiji, hivyo Jeshi la Polisi nchini limeamua kuchukua hatua ya kuimarisha ulinzi katika mipaka hiyo.

Kamishna huyo alisema wananchi wana jukumu kubwa la kulisaidia Jeshi la Polisi katika kuwafichua wahalifu hao ili watambulike na kukamatwa.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa kuwasilisha taarifa za mtu yeyote ambaye wanamtilia shaka ili Jeshi la Polisi liweze kumfuatilia na kuchukua hatua zile zinazostahili dhidi yake.

# Wanne mbaroni tuhuma za wizi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu wanne katika matukio mawili tofauti, likiwamo la watu wanaodaiwa kuvunja duka la vifaa vya majumbani na kuiba vitu mbalimbali.

Duka hilo lipo eneo la Mtaa wa Polisi Manispaa ya Songea vyenye thamani ya shilingi 531,500.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema tukio hilo lilitokea Machi 27, mwaka huu, na kwamba majina yamehifadhiwa kwa sababu za kiupelelezi, walivunja duka la vifaa mbalimbali vya majumbani linalomilikiwa na Michael Shayo (24), mfanyabiashara na kuiba mali mbalimbali zenye thamani kiasi hicho cha fedha.

Kamanda Maigwa alitaja vitu ambavyo watuhumiwa walikamatwa navyo ni ndoo kubwa ya mafuta ya kula, vesti dazani moja, nguo za ndani dazani nne, mabunda mawili ya sigara, soksi jozi 10 na konyagi katoni moja.

Alifafanua kuwa askari waliokuwa doria walishuhudia watuhumiwa hao wakivunja duka na walifanikiwa kuwakamata wawili, ambapo baada ya kuwafanyia mahojiano walikiri kufanya matukio mbalimbali ya uvunjaji.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, polisi walifanikiwa kupata vitu mbalimbali vilivyoibwa katika matukio mengine.

Alitaja vilivyokutwa baada ya kuwahoji watuhumiwa hao ni runinga moja aina ya Codtec nchi 32, redio kubwa Anylup top, EFD mashine moja, runinga mbili aina ya Samsung nchi 32, runinga moja aina ya UK nchi 43, radio nne za subwoofer, kompyuta mpakato moja, power mixer moja, mixer moja na deki tatu.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma limewakamata watuhumiwa wengine wawili (majina yamehifadhiwa) kwa sababu za kiupelelezi wilayani Namtumbo, kwa tuhuma za kuvunja nyumba ya Musa Mohamed (40) na kuiba.

Kamanda Maigwa alisema watuhumiwa hao walikamatwa Machi 28, mwaka huu.

Kamanda Maigwa alitaja vitu vilivyoibwa ni runinga moja aina ya Panasonic nchi 18, redio moja aina ya Subwpoofer na speker zake aina ya aboder, deki moja aina ya Singsung, inverter 1 na heater moja.

Alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

# Ujenzi mahakama Uyui kuanza Julai

BUNGE limeelezwa kuwa ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Uyui mkoani Tabora ni miongoni mwa majengo ya Mahakama za Wilaya 33 yaliyopangwa kuanza kujengwa Juni mwaka huu kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Hayo yalibainishwa jana bungeni katika majibu yaliyotolewa na Wizara ya Katiba na Sheria kwenye swali la Mbunge wa Tabora Kaskazini(CCM), Almasi Maige (pichani chini).

Katika swali lake Mbunge huyo alisema Wilaya ya Uyui haina Mahakama ya Wilaya na ina Mahakama moja tu ya Mwanzo inayotumia chumba kidogo katika jengo la Mkuu wa Wilaya ya Uyui baada ya kutelekeza Mahakama ya Mwanzo ya Upuge.

"Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Uyui?, pia ni kwa nini Serikali ilitelekeza Mahakama ya Mwanzo ya Upuge pamoja na majengo yake katika kijiji cha Upuge?,"alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, yalieleza kuwa uhaba wa majengo ni moja ya kero kubwa inayoikabili Mahakama ya Tanzania na mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za Mahakama hapa nchini ni makubwa.

"Kwa msingi huo, Mahakama imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, lakini ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Uyui ni miongoni mwa majengo ya Mahakama za Wilaya 33 yaliyopangwa kuanza kujengwa mwezi Juni, 2020," Wizara hiyo ilisema.

Wizara hiyo ilibainisha kwa sasa Mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mchakato wa awali ili ujenzi wa majengo hayo uanze kwa muda kama ilivyo katika mpango wa Mahakama.

Pia ilisema Serikali haikulitelekeza jengo la Mahakama ya Mwanzo Upuge, sababu kubwa ilikuwa ni uchakavu wa jengo lenyewe ambalo halikuwa rafiki kuendelea kutumika kuendeshea shughuli za Mahakama.

Hata hivyo, Wizara ilishukuru Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Uyui kwa kuwezesha kupata ofisi kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma za mahakama ya Mwanzo Upuge wakati taratibu za ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya zikiendelea.



# Mamlaka Katibu Mkuu Kiongozi uhamisho watumishi yafafanuliwa



OFISI ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imesema marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, yamempa Katibu Mkuu Kiongozi mamlaka ya mwisho ya uhamisho wa watumishi wa umma.

Serikali imesema kwamba lengo la marekebisho hayo ni kutopingwa au kutotenguliwa na mamlaka nyingine.

Majibu hayo yalitolewa bungeni jana na Ofisi hiyo katika swali la Mbunge wa Tanga Mjini (CUF), Mussa Mbarouk (pichani), ambaye alisema Septemba 12, 2019 Bunge lilipitisha marekebisho hayo.

"Je, kwa kumpa mamlaka ya mwisho Katibu Mkuu Kiongozi hakutasababisha ukiritimba katika uhamisho wa watumishi wa umma?" alihoji.

Katika majibu ya swali hilo, Ofisi hiyo ilisema Sheria hiyo ya Utumishi wa Umma Sura 298, imefanyiwa marekebisho katika Kifungu cha 4(3) kupitia Kifungu cha 69 cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba 13 ya Mwaka 2019 kwa kumpa Katibu Mkuu Kiongozi mamlaka ya mwisho ya uhamisho.

"Hii imezingatia mamlaka yake kama Mkuu wa Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) cha Sheria hii, pamoja na Mamlaka hayo, Kifungu cha 8(2) cha Sheria hiyo kinampa Katibu Mkuu (Utumishi) Mamlaka ya kuwa Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi," ilisema.

Hata hivyo, ilisema katika kutekeleza majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi, Kifungu cha (3)(h) cha Sheria husika kinampa Katibu Mkuu (Utumishi) mamlaka ya kuhamisha watumishi wa umma kutoka Taasisi moja kwenda nyingine Tanzania Bara.

"Ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, Katibu Mkuu (Utumishi) amekasimu mamlaka yake kwa Katibu Mkuu (Tamisemi) ili aweze kuhamisha watumishi wa umma katika mamlaka za Serikali za Mitaa," ilisema.

Vilevile, ilisema Katibu Mkuu (Utumishi) amekasimu Mamlaka yake kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ili kuhamisha watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa yao.

"Pamoja na kukasimisha mamlaka yake, Katibu Mkuu (Utumishi) anaweza kuhamisha watumishi katika mamlaka za Serikali za Mitaa yeye mwenyewe pale inapobidi," ilisema.

Aidha, ilisema mamlaka hayo yatatumika kwa kuzingatia maslahi mapana katika utumishi wa umma au pale ambapo Katibu Mkuu Kiongozi hakuridhika na uhamisho uliofanywa na mamlaka nyingine zilizopewa au zilizokasimiwa madaraka hayo kama ilivyoelezwa.

# Mbunge ahoji ujenzi wa barabara Same-Mkomazi



MBUNGE wa Same Mashariki (Chadema), Naghenjwa Kaboyoka, (pichani) amehoji Serikali ina mkakati gani wa kutimiza ahadi ya Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Same-Kisiwani hadi Mkomazi ambayo inaunganisha majimbo matano.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema barabara hiyo inaunganisha jimbo la Same Magharibi, Same Mashariki, Mlalo, Mkinga na Korogwe Vijijini.

"Je, ni fedha kiasi gani zimetumika kuanzia mwaka 2015/2016 - 2019/2020 kwa ajili ya kukarabati barabara hiyo?" alihoji.

Kwa mujibu wa majibu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, barabara hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka.

Aidha, ilisema kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi 2019/20, kiasi cha Sh. bilioni 3.29 kimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo.

"Kufuatia kufanyika na kukamilika kwa upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina kwa kilometa zote za barabara hiyo kilometa 100.5," ilisema.

Hata hivyo, ilisema serikali kupitia Wizara hiyo imetenga kiasi cha Sh. bilioni tano katika Mwaka wa Fedha 2020/21 ili kitumike kuanza ujenzi kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wadau Tanzanite wasogezewa huduma

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WADAU wa madini ya Tanzanite mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, watanufaika na huduma za kibenki, baada ya benki ya NMB, kuanzisha huduma zake ndani ya ukuta unaozunguka machimbo ya migodi hiyo.

Baadhi ya wadau hao, wakizungumza na Nipashe baada ya gari la kutolea huduma, kufika katika eneo hilo, na kuanza shughuli ya huduma za kibenki, walishukuru kwa kusogezewa huduma hiyo karibu.

Mmoja kati ya wachimbaji wa madini, Hassan Ally, alisema hatua hiyo imeleta maendeleo makubwa kwa taasisi ya fedha kuwajali wadau waliopo ndani ya ukuta huo maarufu kwa jina la ukuta wa Rais John Magufuli.

Alisema watatumia huduma hiyo, kuweka akiba na kutoa fedha, huku akiwataka wadau wengine ambao hawajafungua akaunti wafungue ili kuondokana na tabia ya kutembea na fedha nyingi mfukoni.

Stanley Stephen, mwendesha pikipiki (Bodaboda), alipongeza hatua hiyo, kwa kuwa imewarahisishia kazi wadau hao.

"Hata sisi tutaweka akiba bila kutumia gharama za kwenda kwenye tawi la NMB Mirerani, tutakuwa tunamaliza mambo yetu ya kibenki ndani ya ukuta wa huu," alisema. Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mirerani, Allan Kombe, akizungumza na wadau hao, alisema huduma ya fedha imeanza kutolewa rasmi ndani ya ukuta huo, hivyo amewataka wadau hao kutumia fursa hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, akizungumza na wajumbe wa Mamlaka ya Mji Mdogo, waliochaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kipindi cha miaka mitano, katika kikao cha kwanza cha Baraza la Mamlaka hiyo wilayani humo, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mnyeti awatahadharisha wananchi wake

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara Alexander Mnyeti, amewataka wananchi wa mkoani humo, kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na serikali pamoja na wataalamu wa afya ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Pia, ametoa ovyo kwa wafanyabiashara wanaouza vitakasa mikono bei ya juu.

Alisema maelekezo ya serikali kwa wafanyabiashara wote watakaopandisha bei ya vitakasa mikono wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Mnyeti aliyasema hayo juzi, wakati alipotembelea kiwanda cha Mati Super Brands Ltd cha mjini Babati ambacho kinashirikiana na serikali kutengeneza vitakasa mikono ili kupambana na maambukizi ya virusi vya corona. "Tujitahidi sana kujikinga, kwa kuwa hatua hii sisi ndiyo tunaweza kufanya na siyo tusubiri ugonjwa uingie na uanze kusambaa, ndiyo tutafute matibabu, tutasumbuka sana, hivyo tujitahidi kujikinga kabla ugonjwa huu haujasambaa," alisema Mnyeti.

Katika ziara yake kiwandani hapo, Mnyeti ameupongeza uongozi wa kiwanda hicho, kwa kujali afya za wananchi, na kuwataka waendelee kuzalisha kwa wingi bidhaa hizo, ili wananchi wa mkoani humo na mikoa ya jirani wazipate kwa urahisi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Missaile Musa, alisema bidhaa hizo zitasaidia katika maeneo yenye uhaba wa maji.

Hata hivyo, alisema watawasiliana na uongozi wa wilaya za pembezoni ili wachukue vitakasa mikono na kuvisambaza kwa wananchi kwa kuwa uhitaji ni mkubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mati Super Brand Ltd, David Mulokozi, alisema wameamua kutengeneza vitakasa mikono ili kuwasaidia wananchi kujikinga na maambukizi ya virusi vya Covid 19, na wanawauzia kwa bei nafuu.

Mulokozi alisema, bidhaa hizo, wanauza kwa bei atakayomudu kila mwananchi.

"Vitakasa mikono tunauza kuanzia Sh. 1,500, kwa ujazo wa miligramu 50, Sh. 2,500 kwa ujazo wa miligramu 100, lita tatu ni Sh. 7,500 na lita tano ni Sh. 12,500," alisema.

Kiwanda cha Mati Super Brand Ltd kinajihusisha na utengezaji wa vinywaji vikali, kimeanza kutengeneza vitakasa mikono baada ya kuzuka kwa ugonjwa wa corona na nchi.

## Madiwani waridhia kuipandisha hadhi H/shauri

**Na Zanura Mollel,** ARUMERU

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Meru, limeridhia mapendekezo ya kupandisha hadhi halmashauri hiyo, kuwa halmashauri ya mji kutokana na kukidhi vigezo.

Uamuzi huo umefikiwa baada ya kipindi cha maswali na majibu kuwaridhisha madiwani.

Madiwani hao, walijadili kuhusu idadi ya watu, pamoja na namna maisha ya wananchi yatakavyobadilika baada ya halmashauri hiyo kupandishwa hadhi.

Mwenyekiti wa Kamati ya uchumi, ujenzi na mazingira, Handason Pallangyo, ambaye ni Diwani wa Kata ya Maji ya Chai, alisema endapo halmashauri hiyo, itapandishwa hadhi maisha ya wananchi wake yatabadilika.

"Tutakuwa na mpangilio mzuri wa mji na maisha ya wananchi yatabadilika,pia utaratibu wa kisheria utabadilika kulingana na sheria ya mipango miji kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa halmashauri hii ina ujenzi holela ambao hapo baadaye utakuja kuwa na athari kubwa," alisema.

Alisema mji utabalidisha mfumo wa maisha ya wananchi kwa kupata faida na fursa ambazo sasa hivi hawazipati.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Emmanuel Mkongo, alisema baada ya baraza hilo, kuridhia watakwenda kukusanya maoni ya wananchi na kurudisha kwenye baraza hilo, na baadaye watayapeleka katika vikao vya RCC na Tamisemi.

Mkongo alisema halmashauri hiyo, ikiwa na hadhi kuwa mji kuna mambo yatakayofanyika kwa kiwango kikubwa kwa lengo la kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Alisema hadi sasa halmashauri hiyo ina idadi ya wananchi zaidi ya 300,000.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Nelson Mafie, akisoma maazimio hayo, alisema watamuandikia barua Mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama wilayani humo, kumueleza hali ilivyokuwa mbaya.

# 17,000 vijijini Hai walilia majisafi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

ZAIDI ya wakazi 17,000 wanaoishi vijiji vya Kawaya na Rundugai katika Wilaya ya Hai, wanakabiliwa na kero ya kukosekana kwa huduma ya majisafi na salama kwa zaidi ya miaka 30.

Wakazi wa vijiji hivyo vilivyoko Kata ya Masama Rundugai wanalazimika kutumia maji hayo katika chemchem moja inayotumiwa pia kunywesha maji mifugo.

Kwa nyakati tofauti jana, wananchi wa vijiji hivyo wakizungumza na Nipashe kuhusu tatizo hilo, walisema hali hiyo inawaweka katika tishio la kupata magonjwa ya mlipuko.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Rundugai, Boniface Kodema, alisema wananchi na vijiji vya Kawaya na Rundugai wanalazimika kuamka usiku kutafuta maji katika chemchem ambayo siyo safi na salama kutokana na kutumiwa na mifugo na shughuli za kilimo.

"Tumeshakaa na viongozi wa serikali za Vijiji na Wilaya na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (Muwsa) kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika chanzo cha chemchem ya Mussa Toroka katika Kijiji cha Rundugai," alisema Kodema.

Mkurugenzi wa Mamlaka wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (Muwsa), Mhandisi Arron Joseph na Meneja Ufundi, Mhandisi Kija Limbe, walieleza kuwa zaidi ya Sh. bilioni 1.4 zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo mkubwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, huduma ya maji katika vijiji hivyo inatarajiwa kukamilika kabla ya Juni mwaka huu.




Mafundi mchundo wakikoroga zege kwa ajili ya kuanza ujenzi wa chumba cha mashine ya kusukuma maji katika chanzo cha maji cha Musa Toroka, katika Kijiji cha Rundugai, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro juzi, huku Meneja Ufundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (Muwsa), Mhandisi, Limbe Kija (kulia), akifuatilia kwa karibu. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# 650 waomba TRA kufunga biashara

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kilimanjaro, imepokea zaidi ya maombi 650 kutoka kwa wafanyabiashara wakiomba kufunga biashara za maduka na hoteli za kitalii kutokana sababu mbalimbali.

Miongoni mwa sababu walizozieleza ni watalii kusitisha safari zao za kuja kutalii na kupanda Mlima Kilimanjaro.

Meneja wa TRA, Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza wanahabari, na kuongeza kuwa licha ya maombi ya wafanyabiashara hao, TRA imekusanya zadi ya Sh. bilioni kumi sawa na asilimia 85 ya makisio yake kwa mwezi Machi mwaka huu.

Alisema TRA kila siku kuanzia mwezi Januari mwaka huu imekuwa ikipokea wastani wa barua za maombi zaidi ya 30 kila siku kutoka kwa wafanyabiashara wakiomba kusimamisha biashara zao kwa muda, wengine moja kwa moja kutokana na mwenendo wa biashara zao.

Pia alisema tushio la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa homa ya mapafu corona, nao ukichangia kwa kiasi kikubwa.

Gabriel alisema TRA kuanzia leo itafanya uhakiki maduka na biashara zote zilizoombewa kufungwa, na kwamba kama mfanyabiashara atabainika kuomba kufunga biashara yake huku akiendelea na biashara, mamlaka hiyo itawaburuza mahakamani na kuwatoza faini.

Alisema kuanzia leo maofisa wa TRA watazunguka mitaani kukagua biashara zilizozofungwa na kila mfanyabiashara atapaswa kuonyesha mali zilizobakia na endapo kutakuwapo na ulaghai, mamlaka hiyo itawaburuza mahakamani.

Alisema Machi mwaka huu, TRA ilikusanya zadi ya asilimia 85 ya makisio ya makusanyo ya mapato, na kwamba hatua hiyo imefikiwa baada ya wafanyabiashara mkoani hapa kuwa na mwamko wa kulipa kodi kutokana na elimu na mahusiano mazuri kati ya wafanyabiashara na watumishi wa mamlaka hiyo.

Alisema kwa siku mbili mfululizo Machi 30 na 31 mwaka huu, watumishi wa TRA mjini Moshi walikaa ofisini hadi saa nne za usiku wakiendelea kutoa huduma kwa wafanyabiashara waliojitokeza kwa wingi kulipa kodi kabla ya Machi 31 kumalizika.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kuacha tabia ya kujitokeza tarehe za mwisho za ulipaji wa kodi ili kuepuka kutozwa faini kwani hali hiyo inasababisha msongamano wa walipakodi na kiwakwamisha watumishi wa mamlaka hiyo kutoa huduma bora.

Gabriel alisema ili kuepuka misongamano isiyokuwa na ulazima na kuzuia kuenea kwa maambukizi ya corona katika ofisi za TRA na benki, wafanyabiashara hawanabudi kujenga utamaduni wa kulipa kodi kabla ya tarehe za mwisho.

Alisema TRA mkoani hapa imeendesha kampeni ya utoaji elimu na faida za ulipaji kodi na wafanyabiashara kuwa na mwamko wa kulipa kodi.

Gabriel alisema tishio la corona limesababisha kusitishwa kwa safari za watalii kuja kupanda Mlima Kilimanjaro na kutembelea hifadhi wanyamapori, hivyo kuathiri biashara ya utalii kwani hata hoteli za kitalii zimepunguza ama kuwaondoa wafanyakazi wanaotoa huduma kwa wageni wa utalii.

Alisema amefanya ukaguzi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na kubaini hakuna ndege yoyote kutoka mataifa ya nje wanaokuja kufanya utalii isipokuwa ndege zinaotoa huduma za kusafirisha abiria wa ndani.

## DC azuia mchakato zabuni ya barabara

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesimamisha mchakato wa zabuni ya kumtafuta mkandarasi atakayefanya kazi ya ukarabati wa dharura wa babaraba ya kuingia na kutoka katika Kituo Kikuu cha mabasi cha Bomang'ombe.

Jana, Ole Sabaya alitangaza serikali kuifuta zabuni hiyo, baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai kueleza ilipanga kutumia Sh. milioni 15 kufanya ukarabati wa kuziba mashimo ya kuingia na kutoka katika stendi hiyo.

"Mkurugenzi Mtendaji na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ambaye wewe ni mshauri, nimefuta hiyo zabuni kuanzia sasa, anzeni upya mchakato.

" Tunaonekana wasanii kila siku kwa kuziba viraka halafu muda mfupi tu vinabanduka na kusababisha adha kwa abiria na hasara kwa wenye vyombo vya usafiri. Mlipoziba kipindi kilichopita mmesema mmetumia milioni 17 na sasa mnataka tena kutumia milioni 15, hapana," alisema.

Awali akitoa maelezo kuhusu zabuni iliyotangazwa kitafuta mkandarasi, Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, John Sospeter, alisema ukarabati huo ungehusisha kipande chenye urefu wa mita 220.

Ole Sabaya alikwenda katika eneo la kituo hicho, baada ya madereva wa mabasi ya abiria kupaza sauti, wakilalamikia serikali kwa kushindwa kukarabati miundombinu ya stendi ya mabasi ya Bomang'ombe.

Kituo hicho cha mabasi kinatumika kupakia na kushusha abiria katika mabasi yaendayo mikoani na ndani ya wilaya hiyo.

Wiki iliyopita, baadhi ya madereva katika stendi hiyo walisema eneo hilo limesahaulika kwa muda mrefu bila kukarabatiwa.

Hassan Mbaga, dereva wa basi dogo linalofanya safari zake, kati ya Moshi na Arusha, alisema hali ambayo imesababisha kuwapo na mashimo yanayosababisha mabasi yao kuharibika licha yakuwa wanalipa ushuru.

Naye, Frederick Tesha, alisema katika kituo hicho barabara ya kutoka na kuingia imejaa mashimo makubwa na inapitika kwa shida.

ama
ALHAMISI APRILI 2, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Mbinu za kukwepa kuketi, ili kujiongezea uhai



Ukurasa 16

NIMR yazama kutafiti mitimshamba, dawa mbadala ikiiga China na India



Ukurasa 19

## Unajua kumkaripia, kutomjibu anayouliza unamdhuru mtoto?



WENYE ULEMAVU MAMA, MWANA

# Kutembea, shule, mlo na kulala shida zisizoelezeka

Ukurasa 14



Watu wamekaa wakiangalia televisheni. **PICHA: MTANDAO.**

## Mbinu kukwepa kuketi, kujiongezea uhai

**Na Mwandishi Wetu**

TAFITI za kutoka nchi Australia zinabainisha kila siku ambayo mtu anaketi kama kuangalia luninga, anapunguza uhai wake kwa dakika 22.

Kuketi kwa zaidi ya saa moja mfululizo, pia kunaathiri uwezo wa mwili kudhibiti sukari, shinikizo la damu na matumizi ya mafuta, hivyo inaongeza uwezekano wa kupata magonjwa yanayoambatana nayo, pamoja na saratani.

Vilevile mtu anapoketi muda mrefu, kunaelezwa kunaongeza uwezekano wa mwili kunyooka vizuri na kusababisha shida ya maumivu ya mgongo uzeeni.

Inashauriwa mtu azoeshe mwili wake kwa matendo kama kusimama, kutembea na kunyoosha viungo, kwa muda kati ya saa moja na mawili kila baada ya kuketi.

AFYA

WENYE ULEMAVU MAMA, MWANA

# Kutembea, shule, mlo na kulala shida zisizoelezeka

• Nafasi masomo kwa 'mbinde' • Mahudhurio lazima mama



Joackim Edmund, akiwa na mama yake, Amina Kisembe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**Na Beatrice Philemon**

LIKUWA siku ya Jumamosi iliyopita, majira saa saba na dakika 51 mchana, nilipokuwa nimefika kumuona nyumbani, Joackim Edmund.

Huyo ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Tungini, iliyopo Mtaa wa Madenge, eneo la Chanika, wilaya Ilala, Dar es Salaam, ambaye kiumri amewazidi wenzake darasani.

Ukaribisho huo ulianza kwa hatua, baada ya kufahamisha mama huyo, Amina Kisembe, alimtuma mtu kutupokea kutoka upande wa kituo cha basi na baada ya kufika nyumbani, Mama wa Joackim, aliwakaribisha kwa utaratibu maalum.

Aliomba wageni tukae kwenye kitanda na mtoto Joackim, ahamie katika kiti chake, ili kuweka sawa ulingo wa mazungumzo ya Nipashe na wanafamilia hao.

> "Hapo bado kumuona dokta, vipimo, usafiri, matibabu na mengine yaani ni zaidi ya milioni ila sina jibu sahihi.

Ni katika ushuhuda wa kwanza na mwanahabari mwenzangu, tulimuona mtoto huyo akiwa katika hali ya ulemavu wa miguu yote miwili, akipata shida wakati wa kukaa mpaka apate cha kuegemea.

Lakini unapomtajia suala la elimu, ndio kwanza utashi uko juu na daima hajakata tamaa na hali yake. Hapo, nikiwa na mwenzangu tukikaribishwa nyumbani kwao Chanika nke kidogo ya Dar es Salaam, alikuwa na madaftari yake anasoma.

Pale tu mazungumzo yalipoanza na kugusa ulemavu wake, ghafla mtoto huyo alianza kulia kwa uchungu mkubwa, huku akimuangalia mama yake na akatamka:

" Hebu angalia mimi nilipo ni mwenye ulemavu, mama yangu pia ni mwenye ulemavu, mama hana hela ya kunipeleka hospitali kupata vipimo vikubwa katika Hospitali ya Muhimbili, pia tunaishi maisha ya taabu sana inaniuma sana."

Joackim anaelekeza ombi kwa wafadhili kutoka maeneo mbalimbali wamsaidie kupata vipimo vikubwa na usafiri wa pikipiki wa 'Bajaj' ili mama yake aweze kumpeleka shule na usafiri huo utumike kibiashara, kuwapatia kipato cha kumudu maisha ya kila siku.

"Kwa sababu mama ananipeleka shule kwa shida, anatembea kwa miguu, huku akinisukuma kwenye baiskeli (wheel chair) hadi shule, akifika shule inabidi tena anisubiri hadi nimalize kusoma ndiyo anirudishe nyumbani," anasema.

Kutokana na hali hiyo, mama huyo anasema sasa ameshindwa kufanya biashara, familia yao inaendelea kuishi maisha duni, kula kwa shida, hadi anashindwa kupata huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa ajili ya mwanawe.

"Sina uwezo. Natamani mtu yeyote au kampuni mbalimbali wanisaidie, ili niweze kupata vipimo na Bajaj, ili niweze kusoma vizuri kwa sababu nikisoma nitaweza kumsaidia mama yangu," anasema Joackim.

"Mbali na hilo mama aliniambia kuwa, madaktari wa CCBRT walisema kama akipata mfadhili wa kumlipia vipimo vikubwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, ataweza kutembea vizuri na kuendelea na masomo yake vizuri." anaeleza.

### MAMA YAKE

Mama yake alipoulizwa kuhusu gharama za vipimo alijibu: "Gharama za vipimo ni kubwa sana. Pia, baba yake Joackim ni mzee na ana matatizo ya macho haoni vizuri.

"Pia, gharama za Muhimbili siyo rahisi kuzijua mpaka ufike kule, lakini ni kubwa kwa sababu nasikia kiatu kimoja cha kufanyia mazoezi ni Sh. 150,000, ikiwa miguu miwili ni Sh. 300,000.

"Hapo bado kumuona dokta, vipimo, usafiri, matibabu na mengine yaani ni zaidi ya milioni ila sina jibu sahihi," anasema.

### NDOTO YAKE

Joackim anasema, kama akisoma na kumaliza elimu yake anatamani kuwa daktari kama mama yake mkubwa ambaye anatumikia Hospitali ya Mirembe, iliyoko Dodoma.

"Ila mimi ninachoomba wanisaidie Bajaj ya kwenda shule na kufanya biashara, ili mama yangu aweze kunipeleka shule na hatimaye niweze kutimiza ndoto zangu na huduma zingine za kijamii," anasema.

Akizungumzia hali ya mtoto wake akiwa na uso wa huzuni, Amina anaomba wafadhili wamsaidie aweze kwenda kwenye vipimo vikubwa, akiamini vitamuwezesha Joackim kutembea vizuri.

AFYA

# Kutembea, shule, mlo na kulala shida zisizoelezeka

"Joackim anahangaika sana. Ukimwangalia mwanangu anapenda sana kusoma, lakini changamoto yake kubwa ni ulemavu alionao," anasema Amina .

Anasema hivi sasa hali yake imezidi kuwa mbaya zaidi, kwa sababu yeye mtoto wake hawana shughuli yoyote ya kuwaingizia kipato, hali inayowafanya waegemee mlo mmoja wa kubahatisha.

Ni ombi analoambatanisha na makazi jirani, kwa sababu sehemu wanakoishi wamepanga na gharama ni kubwa, wakitegemea wafadhili kuwalipia kodi.

### ILIKUWAJE?

Amina ana simulizi kwamba, alizaliwa mwaka 2006 akiwa mtoto njiti, katika Hospitali ya Rufani ya Temeke na baada ya hapo kutokana na hali hiyo, alihamishiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, akikaa kwa mwezi mmoja akihudumiwa.

"Mungu akanisaidia mwanangu akaongezeka uzito, nikarudi nyumbani," anasimulia, huku akifafanua: "Tangu nilipojifungua huyu mtoto ndiyo matatizo yalianza ya kutofanya kazi.

"Ikabidi nikae nyumbani namlea yeye tu mpaka alipofika mwaka mmoja na miezi saba, alikuwa hajakaa wala kutembea, ndipo nilipowasikia CCBRT, nikaenda kule kuanza mazoezi."

Anaeleza mazoezi ya afya ya mtoto aliyopata hospitalini CCBRT, ilimuwezesha mtoto kuanza kukaa na kutambaa, lakini alishindwa kumbeba kuendelea, akilalama alielemewa na uzito wa mtoto akidaiwa alishakuwa mkubwa.

Mama Amina anaendelea kusimulia kwamba, mpaka umri mkubwa wa mtoto akiwa nyumbani, alilazimika kumtafutia shule, Joackim akiwa ameshalemaa miguu yote miwili.

"Nimejaribu kumtafutia shule ya kusoma imekuwa ni kikwazo kulingana na ulemavu alio nao. Kwanza, nilimpeleka Shule ya Msingi Kimwani (Chanika) wakasema hawezi kusoma pale," anadokeza na kuendelea:

"Nikampeleka tena Shule ya Msingi Gogo (Chanika). ikawa hivyo hivyo wanasema mazingira siyo rafiki kwake, wakasema wenzake watampiga na yeye anatembea na wheel chair(baiskeli ya kusukumwa )."

Anasema, katika Shule ya Msingi Kimwani, mazingira ya vyoo siyo rafiki kwake na alipoamua kumpeleka katika Shule ya Jeshi la Wokovu, aliambiwa umri wa kuanza darasa la kwanza ulishapita, hakubaliki.

"Niliamua kwenda kwa Ofisa Elimu Mkoa na Ofisa Elimu Wilaya ya Temeke. Kwa hiyo, Ofisa Elimu Mkoa akaniandikia barua nije Shule ya Msingi Tungini, nashukuru Mungu mwaka huu mwezi wa pili, pale walimpokea na miundombinu ni rafiki.

"Tatizo nililo nalo kwa muda huu, sina usafiri wa kumsafirisha kutoka ninapokaa hadi shuleni na kutoka (Chanika ) Kwa Ngwale hadi Tungini ni muda wa saa moja na nusu," anasimulia mama huyo.

Anasema ni kawaida mtoto anapoenda shuleni, yeye mama anamsubiri pale pale shuleni, ilhali hana hata biashara nyingine anayoifanya kumkimu kimaisha.

Ni maisha anayoeleza mama huyo, ni wakazi katika nyumba ambayo kodi yake ni Sh. 40,000, pamoja na umeme analipa jumla Sh. 50,000 kwa mwezi.

"Hivi sasa hali yangu inazidi kuwa mbaya zaidi, kwa sababu sifanyi biashara yeyote, mtoto pamoja na mimi tunahitaji kula na mahitaji mengine," anasema.

### KABLA KUJIFUNGUA

Anarejea nyuma alikotokea, kwamba kabla hajajifungua mtoto Joackim mwaka 2006, maisha yake yalikuwa mazuri, alipokuwa anafanya kazi za ufundibomba kwa muda wa miaka nane, alikoajiriwa na kampuni ya uhandisi ujenzi mkoani Dodoma .

Amina, anasema mkataba wake ulipoisha mwaka 1992, alianza kufanya biashara zake na alikuwa na uwezo wa kupata wastani wa kati ya Sh.20,000 na 300,000 kwa siku kulingana hali ya siku kibiashara.

Mama huyo anafafanua kwamba, alikuwa ananunua chupa za maji, vifuu vya nazi, ndoo za plastiki na madumu ama yaliyopasuka au kuchakaa na kisha aliyauza viwandani.

"Kwa mfano kwenye mzigo wa kopo, kama ukipeleka kiwandani tani moja hadi moja na nusu, ulikuwa unapata Sh. 300,000 na kilo moja ya chupa ilikuwa inauzwa Sh.300," anasema.

Pia, anazungumzia biashara ya vifuu vya nazi alivyouza katika kiwanda kimojawapo jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kutengenezea dawa za mbu ilimpatia wastani wa Sh. 90,000 kwa siku kilo ikiuzwa kwa bei ya Sh. 30.

Upande wa ndoo za plastiki, Amina anasema alipeleka madumu katika kiwanda cha plastiki, yaliyompa kipato, lakini baada ya kujifungua Joackim, alisitisha yote na kuingia katika ukurasa mpya wa maisha magumu.

Anaitafsiri kuwa sehemu kubwa ya muda wake anatumia kumuangalia na kuhudumia mtoto wake, sasa miaka nenda rudi, jambo linalomfanya aombe kusaidiwa walau cherehani, kurekebisha hali ya kipato chake na familia.

***Amina Kisembe, mama wa Joackim Edmund, anapatikana kwa namna za simu: (+255)0682374977.***



Joackim Edmund, akiwa katika picha binafsi chumbani kwake, Chanika jijini Dar es Salaam. PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA.

> **Nikampeleka tena Shule ya Msingi Gogo (Chanika), ikawa hivyo hivyo wanasema mazingira siyo rafiki kwake, wakasema wenzake watampiga na yeye anatembea na wheel chair (baiskeli ya kusukumwa).**



AFYA

# NIMR yazama kutafiti mitimshamba, dawa mbadala ikiiga China na India

• Nguvu za kiume dawa iko jikoni


Wataalamu wa NIMR wakiwa kazini katika maabara yao. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Taifa ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR), sasa inaingia katika orodha ya taasisi kongwe nchini, ikibeba umri miaka 41 tangu ilipoanzishwa kisheria mwaka 1979.

Hadi sasa kimuundo, ina idara ya utafiti za tiba asili, zenye jukumu la kutafiti dawa za mitishamba, zinazotumika kwa miaka mingi sasa.

Katika moja ya mafanikio ya karibuni, NIMR imetafiti na kufanikisha tiba inayokinga au kupunguza vifo vya wagonjwa wenye maambukizi ya fangasi zinazosababisha homa ya uti wa mgongo, hasa kenye maambukizi ya virusi vya Ukimwi, pia maboresho ya kutibu kifua kikuu.

**PROF. MFINANGA**

Mkurugenzi wa NIMR, Kituo cha Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Sayoki Mfinanga, anasema serikali hivi sasa inafanya utafiti unaolenga kutathmini mkakati wa tiba kinga, kupunguza vifo kwa wagonjwa wenye maambukizi ya fangasi.

Hiyo inaelezwa kuwa na kawaida ya kusababisha homa ya uti wa mgongo, kwa wagonjwa wenye maambukizi ya Ukimwi.

Pro. Mfinaga anataja jina la fangasi hizo kwa jina la 'cryptococcus' inayochangia asilimia 25 ya vifo vya wagonjwa wenye maambukizi ya Ukimwi nchini.

> **Uwezo wa kituo wa kufanya utafiti umeongezeka kutoka wastani wa utafiti kubwa 10 kwa mwaka kwenye miaka ya nyuma, kuanzia 2010 mpaka wastani wa utafiti kubwa 20 mwaka 2017.**


Mkurugenzi wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Yunus Mgaya.


Mkurugenzi wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR), kituo cha Hospitali ya Taifa Muhimbili. Prof. Sayoki Mfinanga.

Ni utafiti anaosema, ulifanyika katika nchi mbili za Tanzania na Zambia na ulihusisha jumla ya watu 1,999 wenye Ukimwi na waliambukiza fangasi hao kwenye damu, ingawa ilikuwa haijafikia kiwango cha kusababisha ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo.

Anasema, matokeo ya utafiti yalionyesha kupunguzwa maambukizi kwa asilimia 30, ikilinganishwa na utaratibu wa zamani wa kutotumia tiba kinga kwa waathirika.

"Matokeo ya utafiti huu yametumika kutengeneza mwongozo wa kimataifa wa Shirika la Afya Duniani (WHO) wa kuzuia ugonjwa wa uti wa mgongo unaosababishwa na fangasi kwa wenye Ukimwi," anasema Prof. Mfinanga.

Aidha, anasema walifanya utafiti wa tiba ya homa ya uti wa mgongo kwa wenye Ukimwi, uliotathimini mkakati wa tiba kupunguza vifo kwa wagonjwa wenye maambukizi ya fangasi.

Mkurugenzi huyo anasema, utafiti ulihusisha jumla ya wagonjwa 721 nchini, pamoja na mataifa jirani ya Malawi, Zambia na Cameroon na mkakati ulilenga kutumia mchanganyiko wa aina mbili, zilizofanikiwa kupunguza vifo kwa wastani wa robo tatu ya kila wagonjwa 100 waliotibiwa.

Anasema, utaratibu wa zamani unaotumia dawa ya aina moja, ulipunguza vifo kwa wastani wa robo ya kila wagonjwa wanaotibiwa homa ya uti wa mgongo.

Prof. Mfinanga anasema, matokeo ya utafiti huo yamepelekwa WHO kwa ajili ya kuunda sera mpya ya kutumia michanganyiko wa dawa hizo kutibu ugonjwa wa homa hiyo ya uti wa mgongo.

**UTAFITI WAONGEZEKA**

Prof. Mfinanga anasema, miongoni mwa mafanikio ya miaka minne ya serikali, ni pamoja na hivi sasa kumeongezeka utafiti kutoka 10 hadi 20 kwa mwaka.

"NIMR-Muhimbili tumefanikiwa kufanya utafiti mbalimbali kwenye magonjwa ya kifua kikuu, vimelea vya Ukimwi na magonjwa yasiyoambukiza.

"Uwezo wa kituo wa kufanya tafiti umeongezeka kutoka wastani wa utafiti kubwa 10 kwa mwaka kwenye miaka ya nyuma, kuanzia 2010 mpaka wastani wa utafiti kubwa 20 mwaka 2017," anasema Profesa Mfinyanga.

Anasema, miongoni mwa utafiti huo ni pamoja unaohusu huduma za kudhibiti Ukimwi na kifua kikuu, uliochangia ama kuboresha au kutoa taarifa zilizoboresha huduma za kudhibiti Ukimwi na kifua kikuu.

**MITISHAMBA DAWA**

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, anasema, hivi sasa wapo mbioni kusimika mtambo wa kisasa utakaosaidia kuzalisha dawa za mitishamba, ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali nchini.

Hadi sasa, Prof. Mgaya anataja magonjwa hayo hatari kuwa ni tezi fume na seli nundu, yatakayotibiwa kwa kutumia dawa za mitishamba zilizofanyiwa utafiti nchini.

Anasema, serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, imetoa fedha Sh. milioni 800 zitakazosaidia kununua mitambo na kukarabati eneo patakaposimikwa mitambo hiyo.

Prof. Mgaya anasema, mtambo umeshaagizwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Sh. milioni 600 kati ya Sh. milioni 800 zitatumiwa kusimika mtambo na kufanya kazi kuhakikisha unaanza kutoa huduma.

Anasema, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), ilitoa fedha Sh. milioni 400 kwa ajili ya kujenga maabara ya kuweka mtambo huo, pindi utakapowasili.

"NIMR tupo mbioni kuleta mtambo kutoka China, ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha dawa kutoka kwenye miti dawa kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kukabiliana dhidi ya magonjwa mbalimbali, ambayo yanawagusa wananchi.

"Watalaamu wetu tayari wameshaenda China kujifunza na wametembelea kampuni za mitambo hiyo ya kisasa na tumejiridhisha," anafafanua Prof. Mgaya, akidokeza ndizo dawa zinazotumiwa na waganga wa kienyeji nchini.

Anaendelea: "Sisi tutatengeneza dawa kutokana na asili ya miti dawa. Tunachokifanya ni kutafiti, badala ya kwenda kwa mganga ambaye atakumiminia kwenye kikombe.

"Sisi tutakachokuambia ni kuwa, dawa hiyo ina mchanganyiko wa kiambata fulani na utaitumia kwa kiwango fulani."

Mtaaluma na bosi huyo mkuu wa NIMR, anasema tiba rasmi ya mitishamba duniani imezama zaidi hasa katika nchi mbili, akiwa na ufafanuzi zaidi: "China na India kuna Hospitali kabisa zinatibu kwa kutumia dawa za mitishamba na nchi ya Korea."

Anasema asilimia kubwa ya dawa zinazotumika huko ni miti shamba, isipokuwa zinatengenezwa katika maabara ili kuondoa uasili, kwa sababu hakuna miti ya kutosha kutengeneza dawa nyingi za asili.

Prof. Mgaya anasema, dawa wanayotengeneza hivi sasa ni za asili kutoka miti iliyofanyiwa utafiti kwa ajili ya kutibu magonjwa yatakayolengwa.

Anasema, tofauti ya dawa hizo na zile za waganga wa jadi, ni kwamba zitakuwa zinaeleza kiwango cha dawa iliyopo kwenye ujazo na maelezo ya maabara, kanuni za matumizi yake.

"Kikubwa naishukuru serikali kwa fedha ilizotoa kwa ajili ya kununua mtambo huu wa kisasa wa kutengeneza dawa hizi," anasema Prof. Mgaya, akifafanua wataanza na dawa za kutibu tezi dume na seli nundu, kwa sababu malighafi yake yanapatikana kirahisi na haraka,

Kwa mujibu wa Prof. Mgaya, hatua za baadaye zitahusu dawa za kutibu magonjwa mengine sita, ambazo upatikanaji wa malighafi yake unahitaji maandalizi.

> **Sisi tutakachokuambia ni kuwa, dawa hiyo ina mchanganyiko wa kiambata fulani na utaitumia kwa kiwango fulani.**

**TIBA MAUMBILE**

Hadi sasa taasisi hiyo inasema imeshaanza kutafiti tatizo la upungufu wa nguvu za kiume akihusisha na mikoa ya Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Dodoma.

Prof. Mgaya anasema, hivi sasa wanatafakari kitaalamu sababu ya tatizo hilo na namna ya kudhibiti, akiahisi pindi kazi hiyo itakapokamilika, watatoa taarifa kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ili ichukue hatua ya kudhibiti tatizo hilo.

Kuhusu dai la haja ya matumizi ya dawa za kuongeza makalio, Prof. Mgaya, anasema hadi sasa hawajaanza kufanya kutafiti huo na kama wataona kuwapo umuhimu wa kufanya hivyo, watalazimika kuchukua hatua stahiki.

## Kijue kitunguu saumu kilivyo 'mali' mwilini


Kitunguu saumu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KITUNGU saumu ni jamii ya vitunguu inayotumika kama kiungo katika mboga na tiba ua afya. Mmea hiyo humea, baadhi chini na juu ya ardhi.

Upande wa afya kwa mwanadamu, inatajwa kuwa na faida nyingi. Ili kwenda nayo vizuri, ni vyema kutumia kiasi kidogo wastani usiozidi punje sita na ndani ya kati ya wiki mbili na mwezi mmoja, faida yake huanza kuonekana.

Iwapo mtu anatumia kitunguu saumu na kichwa kinauma zaidi, anaweza kupumzika siku mbili na baadaye anaendelea.

Kinaweza kutumika kusafishia vidonda katika tiba yake na zipo dawa zinazotengenezwa kwa kutumia jamii hiyo ya vitunguu, ikiwemo ya kusafisha mdomo.

Pia, kitunguu saumu, kina uwezo wa kutibu maambukizi ya bakteria, fangasi na virusi vya aina mbalimbali, vivyo hivyo inasaidia kuzuia magonjwa ya moyo kwa kusaidia kurekebisha shinikizo la damu.

Eneo lingine, ni kwamba linasaidia kudhibiti kiwango cha sukari katika damu. Inashauriwa kwamba, wagonjwa wa kisukari wanaotumia sindano za 'insulini' wasitumie kitunguu saumu, isipokuwa anapopata ushauri wa daktari.

**FAIDA TIBA**

Kwanza, vina uwezo wa kutanua mishipa ya damu (vasodilatation) kwa kubadilisha viungo viitwavyo 'polysulfide' zilizopo ndani yake kuwa 'hydrogen sulfides' kwenye seli nyekundu za damu.

Pili, inasaidia kudhibiti kiwango cha sukari mwilini kwa kupunguza kemikali aina ya 'homocystine' na kupunguza madhara ya kisukari.

Tatu, iwapo vitapondwa vizuri, vitunguu saumu hutoa kemikali iitwayo 'allicin' ambayo ni dawa dhidi ya bakteria na 'phytoncide' inayoua fangasi wa aina mbalimbali.

Nne, harufu mbaya ya kitunguuu swaumu, inatokana na gesi aina ya 'hydrojeni sulfide' inayotolewa baada ya kuvila.

**MAGONJWA INAYOTIBU**

- Inayeyusha mafuta mwilini (kolestro).
- Husafisha njia ya mkojo na kutibu (U.T.I).
- Hutibu amiba, minyoo na bakteria wengine.
- Inazuia kuhara damu, tumboni inaondoa gesi, msokoto wake na tiba homa ya matumbo
- Huondoa mabaka ya ngozi
- Tiba mafua na malaria.
- Kwenye kifua kikuu inapotumiwa, siku ya pili mtumiaiji anatokwa na makohozi mengi, ikiwa ishara ya tiba.
- Inadhibiti kipindupindu;vipele mwilini na mba kichwani.
- Huzuia meno kung'oka na kutibu maumivu.
- Inasaidia nguvu za kiume.
- Tiba ya maumivu kichwa, kizunguzungu na kuipa nguvu ubongo.
- Inaondoa tatizo la kukosa usingizi, msongo wa mawazo na kinga ya mwili na kwa muda mfupi.
- Inazuia shinikizo la juu la damu; saratani.
- Hutibu maumivu ya goti.
- Inasaidia mmeng'enyo wa chakula na kuongeza hamu ya kula.
- Huzuia damu kuganda na inatibu kisukari

**KASORO ZAKE**

- Harufu mbaya mdomoni kutokana na kemikali ya 'Allyl methyl sulfide.' Ni hali inayopunguzwa kwa kunywa maziwa, maji mengi au kutafuna karafuu.
- Baadhi ya watumiaji, inawaletea mzio mwilini (allergies au inflammatory reactions)
- Kichefuchefu, kutapika na kuharisha kwa muda mfupi.
- Inaweza kusababisha hatari ya kuvuja damu, kwa sababu inazuia kazi ya seli sahani (platelets) zinazosaidia damu kuganda, hususani kwa wajawazito baada ya upasuaji au baada ya kujifungua.
- Huingiliana katika kazi mwilini na dawa kadhaa, hata kuathiri ufanisi wake .
- Inaelezwa kuwa na madhara kwa wanyama jamii ya paka na mbwa.

**Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali.**

AFYA

# Unajua kumkaripia, kutomjibu anayouliza unamdhuru mtoto?

• Mtaalamu afunguka yaliyojificha



Watoto wakicheza na mwalimu wao, Rehema Laizer, katika kituo cha kulea watoto cha Yeyo Care Centre, kilichopo mjini Babati. **PICHA: JALIWASON JASSON**

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

NI janga linalochukua sura ya mazoea zaidi. Ni tofauti ya zama zilizopita mtoto akiwa na thamani ya kipekee. Ulikuwa utamaduni wa asili, watu wakiwa na mtazamo mmoja kuhusu namna ya kumlea mtoto.

Leo hii kuna mitazamo tofauti inayohusu malezi ya watoto. Wazazi wanaamini mtoto anaweza kulelewa na mtu yeyote, kama wazazi hao wa mtoto wamebanwa na majukumu mengine ya kimaisha.

Lakini wapo watu wachache waliobaki kwamba, ni lazima mtoto akapata malezi salama ya mama na baba, bila kujali wanabanwa na majukumu ya kila siku au la.

**KIJIJINI MAGUGU**

Dukuduku na ufuatiliaji wa hilo kinachojiri katika mada hiyo mkoani Manyara, ndicho kimefikisha Nipashe katika kijiji chenye sura ya mji mdogo wa Magugu, wilayani Babati.

Hapo ndipo kuna Mratibu wa Mradi wa Maendeleo Magugu, Majid Mfinanga, kutoka Shirika la World Vision Tanzania, anayekiri ushuhuda wa mikasa ya ukatili na hatari zake.

Mfinanga anaingia ndani na dhana yake, akisema zaidi ni kwa watoto wenye umri wa miaka na kushuka chini, ukatili dhidi yao unaongezeka kwa kasi kubwa, hukua akitaja mipaka ya ulinzi wa

> **Licha ya kwamba ulinzi wa ustawi wa jamii ni haki ya wote, theluthi mbili ya watoto wote duniani sawa na watoto bilioni 1.3 hawapati ulinzi.**

mtoto ni kuanzia nyumbani hadi shuleni, kumhakikishia ukuaji mzuri.

Je, ni kwanini mtoto anatakiwa kupata ulinzi wa uhakika? Mtaalamu huyo anasema uwezo wa mtoto kujilinda ni mdogo, hivyo mtu mwenye nia ovu ni rahisi kumdhuru na hayo yanatokea.

"Wanaobaka watoto wanafanya kwa sababu ya imani za kishirikina na ni rahisi kurubuniwa, kwa kuwa akili yao bado ni ndogo kupambanua mambo na kubaini mazingira ya mtu mzuri au mbaya, ili ajiepushe naye," anaeleza Mfinanga

Mtaalamu huyo anayejitambulisha ana taaluma ya ualimu na amewahi kuwa mkufunzi katika vyuo vya ualimu, anasema kuna matukio wazazi na walimu wamekuwa wakiwafanyia ukatili watoto wao bila wao kujijua, akitoa mfano mtoto anahitaji kucheza na mzazi anamzuia.

Mwalimu Mfinanga anasema, kuna wanaowakaripia watoto, pindi wanapowauliza maswali na hawawajibu, wajihisi kisaikolojia ni sawa, kumbe tayari wameshawafanyia ukatili pasipo wazi kujijua.

Pia, anasema kuna ulingo mwingine wa utatili kwa wazzi ambao umri wao uko juu, wanapocheza na wadogo huwa wanapigwa au kufanyiwa vitendo vibaya vinavyowaathiri wadogo kisaikolojia, hata wakishakuwa watu wazima.

Mfinanga anasema, kuna baadhi ya walimu wasiokuwa na maadili mema, wanatumia lugha ya ukali au kuwapiga watoto wadogo, kitu kinachowaathiri watoto na kubaki katika akili zao, ikiwajengea wajihi na woga maishani.

Anashauri walimu wanapaswa kuwasaidia watoto, kwani kada hiyo inahitaji kuandaliwa vizuri na kufundishwa bila ya bughudha au kuwapiga, ambayo matokeo yake wanaathiriwa kimaendeleo.

**MADHARA YEPI?**

Ni madhara yepi anayapata mtoto anapofanyiwa ukatili wa aina yeyote? Mkufunzi huyo walimu anataja madhara anayoweza kupata, ni pamoja na kujenga hofu, uwezo wake wa kuelewa kuathirika, akiwa mtu mzima hawezi kujieleza na kujiamini.

"Watu wengi wa namna hiyo maisha huwa yanawashinda kwa kuwa mtoto ni mwanafalsafa ndio maana anakuwa anauliza maswali mengi na magumu, ili aelewe lakini wazazi wengi wamekuwa wanawapuuza," anafafanua

Mfinanga anasema, wanapowapuuza wanasababisha hata wakiwa watu wazima wanakuwa siyo wadadisi na wenye kuthubutu kufanya mambo ya msingi kwa ajili ya maendeleo yao, familia au taifa kwa ujumla.

"Watu wengi wamekuwa mizigo kwa familia na kwa Taifa kwa kuwa walikosa ulinzi wa uhakika na malezi na hivyo ndoto zao kuzimwa kwa kuadhibiwa na kukaripiwa na wazazi au walezi," anasisitiza

Mtaalamu huyo anasema, viongozi wengi wanaoshindwa kuongoza wamelelewa kiimla, kutokana na wazazi wao kuishi maisha ya kikatili, hivyo nao wanayafanya kwa watoto wao ambao baadaye wanakuja kuongoza kidikteta.

"Wapo viongozi wengine hawapokei ushauri na viongozi wengi madikteta wamelelewa kiimla, wanaona mawazo yao ndio sahihi na viongozi wa namna hiyo wanashindwa kulea viongozi wengine kwa kuwa hawatoi fursa ya watu wengine kujifunza," anasema

**NINI KIFANYIKE?**

Mtaalamu huyo anasema, wazazi wengi wanalea watoto wao jinsi walivyolelewa, hivyo wanatakiwa kubadilika kuwa na roho ya upendo, wakiwa na mkakati wa makusudi, ili uingie kwenye nyumba za ibada wazazi wafundishwe.

"Nchi zilizoendelea, wazazi wanapata elimu ya malezi kwa watoto wao na anayeenda kinyume anawajibishwa, maana mtoto akishapendwa, anakuwa na nafasi ya kujieleza kitu ambacho kitamsaidia," anasimulia

Anasema mtoto wa kike ndiye muathirika mkubwa wa ukatili hasa anapofanyiwa ukatili akawa muoga na kuwa na hofu ambavyo vinamfanya hata akiolewa hawezi kuwa na mawazo ya kimaendeleo au mawazo ya kuinuka kiuchumi kwa sababu ya hofu.

Mfinanga anawashauri watunga sera kwamba, suala la malezi liwekwe katika mfumo wa mtaala wa elimu uliopo, ikiwa ndio nyenzo ya unaoweza 'kufinyanga' watu katika malezi.

Kwa mujibu wa Mfinanga, nchi inapaswa kuwa na falsafa au dira inayowekwa kwenye mitaala ya elimu, kwa kuwa kuna vitu vinavyotoa matokeo ya kitaifa.

Mwalimu huyo anafafanua kuwa, Tanzania na Afrika kwa mtazamo mpana ina mambo mazuri, ambayo hata sehemu zingine zinatamani, lakini wako wanajamii wanayapuuza.

Ushauri wake ni kuwapo maadili yatakayosaidia kudhibiti ukatili kwa watoto, jamii inaweza kuwatumia wazee wa kimila wenye ushawishi katika jamii na kinamama maarufu kutoka familia za mfano katika jamii, ili kufundisha malezi.

Mshauri wa Malezi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Davis Gisuka, kutoka Shirika la Children In Crossfire Tanzania lenye makao yake makuu Ireland ya Kaskazini, anasema mtoto anapokosa ulinzi na usalama, anapata udumavu wa ubongo na anaweza kuangukia msongo wa mawazo, maisha yake yanadid-

INAENDELEA UK.19

AFYA

# Unajua kumkaripia, kutomjibu anayouliza unamdhuru mtoto?

INATOKA UK.18



Wazazi wa mjini Babati, wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya (hayupo pichani) katika mkutano. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

imiza uwezo wa kufikiri.

Gisuka anataja athari hizo, ni pamoja na kutomudu lugha anapokuwa mtu mzima, uwezo mdogo wa kujitegemea utakuwa hafifu, kutokana na hofu na woga aliyopandikizwa na wazazi au walezi wake.

**VIONGOZI SERIKALINI**

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya Babati, Getrude Kavishe, anasema kulinda wanafunzi ni jukumu la kila mmoja na wamekuwa wakiwaelekeza wanapowaruhusu kuondoka shuleni, wanawashauri watembee katika makundi, kukwepa waovu.

Kavishe anasema wazazi wengine wanawashuri kwenye mikutano ya shule kuwasindikiza watoto wao wanapoenda shule ili kusaidia kuwavusha sehemu hatarishi na kuwaepusha na watu wasiokuwa wema.

Pia, Kamanda wa Polisi Mkoa Manyara, Paul Kasabago mwishoni mwa mwaka, aliwataka wazazi kuwa waangalifu kwa watoto wao na kuhakikisha wanawasindikiza wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani.

Katika kulidhibiti, hilo aliahidi kufanyika misako ya kihalifu itakayosaidia kuwabaini wabakaji na walawiti na wanaothibitika kufikishwa mahakamani.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alipotakiwa na Nipashe kufafanua hilo, anakiri kuwapo ubakaji na ulawiti kwa watoto wa umri miaka nane na kushuka chini, kwamba vimeongezeka.

Katika hilo anasema, alishamuagiza kamanda wa Polisi Wilaya kufanya msako unaohusiana na matukio hayo, ingawa anakiri kwamba huo si mwarobaini kamili.

Anasisitiza kwamba, mwarobaini kamili ni pale idara ya elimu msingi itapojikita katika kutoa elimu kwa wanafunzi walio hatarini, ili wawe katika nafasi ya kuepuka kadhia hiyo na kukimbia mbinu za waovu .

**WAZAZI**

Mkazi wa Babati, Yusuph Hamisi, anawalaumu wazazi wa sasa hawana muda wa kutosha na watoto wao na ndio inayowasababishia kufanyiwa ukatili, kwa kuwa wanawaachia majukumu zaidi wasaidizi wa kazi, wakiamini wanamudu kuziba pengo hilo.

Hamisi anawataja watoto wa wafanyakazi na wafanyabiashara, ndio walioko kwenye hatari zaidi ya kukosa malezi bora, kwa kuwa hawana muda wa kualea watoto wao, hivyo wanakuwa katika hatari ya madhara ya ukatili.

Kuhusu mamlaka zinazotakiwa kuchukua hatua watoto wanapofanyiwa ukatili anazinyooshea kidole kuwa haziwajibiki inavyotakiwa hasa akilenga kwa wenyeviti wa vijiji na polisi ambao anasema ushahidi unaonekana wazi lakini wamekuwa wakishindwa kuchukua hatua.

> **Utandawazi nao unachangia kwa sehemu kubwa unawaacha watoto hatarini kufanyiwa ukatili, ikiwamo kushuhudia picha chafu kama za utupu kama kwenye televisheni.**

Mkazi mwingine, Asha Juma, anasema utandawazi nao unachangia kwa sehemu kubwa unawaacha watoto hatarini kufanyiwa ukatili, ikiwamo kushuhudia picha chafu kama za utupu kama kwenye televisheni.

Mkazi wa eneo la Dareda, Samson Bayo, anashauri serikali iunde kikosi maalumu cha kupambana na wabakaji na wengine wanaowafanyia ukatili watoto, ili kuweka nidhamu ya jamii, huku akiwasihi viongozi wa dini kuchukua nafasi yao ya kukemea uovu huo.

**RIPOTI UN**

Ripoti ya pamoja iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) na Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka jana, ilieleza namna ilivyo haki kwa ulinzi na ustawi wa jamii kwa watoto.

"Licha ya kwamba ulinzi wa ustawi wa jamii ni haki ya wote, theluthi mbili ya watoto wote Duniani sawa na watoto bilioni 1.3 hawapati ulinzi," inafafanua ripoti hiyo.

Mkurugenzi wa Ulinzi wa Huduma za Ustawi wa Jamii wa ILO, Elizabeth Ortis, anasema ni dhahiri kuna mapengo mengi na muhimu sana kutambua kwamba ni haki ya binadamu kupata ustawi wa jamii kwa watoto wote, akisisitiza kuna uwekezaji mdogo kwa watoto.

Kwa mujibu wa ripoti, watoto wote kuanzia hadi umri wa miaka 14,sawa na asilimia 25 ya watu wote duniani wamewekezewa wastani wa asilimia 1.1 pekee ya pato la dunia.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, akizungumza na wazazi kuhusu maendeleo ya ujenzi wa madarasa ya watoto shuleni.

Elizabeth anaendelea: "Mfano Afrika wanawakilisha asilimia 40 ya watu wote, lakini ni asilimia 0.6 tu ndio uwekezaji uliotengwa kwa ajili ya watoto ya ulinzi wa ustawi wa jamii kwa watoto."

Ripoti hiyo inazitaka mataifa kuangalia upya hatua zake za kukabiliana na changamoto za kiuchumi, zisikandamize haki za watoto ya kulindwa kijamii na kupata ustawi wa elimu, afya, lishe na huduma zingine

Mkuu wa Kitengo cha Umasikini, Watoto na Ulinzi wa Ustawi wa Jamii wa Unicef, David Stewart, anasema umaskini unaowaghubika watoto hivi sasa duniani, ni suala muhimu la kulishughulikia.

"Kuna watoto mil. 385 duniani wanaoishi katika umasikini wa chini ya dola moja (Sh. 2300) na senti 90(Sh. 2070) kwa siku na mara nyingi idadi hiyo wataendelea kuishi katika mazingira ya fedha kidogo ambayo hayawahusu kufikia kilele cha uwezo wao watoto," anasema Stewart

***Mwandishi anapatikana kwa anwani: (+255) 07875***

AFYA

# Corona inavyobadili mazingira ya afya, utafiti, utumiaji dawa



Wateja wa duka la kisasa jijini Dar es Salaam, wakipata huduma huku wamejihami kwa maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

KUZUKA ugonjwa wa homa ya mapafu na vielelezo vingine kama kikohozi, chafya kali na kichwa kuuma au kwa lugha ya haraka corona, ni tukio la aina yake duniani,

Waafrika wakiwa kwenye mshangao, kwingineko matukio aina hiyo yalishatokea, mfano Sars (Severre Acute Respiratory Syndrome) ya mwaka 2012 na homa aina hiyo iliyotokea zaidi Mashariki ya Kati (Middle East Respiratory Syndrome-Mers), wakati huo hadi mwisho wa mwaka jana, ikiambukiza watu 2494 na kuua 858.

Inapolinganishwa na mlipuko wa mkasa wa sasa, covid-19 ina wastani kubwa zaidi ya vifo, ila haienei sehemu nyingi.

Kwa njia hiyo Mers imefanana na ebola, ugonjwa ambao ukiambukizwa, kupona kwake ni taabu zaidi, kuliko virusi vya sasa vya kupumua, licha ya kuwa kuna vianzio vingi vinaanza kufanana katika maeneo tofauti na kwa upande mwingine, utafiti unaouhusu covid-19 unaanzia katika milipuko iliyotangulia.

Kuna jitihada hivi sasa za kuangalia chanjo zilizotengenezwa dhidi ya ebola, zika, sars na mers (licha ya kuwa baadhi hazikukamilika na ugonjwa umeendelea kuua) kama jambo la dharura.

Ikafikia mahali madaktari nchini Marekani wakamwambia Rais wao Donald Trump, kuwa dawa ya hydroxyl-choloroquine, dripu ya choloroquine, inafaa zaidi kwa covid-19.

Baadhi ya wataalamu walipinga, lakini wengine wanakiri inaonyesha matokeo bora na wakati wa jitihada za awali kuzuia kuenea corona, mojawapo ya maeneo yaliyozungumziwa sana ni kuosha mikono na katika mazingira hatarishi kama hospitali unatumia vikinga hewa usoni.

> **Bado kuna suala la kusawazisha mazingira ya kutumia dawa zilizopo au kupatikana dawa mpya, hasa kwa wale ambao covid-19 inawaletea madhara makubwa kwa haraka.**



Abiria wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), akipata huduma ya kunawa mikono, katika stesheni ya Dar es Salaam, kabla ya kupanda treni. **PICHA: TOVUTI TRC**

Katika siku za mwanzo walikuwapo wagonjwa wawili watatu au watano nchini, ilionekana kuwa hatua hiyo ni kinga halisi na kuvaa vikinga hewa ni ya ziada, ambayo hata hivyo haikuanza kuonekana sana barabarani, bali kiasi tu maofisini.

Ugonjwa ulianza kusambaa na sasa kifo cha kwanza kimeshatangazwa, tayari hofu na tahadhari ya kujihami kiafya inachukua nafasi zaidi kwa umma.

Kwa kanuni ya ugonjwa corona,watu wanaokutwa katika chumba kidogo na aliyeambukizwa ugonjwa huo, kama kipindi chake cha kukua mwilini bila udhaifu kuonekana kilikuwa tayari kimesonga mbele, uwezekano wa kuambukiza wengine ni mkubwa.

Dhana ya eneo hatarishi inakuwa tena siyo mtu halisi anayefahamika kuwa ameambukizwa virusi vya corona, ila uwezekano wa kusambaa maambukizi, kwani waliokutana na waathirika wamesambaa.

Ndiyo hapo hofu halisi ya corona inapoanza, pale mtu akianza kushuku usalama wa kupanda basi, kwani unaweza kuketi kando ya mtu aliyekutana na wa karibu au jirani wa mgonjwa mmojawapo na kadhalika.

Kuna wakati, mamlaka za miji zilifanya juhudi kupiga dawa maeneo tofauti hasa majumba marefu na ya makazi, lakini kwa rasilimali tulizonazo haikuwa rahisi kuona .ikirudiwa kila siku, au hata kila wakati.

Njia pekee ambayo hadi sasa imeonekana ngumu ni kutokutoka nje, kwani uwezekano wa kupata mahitaji kwa kutumia simu na kukopeshwa na 'supermarket' kama wanavyofanya kwingineko ni ngumu au haipo kabisa.

Ni tabaka dogo saba la watu wanaoweza kufanya kazi kutoka nyumbani, wakawekewa kompyuta na kila kitu kikaenda sawa; tayari wengine walishaanza kufanya hivyo wiki imepita.

Bado kuna suala la kusawazisha mazingira ya kutumia dawa zilizopo au kupatikana dawa mpya, hasa kwa wale ambao covid-19 inawaletea madhara makubwa kwa haraka.

Hapo, kuna aina mpya ya mazingira ya ugonjwa kuwa katika maambukizi mengi, imepita tu na wale waliopata ugonjwa kupona haraka, kama hawakuwa na mazingira hatarishi ya afya kabla ya hapo.

Ni tofauti na Ukimwi (ugonjwa mwingine wa virusi), ambao unapomkaba mtu, inakuwa rahisi kupata magonjwa ya kudandia kutokana na udhaifu wa mwili. Hii covid-19 haikai mwilini muda mrefu kiasi hicho, kwani isipokuta magonjwa hayo yapo, inatibiwa haraka tu, ila ikiyakuta inakuwa kazi ngumu kutoa hapo na ndiyo maana suala la dawa ya corona inakuwa ni gumu.

Ina maana kuwa katika Ukimwi, kwa mfano kinachoshambuliwa na dawa ni wenyewe, ili magonjwa mengine yasijipenyeze hapo, wakati covid-19 inajipachika katika ugonjwa, kwa kupunguza haraka zaidi kinga za mwili kuliko Ukimwi.

Kiungo muhimu kinachoshambuliwa kama ilivyo katika Sars na Mers ni mapafu, na huku ugonjwa mwingine unajijenga kwako haraka zaidi, ikiwamo kisukari.

Corona inakuwa kama mtihani, ukikutwa una afya njema una uwezekano mkubwa kupona na vinginevyo, balaa liko jirani.

**NAMNA KUJIHAMI**

Eneo moja la utafiti ambalo linaonekana kujenga taswira njema katika kuzuia kujenga athari mbaya mwilini endapo mtu anapata virusi vya covid-19 ni matumizi ya vitamin tofauti, kwa mfano Vitamin C.

Taarifa zinasema, matumizi ya vitamin hiyo yameongezeka kwa wingi nchini Singapore (ni kama sehemu ya Malaysia ila inajitawala), lakini kwa upande mwingine matumizi ya 'multi-vitamin' kwa jumla yanaweza kutoa kinga ya ziada kwa wazee na wagonjwa walio katika hatari ya maambukizi ya covid-19.

Ni kuzuia mwili kudhoofika ghafla, pale virusi hivyo vinapoingia, hivyo dawa za kawaida za kutibu magonjwa nyemelezi - ndiyo hizo dalili za corona kama mafua vile, muamivu makali ya kichwa, homa na kifua kubana.







Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (wa pili kulia), akifuatilia wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi katika mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu juzi, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Kodi wizara ya Ardhi, Denis Masami. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# CST yasisitiza umuhimu elimu jumuishi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA linalohudumia watoto wenye ulemavu la Child Support Tanzania (CST), limesema kuwa mfumo wa elimu jumuishi kati ya watoto wa kawaida na wenye ulemavu, kwa kiasi kikubwa utasaidia kuleta usawa.

Kwa mantiki hiyo, mtoto mwenye ulemavu atapata mahitaji ya ujifunzaji sawa na mwingine jambo ambalo litamfanya ajione sawa na watoto wengine na kusoma kwa furaha.Akizungumza jana na Nipashe, Mkurugenzi wa Shirika hilo, Noela Msuya, alisema wadau na wanaharakati wa kutetea haki za watoto hasa wenye ulemavu wameona ipo haja kwa watoto hao kupelekwa kwenye shule za kawaida kama wenzao ili kushiriki kikamilifu kwenye masomo kama wenzao. Msuya alisema kuwa mfumo wa elimu jumuishi unatoa fursa kwa pamoja ambapo watoto wa kawaida na wenye ulemavu bila kujali tofauti zao kitabaka na kiuwezo, kutasaidia kupunguza vizuizi walivyokuwa wanapata wenye ulemavu na kuongeza rasilimali.

Aidha aliiomba Serikali kuunga mkono jitihada hizo ambapo wamewapeleka watoto wenye ulemavu katika shule nane za Jiji la Mbeya, na watoto hao wameweza kuendana na mazingira bila kujali ulemavu wao. Aliongeza kuwa katika kulipa umuhimu suala hilo, wameamua kuanzisha kauli mbiu isemayo 'Peleka marafiki zangu wote shuleni!' ambapo kupitia kauli hiyo watoto wa kawaida wataweza kutoa hamasa kwa wazazi na jamii kuwapeleka wenzao shule na sio kuwaficha ndani.

"Shirika la Child Support Tanzania limeanza mwaka 2008 nchini na tayari vita dhidi ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia imeanza ni kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa," alisema na kuongeza: "Awali jamii ilikuwa inawabagua watoto wenye ulemavu wengine walikuwa wanafungiwa ndani kutokana na dhana potofu."

Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu Jijini Mbeya, Damas Mwambeje, alipongeza Shirika la CST kwa kuanzisha mfumo wa elimu jumuishi kwani awali watoto wenye ulemavu walikuwa wanapelekwa shule maalum.

Alisema mfumo huo utamsaidia mwenye ulemavu kuchanganyana na wenzake na kufanya vitu kama mtu wa kawaida, na kwamba wako bega kwa bega kuhakikisha suala hilo linafanikiwa kwa kiasi kikubwa. Alifafanua kuwa wameunda timu ya watu 12 ili kuwa na sauti ya pamoja kuhakikisha watoto walemavu wanaenda shule.

# Wanafunzi chuo kilimo wapewa somo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI wa Chuo cha Kilimo cha Mahinya kilichopo wilayani Namtumbo katika Mkoa wa Ruvuma, wamekumbushwa kupeleka utaalamu wao kwa wakulima ili usaidie kuongeza tija ya uzalishaji kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Kituo cha Utafiti wa Kilimo, Tari-Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa akitoa maelekezo ya namna wanafunzi hao wanaweza kutumia ujuzi wao kuwasaidia wakulima.

Dk. Bucheyeki aliwataka wanafunzi hao kuzingatia mafunzo yaliyotolewa na wataalamu wa kituo hicho kwani yatawasaidia kuwa wabobezi kwenye sekta ya kilimo.

"Kituo cha Tari-Uyole ni miongoni mwa vituo vinavyofanya utafiti wenye tija nchini na kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema Dk. Bucheyeki.

Mtafiti wa matunda kutoka kituo hicho, Daud Mbongo, alisema wanafunzi hao walijifunza teknolojia mbalimbali za kilimo ambazo zinabuniwa kituoni hapo.

Alisema miongoni mwa teknolojia hizo ni uzalishaji wa mbegu kwa kutumia muda mfupi, njia rahisi ya upandaji mbegu lakini namna ya kutambua pembejeo bora. Mtaalamu wa zao la mahindi, Julius Sanga, aliwakumbusha wanafunzi hao kwenda kutoa elimu kwa wakulima namna ya kukabiliana na wadudu na magonjwa yanayoshambulia zao la mahidi na tiba yake.

Vilevile, aliwataka wakulima kuzingatia kilimo bora cha zao la mahindi kwa kufuata mtiririko wa kanuni za kilimo bora cha mahindi kutayarisha shamba mapema kwa kutumia zana yoyote iliyo ndani ya uwezo wake, kupanda pindi mvua za mwanzo zinaponyesha na kupanda kwa nafasi ya sentimita 30 kati ya mmea na mmea.

Mwanafunzi wa Chuo cha Mahinya, Esther Nestory, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili wakulima ni uuzwaji wa pembejeo feki, lakini pia kukaidi ushauri wa wataalamu unaowahimiza kutembelea vituo vya tafiti kupata ushauri na kununua mbegu bora.

# Wakulima wapewa mkopo wa mil. 200/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIKUNDI 42 vya wakulima waishio katika vijiji vya Njelenje, Utengule, Mshewe na Mapogoro mkoani Mbeya, vimepewa mkopo wa Sh. milioni 200 kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Kampuni ya Raphael Group, ambayo inajishughulisha na ununuzi wa mazao mbalimbali ya biashara ikiwamo maharage, mpunga, mtama na karanga, Raphael Ndelwa, alisema wanunuzi wameamua kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia mikopo ya kifedha ambayo itasaidia kuzalisha kwa tija.

Ndelwa alisema tangu Kampuni ya Raphael ianzishwe mwaka 1995, inategemea kwa kiasi kikubwa mazao kutoka kwa wakulima, na kwamba walianzisha utaratibu wa kuwasaidia wakulima kifedha ili waendelee kuzalisha zaidi.

Alisema katika utoaji wa mikopo hiyo, kila kikundi kinatakiwa kurejesha mkopo huo kwa kutoa mazao ambayo yanaendana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Aliongeza kuwa ili kuhakikisha mkulima ananufaika na kilimo, walianzisha utaratibu wa kuwatembelea wakulima kwenye maeneo yao ili kutoa ushauri kitaalamu pia kufahamu uzalishaji wao pamoja na changamoto zinazowakabili.

"Tumeamua kumsaidia mkulima kwa kumpatia mkopo wa fedha kulingana na uhitaji wake lakini sharti letu ni rahisi kwani mkulima ataweza kurejesha fedha hizo kwa thamani ya mazao yake, lakini pia lengo letu ni zuri kwani tumeweza kuwatengenezea huduma za kijamii kwa maana ya ukarabati wa zahanati pamoja na huduma za maji," alisema Ndelwa.

Alisema baada ya kufanya ziara ya kuwatembelea wakulima waligundua kuwa ipo haja ya kuwatengenezea maghala ya kuhifadhia mazao yao katika maeneo wanayoishi ambapo maghala 22 yanatarajiwa kukamilika.

Alisema lengo la kutengeneza maghala hayo kwa wakulima ni kurahisisha uuzwaji wa mazao kwani kampuni itakuwa inanunulia mazao kwenye vijiji ambayo tayari vimeshajengewa maghala.

Alisema kuwa uwapo wa maghala hayo utapunguza changamoto ya usafiri kwa wakulima ambao walikuwa wanapata adha kipindi cha masika kutokana na barabara zao kuharibiwa na mvua.

Miongoni mwa wakulima walionufaika na mikopo hiyo akiwamo Jackson Mwaipaja, alisema kampuni hiyo imewasaidia kumudu gharama za kuendesha shughuli za kilimo na kuwafanya wazalishe kwa tija na kupata uhakika wa soko.

Mwaipaja alisema mikopo wanayopewa na kampuni hiyo ni nafuu na haina masharti magumu kwa sababu mazao wanayovuna ndio hutumika kurejesha mikopo.

"Kampuni hii imekuwa mkombozi kwetu kwa sababu inatusaidia wakulima kutengeneza mnyororo wa thamani kwa kuhakikisha kuanzia mkulima mdogo hadi mkubwa ananufaika na kilimo chake," alisema Mwaipaja.

Rachel Saimon, aliishauri kampuni hiyo kuanzisha mpango wa kuwatengenezea wakulima mnyororo wa thamani ili kupata soko la uhakika kutokana na mazao wanayozalisha sambamba na kukopesheka kwenye taasisi za kifedha.



HABARI DODOMA

# Mchakato kupunguza msongamano wafungwa magerezani waanza rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Taifa ya Huduma kwa Jamii imezinduliwa, huku ikipewa jukumu la kushughulikia msongamano wa wafungwa magerezani ikiwamo wenye vifungo vidogo kutumikia adhabu hizo nje.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, katika uzinduzi wa kamati hiyo.

Alisema tatizo la msongamano wa wafungwa magerezani limekuwa ni sugu hivyo Kamati hiyo ina wajibu wa kuhakikisha inatatua.

Alieleza kuwa kamati hiyo inawajibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria ya huduma kwa jamii ambayo inatoa fursa kwa wafungwa waliohukumiwa vifungo vidogo kutumikia adhabu hizo kwenye jamii.

"Magereza ni yale yale hayapanuliwi wakati watu wakiendelea kufungwa, kuna haja ya kuangaliwa upya mfumo wa adhabu kwani wafungwa wengi wamekuwa wakifungwa gerezani wakati kuna njia nyingine za adhabu," alisema.

Simbachawene alisema wale wanaotenda makosa ambayo sio makubwa hakuna haja ya kufungwa gerezani, wanatakiwa kufungwa vifungo vya nje ili kupunguza msongamano.

Waziri huyo alisema mfumo wa adhabu umejikita kufunga tu gerezani.

"Tunaamini adhabu ni kumfunga tu mtu wakati adhabu zingine zipo hili nawaomba sana mliangalie, sio kila mtu ni lazima afungwe ndani ya gereza lakini msisahau kuishirikisha jamii kwenye hizo adhabu ili wazikubali," alisema Simbachawene.

Aliitaka Kamati hiyo kusimamia vyema sheria ya kutokumuonea mtu.

Waziri Simbachawene aliahidi kutoa ushirikiano kwa kamati hiyo muda wowote ambapo watamhitaji huku akiwasihi kumshauri vizuri kwenye utekelezaji wa sheria.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Christopher Kadio, alisema kuanzishwa kwa Kamati hiyo kutakuwa ni chachu ya kuzidi kutenda kazi na itafungua ukurasa mpya wa kufanya kazi kwa weledi.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jaji Zephine Ngaleba, aliimuomba Waziri awasaidie ili Kamati hiyo iwe na nguvu katika utendaji kazi wake ili kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani.

Jaji Ngaleba alisema watajitahidi kutumia maarifa yao yote kuhakikisha wanapunguza msongamano wa wafungwa na mahabusi magerezani.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha Vodacom Tanzania, Jackline Materu (kulia), akiwapa maelezo baadhi ya wananchi kuhusu kazi anazofanya roboti ajulikanaye kwa jina la Pepper, walipotembelea duka la kampuni hiyo, jijini Dodoma juzi. Roboti hilo, limebuniwa ili kufanyakazi ya kuwahudumia wateja wanapofika kwenye maduka ya kampuni hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wataalamu wa Ulaya kuja kutafiti ujenzi miundombinu

**Renatha Msungu,** DODOMA

WATAALAMU kutoka nchi mbalimbali za Ulaya, wamewasili jijini hapa kwa ajili ya kufanya utafiti wa ujenzi wa miundombinu ya kisasa inayotarajia kuanza kujengwa hivi karibuni.

Aidha mradi wa ujenzi wa miundombinu hiyo utafanyika kwa msaada kutoka Benki ya Dunia , ambapo inatarajia kutoa fedha kulingana na gharama watakayopata watalaamu hao baada ya utafiti huo.

Akizungumza jana jijini hapa, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema anamshukuru Rais John Magufuli kwa kuwaleta watalaamu hao ambao watapata taswira ya ujenzi wa Jiji hilo.

"Kama unavyojua Dodoma sasa ni makao makuu ya nchi, hivyo huu mji unatakiwa kujengwa kwa weredi wa hali ya juu, ndio maana Rais wetu katuletea watalaamu watakaofanya survey kwanza ndipo ujenzi huo uanze", alisema Katambi.

Mkuu huyo wa wilaya alisema watalaamu hao wataanza kuangalia mifumo ya majisafi na maji taka, vyanzo vya maji pamoja na miundombinu ya barabara ukiwamo uchimbaji wa mitaro ili hata mvua kubwa zikinyesha zisilete madhara.

Aidha, Katambi alisema, watalaamu hao pia wataangalia ramani ya Jiji zima la Dodoma na kuangalia mpango wa miundombinu ya reli ya kisasa (SGR), uwanja wa ndege pamoja na ujenzi wa magorofa ambavyo vyote kwa pamoja vinatarajiwa kujengwa hapo baadae.

"Huwezi kuomba mkopo Benki ya Dunia bila kujua gharama itakayotumika kujenga miundombinu hiyo, hivyo watalaamu haohao baada ya kazi ya utafiti watapata gharama halisi ya ujenzi huo, itakayosaidia kujua ni fedha kiasi gani itahitajika kuujenga mji wa Dodoma," alisema Katambi.

Aidha, Katambi alisema watalaamu hao wanatoka Hispania, Marekani na Uholanzi.

Kutokana na mvua kubwa zinazonyesha jijini hapa, baadhi ya miundombinu ya barabara kuharibika pamoja na baadhi ya makazi ya watu kubomoka.

Alisema hali hiyo inasababishwa na kutokuwapo kwa mitaro na miundombinu ya majitaka na majisafi kutokuwa vizuri hivyo Serikali iliamua kuweka mpango mpya wa ujenzi huo jijini hapa.

Mpango mpya wa ujenzi wa Jiji la Dodoma, utahusisha pia nyumba za wananchi ambao watatakiwa kujenga kwa mtindo unaofanana kutokana na eneo husika kwa kufuata utaratibu wa Jiji.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alishatoa angalizo nyumba yoyote itakayojengwa bila kufuata taratibu za Jiji itabomolewa, kwani itaharibu mipango mji uliowekwa na Serikali.

# Mch. ataka adhabu wakaidi wa corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MCHUNGAJI Vincent Malenda wa Kanisa la Calvary Assemblies of God Mokedonia Mission Centre ,Kisasa Relini jijini Dodoma, ameiomba serikali kutoa adhabu kali kwa wale wanaokwamisha jitihada za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Hatua hiyo ya Mchungaji Malenda ya kuiomba serikali kuwaadhibu wakaidi hao, imetokana na baadhi ya watu kudharau maelekezo yanayotolewa na viongozi juu ya kuchukua tahadhari kwa lengo la kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo.

Mchungaji Malenda alisema hayo alipokuwa akihubiri kwenye ibada iliyofanyika kanisani hapo kwa ajili ya kuombea Taifa ili kuondokana na ugonjwa huo hatari unaoendelea kutishia maisha ya watu duniani.

Alisema kuwa kuna baadhi ya watu wameuchukulia ugonjwa huo kama mzaha, badala ya kushirikiana na serikali katika kutoa elimu, wao wameamua kuisaidia corona kuenea zaidi.

"Hivyo ni wakati sasa kwa serikali kuchukua uamuzi mgumu kwa watu kama hao, ambao wamekuwa wakirudisha nyuma harakati za kuuondoa kutokana na tabia yao ya kudharau," alisema.

Aidha, alisema ugonjwa huo haujali mtu mwenye cheo, dini, kabila rangi au kiongozi, hivyo mtu yeyote anaweza akapatwa na maambukizi.

Alisema kutokana na hali hiyo, ni vyema kwa serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria watakaobainika kukaidi maelekezo yake.

Katika hatua nyingine, kanisa hilo limeipongeza serikali kwa jinsi inavyosisitiza juu ya kujihadhari na ugonjwa huo kwa watu wake bila kujali itikadi yoyote ya kisiasa au ya kidini.

Mchungaji huyo alisema kuwa Kanisa hilo litaendelea kutoa elimu kwa wengine ikiwa ni hatua yake ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali ili ugonjwa huo usilete madhara kwa Watanzania.





# Polisi sasa kukomesha biashara dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi limesema limejipanga kuhakikisha kwamba biashara ya madawa ya kulevya inatokomezwa nchini na kuwaonya wapiganaji wa Jeshi hilo wasijishughulishe na kuhusishwa kwao.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, wakati akifungua kituo cha polisi Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema biashara ya madawa ya kulevya haikubaliki nchini na Jeshi la Polisi limejipanga kutokomezwa na wahusika wake kukamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

"Jeshi la Polisi tumejipanga kuona kwamba biashara ya madawa ya kulevya haina nafasi tena nchini...lakini pia tunawataka askari wetu wasijishungulishe na biashara hiyo na watakaobainika wajue kwamba watafukuzwa kazi," alisema.

Aliwataka watalii katika ukanda wa kaskazini Unguja wasijishughulishe na biashara ya madawa ya kulevya kwa kuwa watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Vuai Mwinyi, amelipongeza Jeshi la Polisi kwa kuweka kituo cha polisi katika Jimbo la Nungwi lenye idadi kubwa ya hoteli za kitalii.

Alisema uwapo wa kituo hicho utasaidia kudhibiti na kupunguza matukio ya uhalifu kwa watalii pamoja na hoteli zake.

"Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja tumefurahishwa sana na ujenzi wa kituo hichi ambacho matarajio yetu makubwa kitasaidia kupunguza uhalifu kwa sekta ya utalii," alisema.

Kwa upande wake Kamishna wa Jeshi la Polisi ushirikishwaji wa jamii, Mussa Ali Mussa, aliwataka wananchi kukitumia kituo hicho kwaajili ya kutoa taarifa za matukio ya kihalifu.

"Lengo la ujenzi wa kituo hichi ni kuzipatia ufumbuzi changamoto za wananchi zinazohusu matukio ya uhalifu wa aina mbalimbali na kuona zinapatiwa ufumbuzi wa kudumu," alisema.

Ujenzi wa kituo hicho umegharimu Sh. milioni 64 na unatokana na kilio cha muda mrefu cha wananchi na wawekezaji kutaka kuwapo kwa kituo hicho kitakachosaidia kupambana na matukio ya uhalifu ikiwamo wizi katika hoteli za kitalii.

# Mfanyabiashara asaidia vifaa kujikinga corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imepokea msaada wa vifaa vya afya kutoka kwa mfanyabiashara, Said Nassir Bopar, kwa ajili ya kupambana na kujikinga na maambukizi ya corona.

Akipokea msaada huo, Waziri wa Afya Hamad Rashid Mohamed, alisema vifaa hivyo vitasaidia kutoa huduma za matibabu pamoja na kupambana na ugonjwa wa corona nchini.

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na vitanda 36, mashuka, vitakasa mikono, jokofu la kuhifadhia damu, maski, mito na kiti cha kubebea wagojwa.

Hamad alisema serikali inahitaji vifaa vingi kutokana na kuwapo kwa wagonjwa ambao wanahitaji kupatiwa matibabu na wananchi kujikinga maambukizi ili yasienee nchini.

"Mdau huyu wa maendeleo ameleta vifaa hivi wakati mzuri kwa kuangalia shida iliyopo hivi sasa kutokana na kufunguliwa kituo kipya cha Kidimni ambacho kinahitaji vifaa mbalimbali kwa wagonjwa waliopata maambukizi ya corona," alisema Waziri Hamad.

Pia, alimshukuru mfanyabiashara huyo kwa msaada huo ambao utasaidia kutoa huduma kwa wagonjwa na kupunguza maambukizi na kupiga vita ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, waziri huyo aliwataka wananchi kuchukua tahadhari mapema kwa kuepuka mikusanyiko na kufuata maagizo yanayotolewa na serikali ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Wananchi wasikae vikundi wabakie majumbani mwao na kuwadhibiti watoto wao, kufanya hivyo kutasaidia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona nchini," alitahadharisha waziri. Hamad aliitaka jamii kuchukua tahadhari ya kukaa umbali wa mita moja na kufuata maadili na masharti ya wataalamu wa afya.

Aliwataka wananchi wenye wagonjwa katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kupanga utaratibu wa kuwahudumia wagonjwa wao kuingia watu wawili pekee ili kuepusha msongamano ambao utahatarisha maisha yao.

Naye Mfanyabiashara huyo, Said Nassir Bopar, alisema ametoa msaada huo kwa lengo la kuokoa maisha ya wananchi kutokana na hali halisi iliyopo ya mlipuko wa maradhi ya corona pamoja na kujikinga maambukizo hayo.

Alisema kuwa ataendelea kuisaidia serikali kila hali inaporuhusu ili kutoa huduma bora kwa wananchi pia anatarajia kutoa msaada mwengine katika Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A pamoja na Kisiwani Pemba.

"Kila panapotokea tatizo kupenda kuisaidia jamii ili kuepukana na athari," alisema Bopar.



Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed (kulia), akipokea msaada wa vifaa na dawa mbalimbali kutoka kwa mfanyabiashara maarufu Zanzibar, Said Nassir Bopar, kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, katika hafla iliyofanyika

# Serikali kuwaunga mkono vijana maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Lulu Msham Abdallah, amesema serikali itaendelea kuwaunga mkono vijana katika shughuli za maendeleo.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa mbalimbali kwa vikundi vinane vya mikoa yote ya Unguja, alisema serikali inachukua jitihada kuhakikisha vijana wanajikwamua kiuchumi.

Aliwataka kuendelea kuthamini jitihada za serikali katika kuwakomboa na dimbwi la umasikini. Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana, Mwanaidi Mohammed Ali, alisema msaada huo ni miongoni mwa utekelezaji ahadi alizozitoa Naibu wa wizara hiyo katika ziara yake aliyoifanya hivi karibuni katika vikundi vya vijana.

Aliwaomba kuvitumia vifaa hivyo kwa madhumuni yaliyokusudiwa ili lengo liweze kufikiwa.

Akipokea msaada huo, Fahami Ramadhan Wakili, kutoka kikundi cha kwa Mtumwajeni, alipongeza serikali kwa kutimiza ahadi yake ya kuwaunga mkono vijana.

Aliwaomba viongozi wengine kuiga mfano wa Naibu Waziri huyo katika kuwasaidia vijana kujikomboa kiuchumi.

HABARI KITAIFA

# Walia matengenezo barabara Vingunguti

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI na watumiaji wa barabara inayopita eneo la viwandani Vingunguti jijini Dar es Salaam, wameiomba Serikali kuitengeneza kutokana na kupitika kwa shida.

Barabara hiyo inayoanzia relini hadi katika Shule ya Sekondari Majani ya Chai, imekuwa chanzo cha kudorora kwa shughuli za kiuchumi, kutokana na kuharibu magari ya wenye viwanda na watu binafsi.

Baadhi ya madereva wa malori wanaotumia barabara hiyo, walisema magari yamekuwa yakiharibika mara kwa mara na kuwasababishia hasara kubwa ya kununua vipuri.

"Magari mengi yananasa, kupita inakuwa taabu hasa kwa gari ndogo. Na kero hii ilianza tangu ulipokuja ujenzi wa Reli ya Kisasa ghafla maji yakaanza kujaa hapa," alisema mmoja wa madereva hao, Mohamed Salum.

Dereva mwingine, Seleman Mrisho, alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo, wamekuwa wakipeleka magari kwenye matengenezo kila wiki.

"Taabu ni kubwa mno kiasi kwamba 'spring' zinakatika. Sisi wenye malori unaweza kupita hapo taa zisionekane sasa gari dogo si ndio linazama kabisa," alisema Mrisho.

Mmoja wa wakazi wa Vingunguti, Neema Hudson, alisema watu wenye magari madogo wanalazimika kuzunguka nyuma na Zahanati ya Vingunguti na kutokea uwanjani kukwepa kero hiyo.

"Serikali ilione hili na kutusaidia jamani, kero hii ni ya muda mrefu na inatusababishia usumbufu na hasara. Mimi gari langu hii (IST) iliwahi kunasa, maji yalijaa hadi ndani kama ingekuwa usiku sasa hivi tungekuwa tunaongea mengine," alisema Neema.

Alipoulizwa Meya wa Manispaa ya Ilala ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Vingunguti, Omary Kumbilamoto (CCM), alisema Serikali inafahamu kuhusu kero ya barabara hiyo na inajipanga kuitengeneza.

Alisema katika bajeti ya 2020/21 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) umetengewa Sh. bilioni 5.2 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja katika sehemu mbalimbali za manispaa hiyo.

"Si wao tu hata mimi mwenyewe gari langu naona kabisa linavyoumia, baada ya sisi kuliona hilo tumepitisha kwenye bajeti itakayoanza kutekelezwa mwaka mpya wa fedha (Julai).

"Barabara zote zipo Tarura, lakini ukiongea nao watakuambia fedha hawana, manispaa haina hata bajeti ya vifusi, lakini kama mamlaka za kutengeneza barabara zingeachwa manispaa wala hizi kero usingezisikia," alisema Kumbilamoto.

# Taboa: Wapigadebe wapunguzwe vituoni

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wamiliki wa mabasi Tanzania (Taboa), kimetaka kupunguzwa idadi ya wapigadebe kwenye vituo vya mabasi ikiwamo cha Ubungo kwa mwezi mmoja, ili kukabiliana na corona.

Pia, wameanza kupuliza dawa kwenye mabasi yote nchini ili kuhakikisha virusi hivyo havisambai huku wakiwataka wenye daladala kupeleka magari yao kwaajili ya kupulizwa.

Akizungumza na Nipashe, Katibu wa Taboa, Enea Mrutu, alisema bila kupunguza msongamano hali itazidi kuwa mbaya na huenda kukawa na hatari zaidi na kwamba ni vyema wakasimamisha watu kuingia kwa mwezi mmoja ili kuangalia hali itakavyokuwa.

Alisema kwa sasa biashara ni mbaya kutokana na kutokuwa na wasafiri, huku akieleza kuegesha magari yake mawili yanayofanya safari za Dar es Salaam na Arusha. "Tusilete siasa kwenye suala hili kuwa wakipakia abiria kulingana na idadi ya viti hawatapata faida, hili ni janga lisichukuliwe kwa urahisi," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (wa pili kulia), akizindua elimu itakayotolewa kwa wananchi wote wa mkoa huo dhidi ya maambukizi na uenezi wa virusi vya corona inayoendeshwa na Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross), jijini humo, jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Waipongeza serikali kupelekewa maji

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAKAZI wa Kijiji cha Napata wilayani Masasi mkoani Mtwara, wameipongeza serikali kwa kuanza jitihaza za kuwapelekea huduma ya majisafi na salama.

Kijiji hicho tangu nchi ilivyopata uhuru mwaka 1961 haijawahi kuwa na huduma ya maji na wananchi wake wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Wakizungumza na Nipashe, walisema kuwa wameshaanza kujitolea kwa kuchimba mitaro kwa ajili ya kulaza mabomba yatakayotumika kupitisha maji kutoka kwenye chanzo cha Mbwinji.

Venance Petro, alisema katika kijiji hicho kumekuwapo changamoto ya huduma za maji tangu Uhuru.

Alisema kutokana na tatizo hilo, wananchi wanalazimika kutembea umbali mrefu kufuata maji kwenye mito mbalimbali ambayo maji yake sio safi wala salama kwa ajili ya matumizi yao kutokana na kutumiwa na wanyama.

"Wake zetu wanalazimika kuamka usiku wa manane kila siku wakati wengine hulala huko huko visimani kusubiri maji, hivyo kuhatarisha ndoa zetu," alisema Petro.

Naye Zainabu Issa alisema waathirika wakubwa wa tatizo la maji ni wanawake na watoto, kutokana na kinamama kuwa na jukumu kubwa la kutunza familia katika kuhakikisha familia.

Alisema tatizo la maji linawatesa wanawake wa kijiji hicho kwani wao huamka usiku wa manane kisha kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo, huku wakiwa na watoto migongoni, hivyo wanaipongeza serikali kwa kuliona hilo na kuamua kuwapelekea maji.

Asha Salumu, alisema hatua ya serikali kupeleka maji katika kijiji chao na vingine vya jirani ni jambo ambalo linapaswa kuungwa mkono, kwa wananchi wa vijiji hivyo kujitolea kuisaidia serikali kufanikisha jambo hilo.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi wa maji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Masasi-Nachingwea (MANAWASA), John Alex, alisema mradi huo unalenga vijiji sita na utakuwa na vitofu vya kutolea maji 12.

Alisema mradi huo una kilomita 36 na utatumia mabomba yenye kipenyo cha nchi sita mpaka nchi moja na nusu, na kwamba wanufaika wakubwa ni vijiji vya Lukuledi, Nasindi, Mkolopola 'A', Mkolopola 'B', Napata na Kalinga.

"Mradi huu tulianza kwa kupitia nguvu za wananchi wenyewe kwa kuchimba mitaro na mradi huu unatarajia kukamilika mwezi huu, na kwamba maji haya tunayota katika mradi wa maji ya Mbwinji na kupeleka hadi kijiji cha Lukuledi," alisema Alex .

Alisema utekelezaji huo hadi sasa umefikia zaidi ya asilimia 75, na kwamba Mamlaka hiyo inawapongeza wananchi wa vijiji hivyo kwa kuwa na moyo wa kujitolea katika kutekeleza mradi huo.

HABARI KIMATAIFA

## Taharuki yatanda wagonjwa wapya wa corona

**BUJUMBURA,** Burundi

WANANCHI wa Burundi hususani wakazi wa mji mkuu wa kiuchumi wa Bujumbura wameingiwa na wasiwasi baada ya serikali ya nchi hiyo kutangaza kwa mara ya kwanza visa viwili vya maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona nchini humo.

Serikali kupitia waziri wake wa Afya, Thadee Ndikumana, alitangaza kwamba wagonjwa wote wawili ni raia wa Burundi ambao mmoja alitokea Rwanda na mwingine akitokea Dubai. Waziri Ndikumana alibaini kwamba kazi ya kuwatafuta watu waliokaribiana na wagonjwa hao imeanza.

Tangazo hilo la serikali linakuja wiki moja baada ya mashirika mbalimbali ya kigeni yanayofanya kazi nchini humo pamoja na shule linalomilikiwa na serikali ya Ufaransa "Ecole Francaise" kuwataka wafanyakazi wao kubaki nyumbani.

Hata hivyo katikati ya wiki iliyopita, serikali ya Burundi iliyaonya mashirika hayo kuchukuwa hatua kama hiyo wakati haijathibitika kisa chochote cha maambukizi nchini.

Wakati huo huo, serikali ya Burundi imewataka raia wake kuzingatia kanuni za usafi na kuepuka kukaribiana bila kuwa na vifaa vya kujilinda kama vile barakoa na maski nyingine. **RFI**

## Trump awatahadharisha Wamarekani virusi vya corona

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amewataka Wamarekani kujitayarisha kupokea taarifa za hali mbaya zaidi ya athari za maambukizi ya virusi vya corona mnamo wiki mbili zijazo.

Wataalamu nchini humo wamesema huenda watu takribani 100,000 wakafariki kabla ya janga la ugonjwa huo kumalizika. Meya wa Jiji la New York, Bill de Blasio aliomba utawala wa Rais Trump kupeleka msaada wa dharura katika mji huo mkuu wa biashara.

Zaidi ya watu 3,700 wamefariki nchini Marekani tangu kulipuka kwa ugonjwa huo ikiwa ni idadi kubwa zaidi ya waliofariki China ambako janga hili lilianza.

Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO) hadi kufikia juzi jioni, zaidi ya watu 800,000 waliambukizwa kote duniani na zaidi ya 40,000 wamefariki kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona.

Mkurugenzi wa kanda ya Pacific ya Magharibi ya WHO, Takeshi Kasai, akizungumza na waandishi habari kupitia mtandao siku ya Jumanne, alisema ingawa kuna mafanikio yanayopatikana nchini China na Korea Kusini, lakini janga linaendelea kwa haraka katika mataifa mengine na hivyo kuzitaka serikali za dunia kuimarisha juhudi za kupunguza kasi za mambukizi. **VOA**

# Mch. aliyepotosha kuhusu corona apelekwa rumande

**KAMPALA,** Uganda

MAHAKAMA nchini Uganda imempeleka rumande mchungaji aliyetoa matamshi ya kupotosha kwamba hakuna virusi vya corona Afrika, matamshi yanayodhoofisha juhudi za kupambana na kusambaa kwa virusi hivyo.

Mchungaji huyo ni miongoni mwa viongozi wa kidini zaidi ya 20 waliokamatwa mwishoni mwa wiki kwa kukiuka maagizo yanayolenga kukabiliana na janga la virusi vya corona.

Ingawa viongozi wa kidini nchini Uganda waliazimia kuisaidia serikali katika kuhakikisha kuwa maagizo yanayolenga kuepusha kuenea kwa ugonjwa huo yanatekelezwa kuna baadhi ya wachungaji kama vile Augustine Yiga ambao wanapotosha umma kwa kukanusha madhara ya ugonjwa huo.

**Miongoni mwa waliokwepa karantini ya siku 14 ni wanasiasa wakiwamo mawaziri sita na jamaa zao waliotokea ng'ambo.**

Mchungaji huyo ameshutumiwa vikali kwa kuhatarisha maisha ya watu na kukwaza juhudi za serikali za kuhamasisha kila mtu ashiriki katika kukabiliana na janga hilo.

Viongozi wengine 25 walikamatwa mwishoni mwa wiki kwa kukiuka maagizo ya kuepusha mikusanyiko.

Jeshi la Polisi ambalo mwanzoni ilitumia nguvu kukabiliana na wale waliokiuka maagizo inafanya juhudi kuhamasisha watu. Kulingana na msemaji wa Jeshi la Polisi eneo la Kampala, Patrick Onyango, kila mtu ambaye anapotosha umma kuhusu suala ya mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona atachukuliwa hatua.

Vyombo vya usalama vimeunda jopokazi la pamoja kushirikiana na wafanyakazi wa afya katika kuwafuatilia washukiwa wa ugonjwa huo waliotoroka kutoka karantini.

Miongoni mwa waliokwepa karantini ya siku 14 ni wanasiasa wakiwamo mawaziri sita na jamaa zao waliotokea ng'ambo.

Kundi hilo limeelezewa kuwa tishio kubwa kwa umma huku Rais Yoweri Museveni akiwazuia mawaziri hao kutoshiriki vikao vya baraza la mawaziri. **DW**



Daktari Denis Protsenko (kushoto), ambaye amekutwa na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, akiwa na Rais wa Urusi, Putin, walipokutana wiki iliyopita. **PICHA: ALLIANCE**

# 172 wafariki Afrika, 5413 waambukizwa

KITUO cha udhibiti na kuzuia magonjwa cha Umoja wa Afrika kimesema kuwa watu 172 wamepoteza maisha baada ya kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa corona barani Afrika.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa ugonjwa huo umeenea katika nchi 50 barani. Kwa ujumla, watu 5,413 wameambukizwa.

Ilieleza kuwa hadi jana hakuna taarifa zozote za maambukizi katika nchi za Lesotho, Sudani Kusini, visiwa Sao Tome, Principe, Comoro na Malawi.

Hapo jana eneo lililojitangazia uhuru wake Somaliland lilithibitisha kuwapo na maambukizi ya watu wawili. Redio Kulmiye ilitangaza kuwa mmoja kati ya walioambukizwa ni raia wa China aliyekuwa akiishi katika mji wa Berbera. Mwingine ni raia wa Somalia ambaye hivi karibuni alirejea kutoka nchini Uingereza.

Nchi ya Somalia imesambaza vikosi vyake mitaani na kupiga marufuku utafunaji wa mirungi mitaani kuepuka kusambaa kwa virusi.

Afrika Kusini ndiyo nchi inayoongoza kuwa na idadi kubwa ya maambukizi ikiwa imefikisha 1,353, watu saba wakiwa wamepoteza maisha.

Watu 11 wamethibitishwa kuambukizwa virusi vya corona tangu jana nchini Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo (DRC) na kufanya idadi ya walioambukizwa kufikia 109 na vifo nane.

Wangojwa watatu hadi sasa wameripotiwa kupona lakini mgojwa wa kwanza hadi sasa bado yupo hospitalini na serikali haijamruhusu kurejea nyumbani kwake.

Mashirika ya kiraia yamelaani serikali kupuuza kufuatilia kwa karibu utelekezaji wa maagizo ya kuepusha kuenea kwa virusi nchini humo.

Wiki iliyopita serikali ilitangaza kusitisha hatua yake ya kuzuia raia wa kinshasa kutoka nyumbani.

Miongoni mwa maagizo yaliyotolewa na Rais Felix Tshisekedi ni pamoja na kuomba viongozi wa mitaa kuweka maji na sabuni barabarani, lakini hadi sasa vifaa hivyo vya kiafya bado havijasambazwa katika mitaa ya Kinshasa. **BBC**

## Daktari aliyekutana na Rais Putin akutwa na corona

**MOSCOW,** Urusi

DAKTARI aliyekutana na Rais wa Urusi, Vladimir Putin, wiki iliyopita, alipokuwa akizuru hospitali moja huko Moscow, amepatikana na virusi vya Corona baada ya kufanyiwa vipimo, Televisheni ya serikali, Rossiya 24, imeripoti jana.

Putin alizuru hospitali ya Kommunarka wiki iliyopita na kwamba alikutana na daktari mkuu wa hospitali hiyo, Denis Protsenko.

Wote wawili hawakuwa wamevaa vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona wakati wa mazungumzo yao.

Hadi kufikia jana janga la ugonjwa wa virusi vya corona ambalo lilianzia nchini China Desemba mwaka jana kabla ya kuenea duniani kote, limesababisha vifo vya watu 17 nchini humo na watu 2,337 wameambukizwa virusi vya ugonjwa huo, kulingana na ripoti rasmi iliyotolewa na mamlaka nchini Urusi. **RFI**

# Kiwanda chaiomba serikali malighafi vitakasa mikono

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SERIKALI imeombwa kusaidia upatikanaji wa malighafi ya kutengenezea vitakasa mikono ambavyo vinatumika kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona kwa Kampuni zinazozalisha kwasasa.

Ombi hilo limetolewa juzi mjini hapa na Mkurugenzi wa Kiwanda cha Creative Inter Traders, kilichopo Kibaha mkoani Pwani, Prosper Chila, wakati akiongea na waandishi wa habari.

Chila alisema, kwasasa malighafi ya kutengeneza vitakasa mikono inapatikana nje ya nchi na gharama yake ni kubwa kutokana na uhitaji.

"Kiwanda chetu kilikuwa kinatengeneza mafuta ya care na losheni mbalimbali ila kutokana na kuingia huu ugonjwa wa corona tumelazimika kuanza kutengeneza vitakasa mikono wananchi wengi wapate kwa urahisi," alisema Chila.

Alisema, tangu ameanza kutengeneza vitakasa mikono soko lake limekuwa kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi, na kutokana na uhitaji kuwa mkubwa anauza kwa rejareja ili wananchi wapate bila usumbufu.

"Gharama ya kuagiza malighafi nje ni kubwa, lakini nimeangalia na hili janga tulilonalo gharama za hivi vitakasa mikono haiwezi kuwa kubwa na rafiki ili kila mmoja kulingana na uwezo wake amudu kununua," alisema.

Alisema, kwasasa kiwanda hicho kinazalisha tani nane hadi 10 ambazo zinasambazwa mikoa mbalimbali, na pamoja na kupokea oda kutoka nje ya nchi, kwasasa hawezi kuuza huko hadi atakapojiridhisha kuwa hakuna upungufu katika soko la ndani.

Alisema, ametengeneza mazingira ya kujikinga na virusi hivyo kwa wafanyakazi wake kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya.

Ally Abdul, mfanyakazi katika kiwanda hicho alisema, wanapatiwa elimu mara kwa mara kukumbushia kuzingatia maelekezo yanayotolewa kujikinga na corona na kwa upande wao kila mmoja amepatiwa kitakasa mikono na anatembea nayo kujipaka kama kinga anaporejea nyumbani.

Mmoja wa wakazi wa Kibaha, Asma Mohamed alisema, awali walikuwa wakiuziwa bidhaa hiyo kwa gharama kubwa, sasa wameanza kuipata kwa urahisi karibu na kiwanda hicho kwa gharama nafuu.

Naye Athumani Mokiwa, aliwataka wananchi kuzingatia ushauri unaotolewa na serikali kujikinga na corona ili kuepuka kuambukizana na vifo ambavyo vinaweza kusababishwa na ugonjwa huo.



Vijana wakisaidia kushukuma gari lililokwama kwenye ndimbwi la maji yaliyosababishwa na ubovu wa miundombinu ya barabara inayopita ukanda wa viwandani eneo la Vingunguti, Dar es Salaam jana. Habari Uk. 24. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kituo cha afya chasimamishwa huduma

**Na Ambrose Wantaigwa,** MUSOMA

KUTOKANA na mvua inayoendelea kunyesha katika Mkoa wa Mara, huduma muhimu katika kituo cha afya Iringo, Manispaa ya Musoma zimesitishwa kwa muda usiojulikana.

Nusu ya majengo ya kituo hicho ikiwamo wodi ya kinamama na watoto yamefunikwa na maji kutokana na kujaa kwa Ziwa Victoria na kusababisha kingo zake kuvuja kuelekea katika kituo hicho.

Kamati ya usalama ya Wilaya ya Musoma iliyofanya ziara katika kituo hicho juzi, iliagiza kuhamishwa huduma hizo haraka iwezekanavyo kuelekea katika zahanati ya polisi na kituo cha afya cha Nyasho vilivyo karibu.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Naano, aliamuru kuchukuliwa hatua hiyo ili kuwezesha wananchi wa maeneo hayo hususan kinamama kupata huduma ya afya katika kipindi ambacho taifa linakabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

"Katika kipindi hiki ambacho nchi nzima inaendesha hamasa kwa wananchi kuhusu namna bora ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona serikali wilayani hapa itahakikisha wakazi wa maeneo haya wanaendelea kupata huduma za afya bila vizuizi," alisema.

Kituo hicho cha afya pia kinahudumia mamia ya wananchi wanaojishughulisha na biashara ya uvuvi katika mwalo wa Mwigobero pembezoni mwa Ziwa Victoria kikiwa pia kituo cha kupokea na kuondoka wasafiri kuelekea katika visiwa vilivyo karibu.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa wilaya amemuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma, Fidelica Myovella, kugawa viwanja maeneo salama kwa wakazi wote wanaoishi karibu na kingo za ziwa ambao nyumba zao zimefunikwa na maji.

"Wananchi ambao kwa bahati mbaya wamepatwa na janga la kufunikwa makazi yao kwa kujaa ziwa na ambao waliishi maeneo hayo kwa miaka mingi watagawiwa viwanja katika maeneo salama nje kidogo ya mji ili waweze kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa taifa," alisema.

Dk. Naano aliwataka wakazi waliovamia kingo za ziwa hilo na kujenga majengo katika maeneo yasiyopimwa kuondoka mara moja ili kuepuka madhara yatakayojitokeza ikiwamo kusombwa na maji katika kipindi hiki cha mvua nyingi katika ukanda huo.

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kote ulimwenguni, ziwa hilo limeathirika pia ambapo katika siku za karibuni limekuwa likibomoa kingo zake na kuelekea katika makazi ya watu na hivyo kusababisha kufunikwa nyumba zao.

# Waganga wa jadi wanolewa TB, ukoma

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA wa jadi watano na wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wamepatiwa mafunzo ya kutambua dalili za magonjwa wa kifua kikuu (TB) na ukoma kama moja ya kupambana na magonjwa hayo kwenye jamii.

Mafunzo hayo yametolewa kufuatia kuwapo wa mila potofu kwa wagonjwa wa kifua kikuu kukimbilia kwa waganga wa jadi kutibiwa kienyeji kwa madai kuwa wamerogwa, jambo ambalo lilikuwa ni hatari kwa afya na watu wanaowazunguka.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu wa TB na ukoma kutoka Halmashauri ya Mji wa Kahama, Mariamu Mabanga, alipokuwa akizungumza na wanahabari, na kusema wagonjwa wengi wanakimbilia kwa waganga wa jadi badala ya vituo vya afya.

Alisema kati ya hao, waganga wa jadi watano waliopatiwa mafunzo ya dalili za ugonjwa wa TB, waganga wawili pekee ndio wamekuwa wakitoa ushirikiano kwa watoa huduma wa afya kwa kutoa taarifa za wagonjwa wanaofika katika maeneo yao kupatiwa matibabu.

Aidha, Mabanga alisema ugonjwa wa TB na ukoma katika Halmashauri hiyo uko juu ukilinganisha na Halmashauri za Msalala na Ushetu kutokana na Hospitali ya Mji wa Kahama kutibu wagonjwa kutoka Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Nzenga, Geita pamoja na Shinyanga vijijini.

Alilipongeza shirika lisilo la kiserikali la SHDEPHA+ kuwapatia pikipiki za mataili matatu(bajaji) na pikipiki moja kwa ajili ya kufikia wagonjwa waliopo maeneo ambayo hayafikiki na kusaidia shughuli ya usambazaji wa sampuli.

Meneja Mradi wa TB SHDEPHA+, Mwinuka Ereneus, alisema Halmashauri ya Mji wa Kahama waliwapatia bajaji tatu na pikipiki moja katika Hospitali ya Wilaya, Kituo cha Afya Iyenze na Kituo cha Afya Mwendakulima, huku Msalala wakiwapatia bajaji nne na pikipiki moja maeneo ya Isaka, Segese, Lunguya na Chela.

Pia Ereneus alisema mkoani Geita Halmashauri ya Bukombe walipatiwa bajaji mbili na pikipiki tatu huku Halmashauri ya Mbogwe wakiwapatia bajaji moja na pikipiki tatu, vyote vikiwa na dhamani ya Sh. 96,000,000.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyumba kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258

**OFFICE FLATS FOR RENT MIKOCHENI ROSE GARDEN ROAD,** Each flat consist of 8 separate offices all of them being self-contained and one big reception area. The compound also a spacious Parking area a comes along with a Generator. Contact: 0686 172502

**HOUSE FOR RENT AT YATCH CLUB ROAD MASAKI,** A 5 bedrooms, 5 bathrooms, 3 storey beach view house which comes with a number of amenities such as generator, swimming pool and Full Air condition. Contact: 0686 172502

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTAN-

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

AMANI JOSEPH MFOI MKAZI WA WILAYANI KISHAPU MKOANI SHINYANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 200 AZY AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2017 MAENEO YA SHINYANGA MJINI.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA AMANI JOSEPH MFOI KWA SIMU NAMBA 0627-174937 AU 0765-853690.

**RB NAMBA KISH/RB/146/2019.**

21568702

---

**IN THECOURT OFDISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATIONCAUSE NO……OF 2020**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE KIZITO KALYALYA MPELLA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY GODFREY MPELLA KALYALYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the15 day of April, 2020.

Date at Dodoma this 25th day ofMarch, 2020

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT ............ MAGISTRATE

156872

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE**
**ILIYOPO TEMEKE**
**SHAURI LA MADAI NO. 10/2019**
**EDES T. MREMA**
**DHIDI YA**
**ABUBAKAR MOHAMED RAMADHANI**
**Kwa: ABUBAKAR MOHAMED RAMADHANI**

**KUITWA SHAURINI**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa tarehe 23/4/2020 saa 2:30 asubuhi, hivyo basi unatakiwa kufika hapa Mahakamani kwa tarehe na saa iliyopangwa hapo juu bila kukosa wewe mwenyewe au wakili wako ukiwa na vielelezo vyote vya kesi hii.
ANGALIZO: Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itaweza kutoa uamuzi/hukumu kuwa wewe umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 25/3/2020.

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE
DAR ES SALAAM.

115686902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo - MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;91/2020**

Ombi la SOPHIA SIXBERT DUWE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HARMINA SIMON DUWE.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/04/2020.

HAKIMU

156871

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DR. MARGARET NYAMBO anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili TZF 24 ROCSTA ASIA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No: 991081213787B.

115687302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**
**MADAI NAMBARI 18/2020**
**MDAI HONORATA KABUNDUGULU**
**DHIDI YA**
**MDAIWA JORAM KULONGWA**
**KWA JORAM KULONGWA**
**kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba madai ya TALAKA**

kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne 08/4/2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai haya na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 30/3/2020.

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE

215686502

---

## KUPOTEA KWA CHETI



115686702

**Hellena Thomas Mlemwa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1669/0032** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Mlamke. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **DR/KIJ/RB/198498/2020**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi Kwa*

*Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LIVERPOOL KUMRUDISHA STERLING




**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL inaweza kujaribu kumsajili tena Raheem Sterling miaka mitano baada ya kuondoka Anfield, kwa mujibu wa gazeti la Ufaransa la L'Equipe.

Sterling aliondoka Liverpool na kujiunga na Manchester City kwa ada ya pauni milioni 49 mwaka 2015.

Winga huyo alishutumiwa kwa mahojiano yake aliyofanya na BBC kuelekea kuondoka, ambapo alidai anafuata mataji na sio fedha.

Sterling amekuwa akizomewa na mashabiki wa Liverpool mara zote akicheza dhidi ya wekundu hao, lakini hivi karibuni alibainisha kwamba anavutiwa na molari ya klabu hiyo.

Wakati wa maswali na majibu live kutoka kwa wafuasi wake kupitia Instagram, mchezaji huyo wa kimataifa wa England aliulizwa kama atafikiria kujiunga tena na klabu hiyo.

Alijibu: "Nikiwa tu mkweli naipenda Liverpool. Mara zote wapo moyoni mwangu."

L'Equipe sasa limeripoti kwamba, Jurgen Klopp anaweza kufanya usajili wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mmoja wa wakilishi wa Sterling alibainisha kwamba mlango upo wazi kwa mchezaji huyo kuondoka kipindi cha majira ya joto.

Alisema: "Hata kama Raheem yupo Manchester City, lakini hajaisahau Liverpool, kwani pale ndio palipomtambulisha yeye kama mchezaji."

# Coutinho awa dili klabu za EPL

**LONDON,** England

MANCHESTER United imeripotiwa inaongoza dhidi ya klabu za Ligi Kuu ya England katika mbio za usajili wa Philippe Coutinho kutoka Barcelona kipindi hiki cha majira ya joto.

Coutinho ametumia msimu huu akicheza kwa mkopo pale Bayern Munich, ambako amefunga mabao nane katika mechi 22 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, lakini klabu hiyo haipo tayari kumsajili kwa mkataba wa kudumu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake pale Nou Camp, lakini inaonesha wazi kwamba hawezi kurudi Barca na anaweza kuondoka moja kwa moja.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, United inafikiria kumsajili Coutinho ili kuimarisha safu yao ya kiungo, licha ya kumpata Bruno Fernandes aliyeonesha kiwango cha kuvutia tangu aliposajiliwa wakati wa dirisha dogo la Januari.

United inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Leicester City, Chelsea na Tottenham Hotspur kwenye mbio za kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, lakini wanajiamini watashinda kwenye mbio hizo, licha ya kwamba alicheza pale kwa wapinzani wao wakubwa Liverpool.

Coutinho hivi karibuni alipoulizwa kama atakuwa tayari kurudi pale kwenye dimba la Anfield, alijibu kwamba kwa sasa yupo kwenye 'safari nyingine'.

Kocha wa zamani wa Liverpool, Brendan Rodgers, ambaye alimnoa Coutinho wakati akicheza pale Anfield, anatajwa kuvutiwa nae sana na anataka kumchukua akacheze Leicester City ambayo anainoa kwa sasa.



# Tottenham inajiamini kumbakisha Kane




**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham wanajua kwamba watakabiliwa na ushindani mkubwa kumbakiza Harry Kane mwishoni mwa msimu huu kama hawatafuzu kucheza Ligi ya mabingwa Ulaya.

Lakini Tottenham ambao wanamtaja mshambuliaji wao huyo kuwa na thamani ya pauni milioni 200, wanajiamini kwamba watambakisha klabu hapo mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

Kane aliibua shaka juu ya majaliwa yake pale Spurs Jumapili, alipobainisha kwamba hawezi kubakia klabuni hapo 'kwa sababu hiyo'. Lakini habari kwamba, Kane yupo tayari kufikiria kuhusu majaliwa yake kipindi cha majira ya joto hazijaja kwa mshangao hapo Tottenham, ambao wanajua vizuri hali halisi juu ya mshambuliaji wao huyo.

Kane, ambaye hajashinda taji lolote kwa jina lake akiwa klabuni hapo, ameshazungumza hadharani kuhusu nia yake ya kutaka kushinda mataji.

# Sergio asubiriwa kurudi Argentina

**BUENOS AIRES,** Argentina

KOCHA wa Klabu ya Independiente, Lucas Pusineri anataka kumrudisha Sergio Aguero jijini Buenos Aires kipindi hiki cha majira ya joto.

Pusineri anataka kuungana na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake pale Etihad, pamoja na kiungo wa AC Milan, Lucas Biglia.

Kiungo wa zamani Pusineri alicheza pamoja na Pusineri na Aguero wakati wa misimu yake miwili katika klabu hiyo ya nchini Argentina kati ya mwaka 2003 na 2006.

Pusineri ameliambia gazeti la Daily Mirror: "Nina uhusiano mzuri na Biglia na Kun Aguero.

"Tulikuwa wachezaji pamoja na nina heshima kubwa kwa kipindi chao walichocheza nchini Argentina na Ulaya.

"Litakuwa jambo zuri kama nikiwa nao hapa hata kesho. Kwa siku za usoni, nina matumaini makubwa kuwahesabu wao hapa."

Aguero awali alinukuliwa akibainisha mpango wake wa kumalizia kucheza soka katika klabu yake ya zamani ya Independiente.

Alisema: "Mara zote nitajaribu kurudi tena Argentina. Nawajua mashabiki wa Independiente wanachokitaka, lakini nina mkataba na City, na najaribu kujikita kwenye miaka yangu hii miwili iliyobaki.

"Halafu nitaangalia nini kitakachofuata, Rojo (Independiente) ndio kipaumbele changu."







# LIVERPOOL YAJITOA USAJILI WA SANCHO

**LONDON,** England

LIVERPOOL imeacha mlango wazi kwa klabu mbili za Manchester United na Chelsea baada ya kujiondoa kwenye mbio za kumsajili Jadon Sancho, kwa mujibu wa Daily Mail.

Nyota wa Borussia Dortmund, Sancho ni mtu ambaye amekuwa akitajwa kuwaniwa na miamba wa Ligi Kuu ya England baada ya kung'ara kwenye ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na kipindi hiki cha majira ya joto kitaleta vita kubwa ya kuwania saini yake.

Lakini kwa mujibu wa gazeti Mirror, Liverpool sasa imeamua kuachana na mpango wa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 na hivyo kuacha mwanya kwa United na Chelsea ambazo nazo zinawania saini yake.

Hata hivyo, klabu hizo zimebainisha kwamba, hazipo tayari kulipa kiasi sha pauni milioni 100 kinachotakiwa na klabu ya Dortmund. United imeripotiwa kuwa karibu na wakala wa Sancho, lakini bado hawajapeleka ofa yao kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo.

Wakati huo huo, ripoti zinadai kwamba, Chelsea imeanza ushawishi wa kujaribu kumsajili mchezaji huyo, ingawa imebainisha kuwa haitakuwa tayari kulipa ada ya pauni milioni 100 inayotakiwa.

Dortmund hivi karibuni ilibainisha kwamba, suala la Sancho kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto halipo mikononi mwao.

# *Manchester Utd yamtega de Ligt*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ipo tayari kutoa ofa kwa Matthijs de Ligt kuepuka mzunguko wa pale Juventus kama mlinzi huyo wa kimataifa wa Uholanzi ataendelea kuwa kwenye wakati mgumu kule nchini Italia.

De Ligt alikuwa mmoja wa wachezaji waliotajwa sana kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto kilichoita wakati alipokataa ofa ya klabu kadhaa na kuamua kujiunga na Juve kwa pauni milioni 67.5 baada ya kuiongoza Ajax kutinga nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, beki huyo mwenye umri wa miaka 20 ameshindwa kuzoea soka la Serie A kwenye msimu wake wa kwanza nchini Italia, na amepoteza namba kwa Merih Demiral kabla ya kuumia Januari.

United imekuwa ikifuatilia hali halisi pale Juve ili kuangalia uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo. United wanaimani kwamba wakala wa mchezaji huyo, Mino Raiola anauwezo wa kuharakisha usajili wa wateja wake na De Ligt anaweza kuwa sokoni kipindi kijacho cha majira ya joto au hivi karibuni.

United imekuwa na machaguo kadhaa kwenye safu yao ya beki wa kati kwa sasa baada ya kutumia pauni milioni 80 kumsajili Harry Maguire kipindi cha majira ya joto kilichopita ambaye anacheza pamoja na Victor Lindelof, Eric Bailly, Axel Tuanzebe au Phil Jones.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AITAKA BARCA NA PUYOL, CRUYFF

Mimi ni mtu wa timu, sitaki kuamua mwenyewe, ningependa kuingia na watu kutoka...

**DOHA,** Qatar

LICHA ya kuikataa nafasi ya kuinoa Barcelona Januari, mwaka huu, kiungo wa zamani wa miamba hiyo ya Camp Nou, Xavi Hernandez ambaye kwa sasa anainoa Al Sadd ya Qatar, ameelezea mipango yake ya kuwa kocha wa timu hiyo ya Hispania kwa baadaye.

**Xavi amewataja wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona, Carles Puyol na Jordi Cruyff kama watu anaowataka kufanya nao kazi kama atapewa nafasi ya kutimiza lengo lake la kuwa kocha wa miamba hiyo ya Camp Nou.**

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona mwenye umri wa miaka 40 kwa sasa, ameipa ubingwa Al Sadd kwa mara ya pili akiwa kama kocha wakati alipoiongoza kutwaa ubingwa kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Qatar Januari, mwaka huu ikiwa ni siku chache baada ya kuikataa ofa ya kuwa kocha wa Barcelona.

Wakati huo, Xavi alisema ilikuwa "mapema mno" kwake yeye kuwanoa mabingwa hao wa LaLiga, lakini katika mahojiano yake na Jarida la La Vanguardi aliweka wazi kuwa kocha wa Barca kupo sana katika mipango yake.

"Ni muwazi kwamba nataka kurudi Barca," alisema. "Nimefurahia sana.

"Sasa kwamba ninajiona binafsi nikiwa kocha, nadhani ninaweza kuchangia kitu kwa wachezaji.

"Lakini ninaweka hili wazi kwao kwamba nilijikuta katika mradi ambao ulianza kutoka mwanzo na katika uamuzi ambao ulikuwa wangu."

Xavi ambaye alitangazwa kocha bora wa mwezi Desemba na Januari, alishirikiana miaka 15 ya mafanikio Barcelona na Puyol na kwa pamoja walitwaa ubingwa wa LaLiga mara sita, Kombe la Mfalme [Copa del Rey] mara mbili, ubingwa wa Ulaya mara tatu, UEFA Super Cup na Kombe la Dunia mara mbili.

Cruyff nyakati zake hapo Camp Nou zilikuja katikati ya miaka ya 90, lakini Xavi alisema nyota huyo wa zamani wa Barca mwenye umri wa miaka 46, ambaye kwa sasa ni kocha mkuu wa Ecuador, anaweza kuwa chaguo lake la kwanza kama katibu wa ufundi.

"Ningependa kufanya kazi pamoja na watu ambao ninaimani nao, ambao kuna uaminifu, na ni watu gani halali," alisema Xavi. "Hakuna mtu anayeweza kuwa na sumu karibu na chumba chenye kufuli.

"Tunazungumza kuhusu Carles Puyol, ambaye alikuwa nahodha wa Barca, na Jordi Cruyff, biashara nzuri na uzoefu mkubwa katika ukatibu wa ufundi.

"Mimi ni mtu wa timu; sitaki kuamua mwenyewe. Ni wazi ningependa kushirikiana sana na kila mtu.

"Kwenye chumba cha kufungwa kunaweza kuwa hakuna uzembe, hakuna sumu. Ningependa kuingia na watu kutoka mazingira yangu kuunda timu nzuri."

## ZISIKUPITE

### UTD YAJIPANGA KWA DE LIGT

MANCHESTER United inaandaa ofa kwa beki wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt, 20, huku kiungo Mfaransa Paul Pogba, 27, akijiandaa kuondoka Old Trafford na kwenda njia nyingine. ***(Star)***

### EVERTON KWA BALE, RAMSEY

EVERTON inapanga kutoa ofa kabambe majira ya joto kwa mshambuliaji wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale, 30, na kwa kiungo wa Juventus, raia wa Wales, Aaron Ramsey, 29. ***(90min.com)***

### ARSENAL YAMTAKA TRAORE

ARSENAL inavutiwa na kiungo wa kimataifa wa Ivory Coast, Hamed Traore, 20, ambaye anacheza kwa mkopo Sassuolo akitokea Empoli, na kaka yake Amad, 17, anayecheza nafasi ya winga katika klabu ya Atalanta. ***(90min.com)***

### SANCHEZ KUITOBOA UNITED

MANCHESTER United inaweza kulazimishwa kumlipa mshambuliaji wa Chile, Alexis Sanchez, 31, kiasi cha pauni milioni 1.1 kama ada ya uaminifu kwa kila mwaka wakati atakaporejea kutoka Inter Milan anapocheza kwa mkopo. ***(Sun)***

### LIVER YAJITOA MBIO SANCHO

LIVERPOOL imejiweka kando katika mbio za kumsajili Jadon Sancho - hivyo kuiacha Manchester United na Chelsea kama klabu mbili za Ligi Kuu England zinazowania nyota huyo wa kimataifa wa England. ***(Daily Mirror).***

### AJAX YAACHANA NA NOURI

AJAX imefuata mkataba wa Abdelhak Nouri ikiwa ni siku chache baada ya kunusurika kifo. ***(De Telegraaf)***

### ANCELOTTI KUIPAISHA EVERTON

KOCHA Mkuu wa Everton, Carlo Ancelotti, ameripotiwa kutaka kufanya usajili wa nyota wakubwa katika majira ya joto ili kumsaidia katika kuufanya mradi wake hapo Goodison Park kuwa wa daraja la juu na akitaka kupaisha klabu hiyo nafasi sita za juu. ***(90min.com)***

### KUMFUATA GIROUD

INTER Milan na Lazio zinajiandaa kuingia vitani kuisaka saini ya mshambuliaji wa Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, ambaye ana mabao matatu katika mechi 13 alizocheza msimu huu. ***(Tuttosport)***

### CHELSEA HESABU NA CUCURELLA

CHELSEA ipo tayari kumsajili beki wa pembeni wa Getafe, Mhispania Marc Cucurella, 21, majira haya ya joto kwa pauni milioni 23. ***(Diario Sport - in Spanish)***

### ARSENAL JICHO KWA FEKIR

KLABU ya Arsenal inaonekana kufikiria kumsajili Nabil Fekir ambaye walijaribu kumuwania mwaka jana na sasa wanapanga kumchukua kutoka kule Real Betis ya Hispania. ***(Daily Star)***

### GOMES MTEGONI MADRID

REAL madrid inataka kumsajili kiungo Mbrazili Igor Gomes, 21, ambaye anaweza kuigharimu pauni milioni 45 kutoka pale Sao Paolo. ***(AS - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA YATANGAZA RASMI KUMWANIA NDEMLA

Na Somoe Ng'itu

KATIKA kuhakikisha inakuwa na kikosi imara katika msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, uongozi wa Polisi Tanzania umesema unajiandaa kuwasilisha ofa ya kumsajili kiungo wa Simba, Saidi Ndemla, imefahamika.

Taarifa za ndani zinasema Ndemla ambaye aliwahi kufaulu majaribio ya kujiunga na klabu ya AFC Eskilstuna amekataa kusaini mkataba mpya Simba kutokana na kujiandaa kuelekea Sweden kujiunga na klabu hiyo akiwa mchezaji huru baada ya awali kushindwa kulipa dau walilotakiwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema tayari kocha mkuu wa timu hiyo amebainisha kumhitaji Ndemla ambaye mkataba wake na Simba unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu.

**Munisi alisema anaamini wakifanikiwa kupata saini ya kiungo huyo, kikosi chao kitaimarika zaidi katika eneo la katikati na hivyo kujiweka vizuri kwenye kukabiliana na ushindani.**

"Tunajiandaa kukutana na wasimamizi wa Ndemla, ni mchezaji ambaye akikubali kutua Polisi Tanzania atapata nafasi ya kucheza, huko aliko amebanwa sana, tutaangalia pia mahitaji yake mengine kama mchezaji mwenye kipaji," alisema Munisi.

Kiongozi huyo aliongeza Polisi Tanzania haitakuwa na kizuizi endapo nyota huyo atapata klabu ya kuichezea nje ya nchi kama ambavyo ndoto za wachezaji wengi zilivyo.

"Tunajua anatamka kwamba huu ni wakati sahihi kwake kwenda Ulaya, lakini hujui Mungu amemwandikia nini, tutafanya mazungumzo naye na mkataba wetu tutazingatia matarajio yake ya baadaye," Munisi alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Polisi Tanzania iko nafasi ya sita ikiwa na pointi 46 baada ya kucheza mechi 29 huku vinara wa ligi hiyo wakiwa ni Simba na pointi zao 71 wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 huku Yanga ikishika nafasi ya tatu baada ya kufikisha pointi 51.

## Mwadui wajifua kupitia WhatsApp

Na Shufaa Lyimo

ILI kulinda viwango vya wachezaji wake, Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amesema ameanza kuwapa nyota wake programu za mazoezi kwa njia ya simu katika kipindi hiki cha kuepuka msongamano ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19).

Adam aliliambia gazeti hili jana kuwa amechukua uamuzi huo ili kuwaleta wachezaji wake karibu na kuwaweka tayari na ligi ambayo wakati wowote inaweza kurejea.

"Ninawapa wachezaji wangu programu maalumu za mazoezi kwa njia ya WhatsApp na kila kitu kinakwenda vizuri, ninataka kuona wanaimarika na kujiweka tayari na mapambano ya mwisho," alisema Adam.

Kocha huyo alisema wachezaji wake hawatafanya mazoezi magumu kwa sababu huu si wakati wake na anaamini programu anazowapa zitawaimarisha.

"Huu si wakati wa mazoezi magumu, ni wakati wa kufanya mazoezi mepesi mepesi ili kuiweka vizuri miili yao isikakamae," Adam alieleza.

Aliongeza atawafanyia vipimo maalumu mara tu watakaporejea kambini ili kujua hali yao ya kiafya kabla ya kuanza tena mechi za ligi.



## Konde Star FC yalia na ukata

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

UONGOZI wa Konde Star FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba umesema timu yao imefanya vibaya katika msimu huu kutokana na kusajili wachezaji wasiokuwa na uwezo wa kushindana, imeelezwa.

Timu hiyo Kongwe inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba inayoshirikisha klabu 18, ikiwa na pointi tatu baada ya kucheza michezo 13.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa timu hiyo, Masoud Seif Salum, alisema wachezaji waliosajiliwa walishindwa kwendana na kasi ya ligi hiyo ambayo ina ushindani katika kila mechi.

Salum alisema walishindwa kusajili wachezaji wazuri na wenye viwango kutokana na changamoto ya fedha waliyonayo ambayo ilisababisha kusajili wachezaji "wa kawaida".

"Tumeanza vibaya ligi, hatujashinda hata mchezo mmoja kati ya michezo 13 tuliyocheza, hii inatokana na kukosa wachezaji wenye viwango vya juu ikiwamo katika safu ya ulinzi na hata ushambuliaji," alisema Salum.

Hata hivyo, alisema matumaini yao ni kuona wachezaji wanaongeza juhudi kupambana ili kubaki katika ligi hiyo licha ya changamoto ya fedha waliyonayo.

'DONGO'...




Kiungo mshambuliaji wa klabu ya Yanga, Bernard Morrison, humwambii kitu kwa ugali wa dona ('dongo'), hapa akiwa na sahani yenye msosi huo ambayo ameiposti mtandaoni na kuiandikia ujumbe "unakaribishwa kwa nyumba yangu katika msimu huu wa karantini". **PICHA: MTANDAO**

## *Namungo yajivunia kutimiza malengo*

Na Saada Akida

UONGOZI wa Namungo FC umesema timu yao ambayo iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imevuka malengo waliyojiwekea msimu huu wa 2019/20, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alisema nafasi waliyopo sasa ni nzuri na mwelekeo wanaokwenda nao katika mechi zilizobaki za msimu huu ni mzuri.

Zidadu alisema malengo yao wakati msimu unaanza yalikuwa ni kupambana na kumaliza kwenye nafasi 10 za juu, nafasi ambayo ingewahakikishia kubaki kwenye ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

"Hata katika makubalino yetu tulipoingia mkataba na Kocha Thiery Hitimana, tulimweleza tunahitaji kumaliza katika nafasi nzuri ambayo tutaendelea kubaki kwenye ligi, hilo amelifanikisha na kupata kibali cha kuendelea kukinoa kikosi chetu," alisema Zidadu.

Kiongozi huyo alisema walimpa sharti kocha huyo kama timu isingefikia malengo hayo, nafasi ya kuendelea kukinoa kikosi chao ingeishia njiani.

"Sasa timu yetu imevuka malengo, kutoka nafasi ya 10 tuliyojiwekea hadi ya tano, ni hatua kubwa, nina imani kwa mwenendo mzuri wa timu yetu kwa michezo iliyobaki dhidi ya Yanga na Azam FC ni kuongeza umakini ili timu hizo zisituharibie," alisema Zidadu.

Namungo yenye pointi 50 ipo katika nafasi ya nne baada ya kucheza michezo 28 wakati Yanga inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama 51 ikicheza michezo 27 wakiwa nyuma mchezo mmoja dhidi ya Azam iliyoko nafasi pili wakiwa na pointi 54 na vinara Simba pointi 71.

# Michezo

Alhamisi Aprili 2, 2020

Nipashe



Xavi aitaka Barca na Puyol, Cruyff UKURASA 30



Nahodha wa Simba, John Bocco akifunga moja kati ya mabao matatu aliyofunga msimu huu. Bocco amewahahikishia mashabiki wa timu hiyo kutetea ubingwa wao bila presha. **PICHA: MAKTABA**

## Bocco atuliza mzuka Simba

**Na Somoe Ng'itu**

ZIKIWA zimebakia wiki mbili ili kufahamu hatima ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imesimama ili kuepuka maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19), nahodha wa Simba, John Bocco, amewatoa mashabiki wao hofu kwa kuahidi kikosi chao kitatekeleza kwa vitendo ahadi ya kutetea taji wanalolishikilia.

Bocco aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wote wanaendelea na mazoezi binafsi, kwa sababu wanaamini ligi itakaporejea, kutakuwa na ushindani zaidi. Nahodha huyo alisema ushindani utaongezeka kutokana na idadi ya michezo iliyobaki kuwa michache na kila timu ikihitaji kuvuna pointi na kutimiza malengo.

"Hatutaki kusema mengi, tutawaonyesha, hatutaki kuahidi ila tumejipanga kuonyesha vitendo, tutapambana," alisema kwa kifupi nahodha huyo.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema benchi la ufundi linawasiliana na wachezaji wote ili kufahamu hali zao na hii ni kutaka kufahamu utimamu wao.

"Tunawahimiza kutobweteka, hii itasaidia kulinda viwango vyao na kasi tuliyokuwa nayo kabla ligi haijasimama, huko mbele tunatarajia mambo yatakuwa magumu zaidi," alisema meneja huyo.

Simba inayoongoza ligi ikiwa na pointi 71, imebakiza mechi 10 na inahitaji pointi 14 tu ili kufikisha 85 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine msimu huu na kutetea ubingwa wao. Vinara hao wanaofundishwa na Mbelgiji Sven Vandenbroeck na nahodha wa zamani wa klabu hiyo, Suleiman Matola pia wametinga katika hatua ya nane bora ya mashindano ya Kombe la FA, ambayo bingwa wake kupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Yanga yatua AS Vita kwa Kisinda

## ●●● Uongozi wasema ni straika chaguo la kwanza kwa Eymael ambaye anataka kumuunganisha na...

**Na Saada Akida**

HUKU uongozi wa klabu ya Yanga ukihakikisha unajipanga kwa kukijenga kikosi chao kuwa imara kuelekea msimu ujao, tayari umeingia katika mbio za kuinasa saini ya mshambuliaji wa AS Vita ya DR Congo, Tuisila Kisinda mwenye uwezo pia wa kucheza kama winga wa kulia, imefahamika.

**Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jijini jana kutoka ndani ya Kamati ya utendaji ya klabu hiyo, zimeeleza kwamba mshambuliaji huyo ni miongoni mwa majina ambayo yamependekezwa na bosi wa benchi la ufundi wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael.**

Mjumbe huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema Kisinda ni miongini mwa majina ambayo yalipendekezwa katika ripoti ya kocha huyo na kamati ya usajili kwa kushirikiana na mdhamani ili kuhakikisha mchakato huo unakamilika.

"Ni kweli Kisinda ni miongoni mwa nyota ambaye jina lake linajadiliwa katika kamati husika huku tukiangalia mikataba yake na klabu yake ya sasa, kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya kuinasa saini yake," alisema Kigogo huyo.

Alisema Eymeal amehitaji washambuliaji wawili, hivyo wana imani wakifanikiwa kupata huduma ya nyota huyo tatizo la safu ya ushambuliaji litakuwa limeisha ndani ya kikosi cha Yanga.

Kigogo huyo alisema mipango ya Kamati ya Utendaji kushirikiana na mdhamini wao huyo ni kuhitaji kujenga kikosi cha Yanga kwa kuimarisha hasa safu ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikijisuasua kwa msimu huu kutokana na mabao machache iliyofunga ukilinganisha na wapinzani wao, Simba.

Wakati huo huo Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema hakuna kisichowezekana kwa klabu hiyo kumnasa nyota huyo na kwamba ipo mikakati madhubuti ya kuhakikisha wanafanya usajili wa wachezaji watakaoimarisha kikosi cha timu yao.

Nugaz alisema uongozi umejipanga kuimarisha kikosi chao ili msimu ujao warejee kwenye ushindani katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine watakayoshiriki kwa msimu ujao.

Hadi Ligi Kuu inasimama kutokana na kuepuka maambukizi ya virusi vya corona, Simba ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 71, huku pia ikiongoza kwa mabao ya kufunga 63 na machache ya kufungwa 15, wakati Yanga iliyopo nafasi ya tatu na alama zake 51, imecheka na nyavu mara 31 tu na kuruhusu nyavu zake kutingishwa mara 20.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >